Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 23 Aprili, 2008

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)Alisoma Dua*

## D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaanza agenda za kikao chetu asubuhi hii ya leo ninaomba kwa heshima na taadhima nitambue uwepo wa Mheshimiwa Samwel Sitta, Mbunge wa Jimbo la Urambo Mashariki, katika kiti chake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mbunge wa Urambo Mashariki karibu sana katika Shughuli za Bunge kwa asubuhi hii ya leo. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 146

### Ahadi ya Kufanya Iramba Mashariki Kuwa Wilaya

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza:-

Kwa kuwa, tarehe 23/09/2005 Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete pamoja na ahadi nyingine aliahidi kuwa, Iramba Mashariki itakuwa Wilaya; na kwa kuwa, tarehe 23/07/2007 aliyekuwa Waziri Mkuu Mheshimiwa Edward Lowassa wakati akiongea na wananchi wa Iguguno aliahidi kuwa, Iramba Mashariki itapewa Halmashauri ya Wilaya kwanza na baadaye kuthibitisha kauli hiyo kwenye Kikao cha RCC cha tarehe 24 Julai, 2007 Mkoani Singida kwa kueleza kuwa, Iramba Mashariki imetimiza masharti yote.

Kwa kuwa, kigezo cha Serikali kutokuwa na fedha kimeshafahamika kwa wananchi na wako tayari kuisaidia Serikali kwa kufyatua matofali na hata kuanza kujenga kwa maelekezo ya Mainjinia:-

Je, Serikali inasemaje juu ya hatua hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkutano wa Kwanza wa Bunge lako Tukufu nilijibu swali Na. 37 la Mheshimiwa Mgana Msindai linalofanana na swali hili. Nilieleza kwamba uundwaji na ugawaji wa maeneo mapya ya kiutawala hapa nchini unatawaliwa na Sheria ya Serikali za Mitaa Na. 7 (Mamlaka za Wilaya) na Sheria Na. 8 (Mamlaka za Miji) za mwaka 1982 na Sheria ya Taratibu za Uanzishwaji wa Mikoa na Wilaya Na. 12 ya mwaka 1994 pamoja na vigezo vilivyowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Iramba ni mojawapo ya Wilaya za Mkoa wa Singida ambayo idadi ya wakazi wake imekua ikiongezeka kwa kasi mwaka hadi mwaka. Kwa mujibu wa Sensa ya Mwaka 2002 Wilaya ya Iramba ilikuwa na watu 367,036 na eneo lenye kilometa za mraba zipatazo 7,900.

Kwa kuzingatia sababu hizo Mkoa wa Singida kwa kupitia Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) kilichofanyika tarehe 10/11/2006 kilipitisha azimio na kuwasilisha ombi Serikalini kwa ajili ya kuzigawa Wilaya za Mkoa wa Singida ikiwemo Wilaya ya Iramba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tarehe 25/9/2005 Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete wakati huo akiwa mgombea Urais kwa Chama cha Mapinduzi (CCM) pamoja na ahadi nyingine alizungumzia suala la umuhimu wa kuigawa Wilaya ya Iramba kuwa katika sehemu mbili za kiutawala.

Hata hivyo, Mheshimiwa Rais hakuahidi Iramba Mashariki kuwa Wilaya. Alichosema Mheshimiwa Rais ni kwamba atapokea maombi ya kuifanya Iramba Mashariki kuwa Wilaya na kuyashughulikia maombi hayo pamoja na maombi ya Wilaya zingine kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa na Serikali na pia uwezo wa Serikali (Kiuchumi) wa kuanzisha maeneo mapya ya utawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wananchi kuwa tayari na kuisaidia Serikali kwa kufyatua matofali na hata kuanza kujenga kwa maelekezo ya Wahandisi kama hatua ya kuharakisha maendeleo ni suala hili ni zuri na ni mwamko wa kupongezwa. Hata hivyo, ikumbukwe kuwa uanzishwaji wa Wilaya au Halmashauri unahusu sio tu ujenzi wa majengo lakini kunahitaji pia kuweka raslimali watu ikiwa ni pamoja na uongozi wa Wilaya, Halmashauri na watumishi wengine watakaohitajika na kuboresha miundombinu na mambo mengine. Hivyo, Serikali itaendelea kugawa maeneo mapya kwa awamu kadri itakavyoamuliwa kulingana na uwezo uliopo kifedha.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa sheria alizozisema Mheshimiwa Waziri hapa tunazifahamu na mimi nimeshatafakari hata kwa wananchi wa Iramba Mashariki. Na kwa kuwa watu wa Iramba Mashariki wanaomba Wilaya kwa sababu ya matatizo wanayoyapata huduma za matibabu wanakwenda Mkoa wa Manyara yaani Wilaya ya Mbulu. Wananchi wa Iramba Mashariki wanashindwa kwenda Makao Makuu ya Wilaya yao kwa sababu ya umbali na usafiri. Je, Waziri haoni kwamba kilio cha watu wa Iramba Mashariki ni kikubwa kuliko sababu alizozitaja hapa?

Swali la pili. Kwa kuwa wananchi wako tayari kwa uchungu kuisaidia Serikali kufanya kazi zote zinazohusu ili kuanzishwa Wilaya. Sasa Serikali itaahidi kwamba itakapogawa Wilaya sasa au wakati unaokuja Iramba itakuwa mojawapo?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vitezo ambavyo vinatumika katika kugawa Wilaya ni kama vifuatavyo. Eneo linatakiwa liwe na *square kilometre* za mraba 5,000 na Iramba Mashariki ina *square kilometre* 3,939. idadi ya wakazi wawe 1,000 na zaidi. Iramba Mashariki ina wakazi wapatao takribani 1,071. Tarafa zinatakiwa ziwe 5 na kuendelea mbele. Iramba Mashariki ina Tarafa 3 tu. Kata zinatakiwa ziwe 15 na kuendelea. Lakini Iramba kwa ujumla ina Kata 26 kwa hiyo ukizigawa zitakuwa Iramba Mashariki Kata 13 na Iramba Magharibi Kata 13.

Kwa hiyo kuna baadhi ya vigezo ambavyo Iramba Mashariki ime-*qualify* kuigawa lakini kuna baadhi ya vigezo bado havijafikiwa. Kwa hiyo tunaangalia zaidi vigezo na zipo Wilaya ambazo zina vigezo vilivyofikiwa Iramba ina baadhi tu ya vigezo ambavyo vimefikiwa kisheria.

Kwa upande wa wananchi kuwa tayari. Kama nilivyojibu kwenye swali la msingi pamoja na kwamba wananchi wanaweza wakawa na moyo wa kujenga maboma, nyumba lakini tatizo lipo pale pale kwamba kuanzisha Wilaya sasa hivi gharama yake ni takriban kuanzia shilingi bilioni 2 mpaka bilioni 4. Sasa hata kama wananchi watajenga maboma lakini kuna mahitaji mengine ya kiutawala kama vile watu, watumishi, miundombinu na kadhalika. Kwa hiyo, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwamba maeneo ya utawala yataendelea kugawanywa kulingana na uwezo wa Serikali. Kwa sasa hivi tunamaliza kwanza yale maeneo yaliyogawanywa kiutawala ambayo bado hatujamaliza hata miundombinu yake. Mnafahamu Wilaya mpya kama Kilindi ndiyo imeanza kujengwa sasa hivi, Ruangwa ndiyo imeanza kujengwa. Kwa hiyo tunaona kwamba ni busara tumalize kwanza hizo Wilaya ambazo ziko tayari tumeshazigawanya ndipo tuanze kugawa maeneo mengine ya utawala. (*Makofi)*

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa vigezo anavyovisema Mheshimiwa Naibu Waziri vimetimizwa kabisa na Halmashauri ya Wilaya ya Singida na kwa maana hii kutoka mpaka wa Singida Kaskazini ambako ni Mlima Hanang hadi mpaka wa Manyoni kuna zaidi ya kilomita 200. Na kwa kuwa itakuwa rahisi zaidi kuanzisha Halmashauri ya Wilaya kabla ya

kufikia mchakato wa kuanzisha Wilaya.  Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba Ilongelo sasa itangazwe kuwa Halmashauri ya Wilaya kwa ajili ya kuzifanya ziwe mbili katika Singida Vijijini?  (*Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli naomba nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba Wilaya ya Singida Vijijini ni kubwa na kuna vigezo vingi ambavyo imefikia kisheria.  Lakini kama nilivyosema kwa sasa ni kwamba tunamaliza kwanza zile Wilaya ambazo tumeshazigawa na baadaye ndipo tutaingia kwenye mchakato wa Wilaya nyingine ambazo zimefikia vigezo hivyo.

Wilaya ziko nyingi, ziko Wilaya kama 37 hivi ambazo zina vigezo kabisa vya kuanzishwa Wilaya mpya, Wilaya ya Singida ni mojawapo kati ya Wilaya hizo.

Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge awe na subira hali ya fedha ikiwa nzuri Wilaya zitagawiwa kulingana na uwezo wetu kifedha.  (*Makofi*)

Na. 147

**Mji wa Nzega Kuwa Halmashauri ya Mji**

**MHE. LUCAS L. SELELII** aliuliza:-

Kwa kuwa Mji wa Nzega ambao ni Makao Makuu ya Wilaya ya Nzega unakidhi viwango vyote vya kuanzishwa Halmashauri ya Mji:-

(a) Je, ni utaratibu gani unaochukuliwa na Serikali kufanikisha azma hiyo?

(b) Je, Serikali ipo tayari kuupandisha hadhi Mji wa Nzega ili katika uchaguzi wa 2009 na 2010 uwe ni Halmashauri ya Mji?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii, Mbunge wa Nzega, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji Mdogo wa Nzega ulitangazwa na Serikali kupitia Tangazo lake la tarehe 17 Septemba, 2004 na baadaye Mamlaka ya Mji huu Mdogo kuzinduliwa rasmi tarehe 20 Aprili, 2007.  Kwa mujibu wa kifungu cha 20 cha Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Namba 7 ya mwaka 1982, Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa ndiye mwenye Mamlaka ya kuanzisha Halmashauri ya Mji.  Katika kutekeleza maelekezo hayo ya kisheria, Waziri atatoa

maelekezo ya kuzingatiwa kwa vigezo ili kuwezesha Mamlaka ya Mji Mdogo kupandishwa hadhi kuwa Halmashauri ya Mji. Vigezo vya uanzishwaji wa Halmashauri ya Mji vinavyotumika na ambavyo vinazingatia Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 ni:-

(i) Eneo la Mji Mdogo kuwa na wakazi wasiopungua 30,000.

(ii) Mji Mdogo kuwa na eneo la ardhi linaloweza kukidhi mahitaji mbalimbali.

(iii) Uwezo wa eneo kujiendesha wenyewe, yaani liwe na uwezo wa kukusanya mapato kutokana na vyanzo vyake yanayoweza kukidhi zaidi ya asilimia 50 ya bajeti yake kwa mwaka.

(iv) Kuwepo kwa miundombinu inayokidhi utoaji wa huduma mbalimbali za kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna baadhi ya vigezo nilivyovitaja hapo juu vinakidhi mahitaji kwa eneo hilo la Nzega kupandishwa hadhi kuwa Halmashauri ya Mji. Lakini kwa mwaka 2005, Serikali ilitafakari uwezekano wa maelekezo kwa uongozi wa Mkoa wa Tabora kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Nzega kuingiza Kata za Ijanija, Itilo, Nzega Ndogo na Migua katika eneo la Kata ya Nzega Mjini ambalo lilitangazwa kuwa Mji Mdogo.

Maelekezo hayo ambayo Mkoa na Halmashauri hazijatekeleza hadi sasa, yamo kwenye barua (Kumb. Na. HA. 131/395/01) ya tarehe 10 Juni, 2005 na ambayo Mheshimiwa Mbunge alipewa nakala; mpaka sasa hivi utekelezaji wa maagizo haya haujafanyiwa kazi. Utaratibu wa kuanzisha Halmashauri yoyote nchini unaanzia katika Halmashauri husika katika vikao vyake vya Mkoa na baadaye Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kufuatilia utekelezaji wa suala hili la kuanzisha Halmashauri ya Mji wa Nzega. Natoa agizo kwa uongozi wa Mkoa na Halmashauri ya Wilaya ya Nzega kurejea maelekezo hayo ya Serikali na kuyafanyia kazi kwa ukamilifu kama ilivyoshauriwa na baadaye kuwasilisha Ofisi yangu itafanyiwa kazi na kuchukuliwa hatua zinazofaa.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo ya Naibu Waziri bado nasikitika vikwazo vyote hivi havijafanywa na Halmashauri ya Nzega bali vinakwamishwa na Serikali Kuu yenyewe kutoa agizo au kutoa maelekezo ya kukubali Nzega kuwa Halmashauri ya Mji.

Je, Waziri sasa anatoa ahadi kwa sababu wakati ule 2005 anasema ni wakati wa Uchaguzi, hivyo isingekuwa sahihi kuanza kugawa wakati wa Uchaguzi umeshafika. Waziri anatoa maelekezo gani ili Uchaguzi ujao wa 2009/2010 Halmashauri ya Nzega iwe tayari ni Halmashauri inayojitegemea?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali sio kikwazo kwa uanzishwaji wa Halmashauri ya Mji ya Nzega. Kwanza Serikali ilitangaza Mji Mdogo wa Nzega mwaka 2004. Utekelezaji wake Halmashauri ya Mji Mdogo utekelezaji umeanza mwaka 2007. Mpaka sasa hivi Mji Mdogo wa Nzega haujafanya kazi kwa muda hata wa mwaka mmoja. Kwa hiyo, hata ile Mamlaka ya Mji Mdogo ule utendaji wake wa kazi mpaka sasa hivi huwezi ukaupima kwa uzuri zaidi.

La pili, kama nilivyosema kwamba masuala ya uanzishwaji wa Miji unaanzia kwenye Halmashauri husika tulitoa maelekezo kwenye Halmashauri husika kwamba waingize baadhi ya Kata kwenye Mamlaka ya Mji Mdogo ili walete hayo mapendekezo katika Ofisi yetu. Mpaka sasa hivi hawajafanya hivyo na sisi tunaheshimu sana maamuzi ya Halmashauri husika iwapo watafanya hivyo Serikali itakuwa tayari kuwasaidia, lakini wakicheleweshsha ina maana kwamba hatuwezi tukafanya lolote kwa sababu mambo yote yaanzia katika ngazi za Halmashauri zenyewe.

Na. 148

**Dawa Zinazoteketezwa Kwa Kuisha Muda Wake na Matumizi**

**MHE. JANETH M. MASSABURI** aliuliza:-

Kwa kuwa, *Medical Stores Department* (MSD) imekuwa ikilalamikiwa na wananchi ambao hawana uwezo wa kupata huduma za afya kwenye hospitali binafsi; na kwa kuwa, kumekuwa na uteketezaji wa dawa hizo kwa sababu za muda wa kutumia dawa hizo kuisha.

(a) Je, kwa nini dawa hizo hazikutumika wakati maeneo mengi kwenye hospitali na zahanati hapa nchini hazina dawa?

(b) Je, ni kiasi gani cha dawa kimeteketezwa kwa mwaka 2006/2007 na ni aina gani ya dawa hizo?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuleta marekebisho ya sheria ambayo itaboresha Idara ya *MSD* ili kuleta mfumo mzuri wa ugawaji wa dawa wenye kuleta tija?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, dawa ambazo hazikutumika hadi muda wake kwisha ni zile ambazo muda wake wa kutumika ulikuwa mfupi zilipoingizwa nchini au zile zilizoharibika kabla ya kuagizwa na kusambazwa kwenye zahanati, vituo vya afya na hospitali za umma. Orodha ya dawa, vifaa tiba, kemikali na vitendanishi vilivyoharibika tayari imeandaliwa kwa ajili ya kuombewa kibali cha kuteketezwa. Kwa kuwa orodha hiyo ni kubwa sana sio rahisi kuisoma hapa, namwomba Mheshimiwa Mbunge tuwasiliane ili aweze kuiona.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2006/2007 hakuna dawa, vifaa tiba, kemikali na vitendanishi kutoka *MSD* vilivyoteketezwa. Uteketezaji wa bidhaa hizo hufanyika baada ya kupata kibali cha Hazina. Aidha, kati ya mwaka 2000/01 na 2005/06 thamani ya dawa, vifaa tiba, kemikali na vitendanishi vilivyoharibika kabla ya kutumika ni shilingi 1,280,806,885.42.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, malalamiko mengi juu ya *MSD* ni ya kiutendaji ni siyo juu ya sheria iliyounda *MSD.* Aidha, Serikali bado haijaona kasoro za kisheria zinazotakiwa kufanyiwa marekebisho katika kuimarisha utendaji wa *MSD.* Kwa sababu hiyo, kwa sasa Serikali haina mpango wa kuwasilisha Bungeni marekebisho yoyote ya Sheria ya *MSD.* Badala yake, Serikali kupitia Wizara yangu inashughulikia hatua za kuboresha na kuimarisha utendaji wa *MSD* ili kuboresha mfumo wa upatikanaji na usambazaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika zahanati, vituo vya afya na hospitali za umma.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa wananchi wengi Mkoa wa Dar es Salaam na hasa pembezoni hupata taabu katika kutafuta huduma za afya na ukizingatia hospitali zinazotegemewa pale ni Amana, Mwananyamala na Temeke. Je, ni lini Serikali itaenda kuboresha zilizopo maeneo ya vijijini kwa kuzijengea uwezo na hasa ukizingatia matibabu na dawa hazipatikani kwa uhakika?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti**,** ni kweli kwamba kumekuwa na msongamano wa wagonjwa Hospitali za Dar es Salaam. Lakini kama tulivyokuwa tukizungumza hapa Bungeni tunao Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi ambao utaanza rasmi mwaka 2008/2009. Kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine watambue kwamba tukianza Mpango huo wa Maendeleo ya Afya ya Msingi basi huduma zote za vijijini zitaboreka kuanzia ngazi ya Kata, Wilaya na hadi kufikia Mkoa kwa maana hiyo msongamano wa Amana, Mwananyamala na Ilala utapungua.

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Kwa vile utendaji wa *MSD* hauridhishi na kwa kuwa ushindani wa biashara siku zote unaleta ufanisi zaidi kwa nini hatuwaruhusu Waganga Wakuu wa Wilaya kununua vifaa na madawa popote pale wanapovipata kwa bei za kuridhisha ili kufanya ushindani na *MSD.?*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna matatizo ya *MSD* kwamba dawa nyingine hazifiki. Lakini sasa hivi wakati tunaangalia jinsi gani ya utendaji mzuri wa *MSD* Wizara inafikiria kuanza kutenga kiasi cha fedha ambazo zinakwenda *MSD* ziwapatie Waganga Wakuu kiasi cha asilimia 30 ili waweze kununua dawa wakati wakiwa wanasubiri dawa kule *MSD?*

Na. 149

**Walemavu wa Ugonjwa wa Ukoma**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa, kwenye kijiji cha Sukamahela Kata ya Solya Tarafa ya Kilimatinde Wilayani Manyoni kuna kituo na nyumba zilizojengwa na Serikali kwa ajili ya watu walioathirika na ugonjwa wa ukoma ambao baadhi yao hawana viungo kama vidole na kadhalika; na kwa kuwa, licha ya kujengewa nyumba hizo hakuna huduma endelevu ya mahitaji ya msingi:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kukitambua rasmi kituo hicho?

(b) Kwa kuwa, wengi wao ni wazee sana, ambao hawawezi kujihudumia hivyo, kukaa barabarani ili kuomba misaada kwa wapitaji hali inayohatarisha maisho yao kwa kugonga, kuliwa na wanyama wakali, adha ya jua, mvua na kadhalika. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwapa huduma ya mahitaji ya msingi, kama vile chakula, nguo, matibabu, ukarabati wa nyumba zao na kadhalika?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, makazi ya Sukamahela yaliyoko Wilayani Manyoni ni miongoni mwa makazi yanayoendeshwa na Serikali chini ya Idara ya Ustawi wa Jamii. Serikali inawapatia wakazi wa Sukamahela huduma zote za msingi ikiwa ni pamoja na chakula, malazi na matibabu. Katika mwaka wa 2006/2007 Serikali ilitumia jumla ya shilingi 11,571,588 kwa ajili ya chakula cha wakazi wa Sukamahela na shilingi 1,100,000/= zilitumika kwa ajili ya huduma za matibabu. Mwaka huu wa fedha (2007/2008) Serikali imekwishatumia hadi sasa shs. 5,146,000/= kwa ajili ya chakula.

Serikali inalifahamu tatizo la uchakavu wa majengo ya Sukamahela na kwa kutambua hilo imetenga kiasi cha shilingi 110,000,000/= mwaka 2007/2008 kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya Sukamahela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kuwa kutokana na ufinyu wa bajeti ya Serikali; fedha zinazotengwa kwa ajili ya huduma hii ni

ndogo na hivyo kutoweza kutosheleza mahitaji yote. Kwa kuwa kimsingi jukumu la kuwatunza watu wasio na uwezo ni la jamii husika, na kwa kuwa walemavu hawa wa ukoma ni sehemu ya jamii ya wakazi wa Halmashauri ya Manyoni, namwomba Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na Halmashauri ya Manyoni kuona jinsi ya kuwasaidia walemavu hawa hususan katika maeneo ambayo bajeti ya Wizara yangu haitoshelezi.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

La kwanza kwa kuwa huduma hii inayopelekwa Sukamahela inatoka Wizarani kwenda moja kwa moja kwenye kituo husika bila kushirikisha Halmashauri ya Wilaya na Wilaya husika. Je, Serikali haioni sasa kuna kila sababu ya kushirikisha Wilaya na Halmashauri kufuatilia kile kinachopelekwa ili kiweze kufika chote kuliko ilivyo sasa chakula kingine hakifiki.

Kwa kuwa kituo hicho pamoja na huduma inayotolewa na Serikali bado waathirika hawa wanakabiliwa na tatizo la mavazi, chakula kidogo na maji ni haba. Na kwa kuwa kituo hicho kina eneo kubwa la kilimo, na kwa kuwa kituo hicho kina visima vilivyochimbwa zamani na Wamisionari. Je, Serikali itakuwa tayari pamoja na huduma inayotoa ya chakula kuwalimia mashamba pale pale ili kuwa na chakula cha kutosha na kufufua vile visima ili waathirika hawa waweze kupata huduma inayotosheleza?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba fedha za Serikali kwa ajili ya makazi ya Sukamahela kutoka kwa Afisa Ustawi wa Mkoa kupitia Hazina Ndogo, Serikali inafanya mpango ili kuweza kupeleka Maafisa Ustawi hadi ngazi za Wilaya. Kwa maana hiyo sasa hivi kule Sukamahela kuna Afisa Ustawi Mfawidhi ambaye anatakiwa awe anawajibika kule kwa Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba wanakosa malazi, chakula na kuna visima na eneo la kulima na kadhalika.

Kama nilivyosema katika jibu langu la msingi hawa walemavu walioko katika maeneo ni sehemu ya Wilaya na katika huduma za afya tunazotoa kila mwananchi anapewa *USD 0.750.* Kwa hiyo huyu mwananchi ambaye ni mlemavu na yeye ana sehemu yake ya Bajeti katika zile fedha za *Basket Fund* ambazo zinatoka katika ile Wilaya husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo mimi ninaomba wakati tunapokuwa tunapanga mipango yetu ya Halmashauri na kuzingatia kwamba Wizara ya Afya sasa nyingine tunakuwa na pesa pungufu na wenyewe waweze kupata mgao katika zile pesa za basket fund wapate huduma katika makato haya. Kwa sababu Serikali peke yake sisi

hatuwezi tukahudumia kwa sababu ya Bajeti finyu. Kwa hiyo, ningeomba Mheshimiwa Mbunge pamoja na Wabunge wengine waende wakawashauri wakakae kwenye zile Bajeti ili kuweza kusaidia kwamba katika zile pesa tunazopeleka kule Wilayani kwenye Basket Fund na pesa nyingine na wenyewe hawa wapate mgao wao kama vile ambavyo wananchi wengine wanapata.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Ahsante kwa kunipa nafasi namimi niulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kwa matatizo ya Sukamahela yanafanana na matatizo ya Kambi ya Ipuli Manispaa ya Tabora; na kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuwa anatembelea eneo hilo alikumbana na matatizo ya wananchi wa maeneo hilo kuhusu chakula kibovu na alikiona mwenyewe Mheshimiwa Naibu Waziri na mpaka alitaka kulia kwa sababu chakula kile kilikuwa kinatoa na wadudu aina ya funza. Je, Serikali imechukua hatua gani kwa wale ambao watu wa tender waliopeleka chakula kibovu ambacho hakifai kuliwa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa katika kambi anayozungumzia Mheshimiwa tulitembelea na kukuta chakula kibovu. Lakini tulipokuwa pale tulitoa maagizo kwanza kabisa kwa uongozi wa Halmashauri au uongozi wa Wilaya uliokuwa pale kwamba wahakikishe kwamba chakula wanachopewa wale watu si kibovu. Lakini vilevile tulikuwa tumeagiza wataalam wetu ili waweze kwenda kufuatilia na kuhakikisha kwamba yule Afisa Mfawidhi ambaye alihusika na kuuza chakula kibovu achukuliwe hatua. Nitafuatilia na niweze kumpa jibu Mheshimiwa Mbunge ili kuona kuwa ni hatua gani mpaka sasa hivi amechukuliwa.

Na. 150

**Utekelezaji wa TASAF Awamu ya Pili**

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO** aliuliza:-

(a) Je, ni miradi mingapi imetekelezwa kwa upande wa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar?

(b) Je, ni Wilaya ngapi zimefikia malengo yaliyokusudiwa; na ni Wilaya ngapi hazikufikia malengo hayo na ni kwa nini?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSUF MZEE)** alijibu:-

Kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya pili ya autekelezaji wa Mradi wa *TASAF (TASAF* II) ilianza rasmi utekelezaji wake mwezi Mei, 2005 na inatarajiwa kukamilika mwezi Desemba 2009. Tokea kuanza kwa utekelezaji wa awamu hii hadi kufikia mwezi Machi, 2008, jumla ya miradi 3,820 kutoka Tanzania Bara na miradi 193 kutoka Tanzania Zanzibar imepatiwa fedha za utekelezaji na miradi hiyo yote iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya pili ya *TASAF* inatekelezwa katika Wilaya zote za Tanzania Bara pamoja na Visiwa vya Ungoja na Pemba. Ili kuwa na utekelezaji ulio bora zaidi, kila Wilaya imetengewa fedha za autekelezaji kwa miradi yake. Kutokana na hali hiyo, ni dhahiri kwamba upimaji wa malengo ya utekelezaji utakamilika mwaka 2009 wakati wa kukamilika kwa mradi. Hata hivyo, tathimini ya awali inaonyesha kuwa licha ya kwamba zaidi ya nusu ya muda wa utekelezaji kupita, ziko chini ya asilimia 50 kiutekelezaji ukilinganisha na matarajio. Wilaya hizo ni pamoja na Makete, Kibondo, Kasulu, Liwale, Kilwa na Rungwe. Uongozi wa *TASAF* kwa kushirikiana na Halmashauri husika unafanya utaratibu wa ufuatiliaji kwa karibu ili kuweza kuzifanya Wilaya hizo kufikia lengo kabla ya kukamilika kwa *TASAF II.*

**MHE. ANIA C. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa baadhi ya miradi ina gharama kubwa je, uchangiaji wa wananchi katika miradi ya *TASAF* awamu ya tatu ni sawa na asilimia 20 kwa kila mradi?

La pili, kama zipo Wilaya ambazo wametengewa pesa na hawajazitumia. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba wafadhili wanaweza kukataa kuendelea kutupa pesa kwa miradi ya TASAF kwa awamu ya tatu inaendelea.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSUF MZEE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka nilieleze Bunge lako Tukufu kwamba miradi ya *TASAF* iko ya aina mbalimbali kama Mheshimiwa Mbunge alivyoeleza baadhi ya miradi inagharama kubwa kwa mfano miradi ya maji. Kwa kuzingatia hilo Serikali imeweka michango ya wananchi nayo vilevile itofuatiane. Miradi ya Elimu, Afya michango ya wananchi ni asilimia 20. Lakini kwa miradi ya maji ambayo inagharama kubwa michango ya wananchi ni asilimia 5.

Swali la pili ambalo Mbunge ameliuliza ni kwamba kama Wilaya hizi hazijakamilisha matumizi ya fedha wafadhili hatuoni kwamba watatunyima fedha kwa ajili ya kutekeleza awamu ya tatu ya *TASAF*. Nataka niseme tu kwamba uzoefu umetuonyesha kwamba baadhi ya Wilaya wanapoanza huwa wanaanza taratibu. Lakini baada ya ku-*gain experience* huwa wanaendelea vizuri na hatimaye wanamaliza ule mgao. Lakini huu mgao ni utaratibu wetu wa ndani kila Wilaya tungependa na ninawashauri Waheshimiwa Wabunge watusaidie kufanya hiyo kazi tumalize ule mgao ambao tumeutoa kwa kila Wilaya. Lakini inapotokezea kwamba Wilaya haikumaliza kama nilivyosema awali utaratibu wa mgao ni wetu wa ndani fedha zile zitahamia kwa Wilaya nyingine ambazo za kwao wamemaliza na wanahitaji za ziada.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA**: Nashukuru sana kwa kuniona. Ningependa kuuliza kuhusu fedha hizi za *TASAF* hasa katika awamu hii ya pili. Kuna vijiji ambavyo vimetekeleza vizuri sana miradi hii ya *TASAF* kwa kushiriki na kutumia vizuri zile fedha walizotengewa lakini inapoonekana wametumia fedha vizuri na fedha zimebaki Ofisi ya *TASAF* inaagiza fedha zile zilizobaki zirudishwe badala ya wananchi kupanga mpango mwingine wa kuzitumia zile fedha katika kijiji kilekile. Je, hii ni sahihi, kwanini hizo fedha zisibaki katika vijiji hivyo ili ziwasaidie wananchi waliotumia vizuri fedha zile kuweza kuendeleza miradi mingine katika vijiji vyao?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSUF MZEE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanatakiwa kuibua mradi na wanapoibua mradi kila mradi wanaleta gharama za ule mradi. *TASAF* wanazofanya inapeleka katika akaunti ya mradi fedha zile ambazo wananchi wamezihitaji na inapotokea wananchi wamemaliza ule mradi lakini kuna fedha za ule mradi kiutaratibu fedha hizi zinatakiwa zirudi. Lakini *TASAF* haikatazi na wala haigombi kama kuna kijiji kinataka kuibua mradi mwingine waibue na waombe pesa na watapatiwa pesa nyingine.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala imepata fursa ya kutembelea Wilaya mbalimbali na kujionea utekelezaji wa miradi ya *TASAF* na kwa kuwa inasemekana nusu ya Wilaya zimetekeleza vizuri; Je, kuna utaratibu gani sasa Serikalini wa kuandaa awamu nyingine ya TASAF ili uzoefu uliopatikana usije ukapotea?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSUF MZEE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nieleze kwamba tulianza na *TASAF I* kwa Wilaya 40 za Tanzania Bara na Visiwa vya Unguja na Pemba. Baada ya kupata uzoefu kutokana na *TASAF I* Serikali ikaamua kuanza mchakato wa kuja na *TASAF II* ambao unakwenda kwa Wilaya zote za Tanzania Bara na Visiwa vya Ungaja na Pemba. Uzoefu tayari tunao mchakato wa kuanzisha *TASAF III* tutaanza hivi karibuni na tutakapokamisha *TASAF II* basi tutaendelea na *TASAF III*.

Na. 151

**Ukunda wa Maalum wa Uchumi –Kyaka, Bunazi na Mtukula**

**MHE. JANETH B. KAHAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki imeongeza eneo lake kwa kujumuisha wanachama wapya wa nchi za Rwanda na Burundi; na kwa kuwa Mkoa wa Kagera utakuwa kiungo muhimu kati ya nchi wanachama yaani Tanzania, Uganda, Burundi, Rwanda na hata Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Je, Serikali haoni kwamba itakuwa ni jambo la manufaa kwa uchumi wa Tanzania kustawishwa na kuendeleza Ukanda wa Kyaka. Bunazi na Mtukula katika Mkoa wa

Kagera kwa *Special Economic Zone* kwa ajili ya kuzalisha bidhaa za kuuza kwa nchi jirani za Rwanda, Burundi na Kongo *(DRC).*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSUF MZEE)**alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Bina Kahama, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba mkoa wa Kagera ni kiungo muhimu kati ya nchi yetu na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Aidha Serikali katika mipango yake imeona kuwa itakuwa ni jambo la manufaa kuanzisha maeneo maalum ya uwekezaji rasilimali (*Special Economic Zones)* katika Mikoa mbalimbali hapa nchini ambayo ni viungo na nchi jirani ukiwemo Mkoa wa Kagera.

Maeneo hayo ya uwekezaji rasilimali yatakapokamilika yanatarajiwa kuzalisha bidhaa mbalimbali zaidi kwa ajili ya soko nchi nje ikiwa ni pamoja na soko la nchi jirani. Hata hivyo, ni vyema ikaeleweka kuwa kuanzisha *SEZ's* kuna gharama kubwa kwa maana hiyo Serikali itatekeleza kwa awamu mpango huu na kwa Mkoa ambao ni kiungo ni vyema kuanza kujipanga vilivyo ili Serikali iweze kuelewa maeneo ya kusaidiana na Serikali ya Mkoa.

**MHE. JANETH B. KAHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana na nimefarijika kuona kuwa hata Mkoa wa Kagera upo lakini nilikuwa nikiona kwamba kwa kuwa wachina wamekwisha ahidi kwamba watasaidia katika uanzishwaji wa *Special Economic Zone* katika Mikoa ya Dar es Salaam na Mikoa ya Tanga. Je, hawaoni kuwa kuna fursa basi tuchukue wakati huu ya kuhakikisha kabisa kuwa Mkoa wa Kagera kwa mazingira ya Ushirikiano wetu wa Afrika Mashariki sasa kuna umuhimu wa kuufanya kuwa uwe ni Mikoa ya mwanzoni kuifikiria kwa ajili ya Afrika Mashariki na pia kuiunganisha barabara ya Kyaka mpaka Benako kwa kiwango cha lami kupitia Karagwe?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSUF MZEE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yake tumeyasikia na tutayafanyia kazi.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Urafiki ni jambo zuri lakini imani pia inataka ichukue mkondo wake katika mkondo huo. Hivi tunavyoanzisha urafiki huu wa Afrika Mashariki na kuziongeza nchi mbalimbali katika eneo letu hili, lakini nchi hizi baadhi yake zimekuwa zikipigana kila siku. Tanzania tumejitayarisha vipi katika kuwahami wananchi wetu katika vijiji vya mipakani katika suala zima la ujambazi na kutokana na hivi sasa silaha zimekuwa zikienea?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSUF MZEE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli anayosema kwamba baadhi ya nchi jirani zilikuwa na vurugu lakini hatutoweza kama sisi ni Jumuiya ya Afrika ya Mashariki tukawaachia wenzetu waendelee na vurugu. Ni vyema tukawa nao pamoja tukazungumza nao ili vurugu hizi ziweze kukamilika na tunaamini kwamba vurugu hizi zitakamilika kwa kuka anao.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, swali namba 152 ambalo lilikuwa liulizwe na Mheshimiwa Jenista Mhagama, kutokana na sababu za kimaslahi swali hilo litapangiwa muda mwingine mwafaka na hivyo tunaendelea na swali linalofuata. (*Kicheko*).

Na. 153

**Tatizo la Kukatika Umeme – Mpwapwa,**
**Kongwa na Kibakwe**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa huduma ya umeme ni muhimu sana katika maendeleo na uchumi kwa wananchi; na kwa kuwa katika Mji wa Mpwapwa, kongwa na Kibakwe umeme hukatikakatika mara kwa mara wakati wa mvua.

(a) Je, ni sababu gani zinasababisha umeme katika maeneo hayo?

(b) Je, ni lini Serikali itaondoa tatizo hilo ambalo ni kero kwa wananchi wa maeneo hayo ili nao waweze kupata umeme hata nyakati za mvua?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, sababu zinazosababisha umeme kukatikakatika katika miji ya Mpwapwa, Kongwa na Kibakwe hasa wakati wa mvua ni uchakavu wa nguzo zilizo katika njia ipelekayo umeme Mpwapwa, Chamwino, Kongwa hadi Vijiji vya Gairo na Kubakwe, kutokea kituo cha umeme cha Zuzu (*sub-station*).

Takribani nguzo 1600 kati ya 2411 zilizoko katika njia hiyo zimechakaa kutokana na kuoza au kuliwa na wadudu hali ambayo husababisha nguzo kuanguka wakati wa mvua na upepo. Nguzo zilizokatika njia hii hazijabadilishwa kwa kupindi kirefu kutokana na hali mbaya ya kifedha ambayo iliikumba *TANESCO* katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuondokana na tatizo hilo *TANESCO* wamekamilisha kazi ya kuzitambua nguzo ambazo zimechakaa katika njia hiyo ya kutoka

*Zuzu Substation* kwenda Mpwapwa, Chamwino, Kongwa hadi vijiji vya Gairo na Kibakwe. Gharama ya ukarabati wa njia hiyo ambao unajumuisha kubadilisha nguzo zilizochakaa na vikombe vilivyopasuka kutokana na kuanguka kwa nguzo hizo ni shilingi milioni 905. *TANESCO* wanatafuta fedha ili kuanza kazi ya ukarabati wa njia hiyo. Aidha kazi hiyo ya ukarabati wa njia hiyo itaambatana na kufunga. *Load Breaker* ili kutengenisha maeneo yenye hitilafu kwa haraka na kurejesha umeme maeneo yaliyo salama badala ya kuzima njia nzima wakati tatizo linapotokea eneo moja.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali la nyongeza. Kwa kuwa jana tumepitisha Muswada wa Umeme na nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kujibu hoja zetu vizuri. Sasa nina swali. Kwa kuwa wananchi wengi wanahitaji umeme katika maeneo yao na hasa mijini na vijijini na kwa kuwa ombi la wananchi ni kwamba gharama za kuunganisha umeme ni kubwa shilingi laki tano hawana uwezo huo.

Je, sasa Mheshimiwa Waziri utakubaliana nami kwamba ili *TANESCO* wapate wateja wengi iko haja ya kupunguza gharama za kuunganisha umeme?

Swali la pili kwa kuwa mwaka 2004 tulipitisha Sheria ya umeme vijijini na Serikali ilitenga zaidi ya bilioni kumi kwa ajili ya kusambaza umeme vijijini. Je, ni sababu gani za msingi ambazo zilisababisha utekelezaji wake ukwame na kusababisha vijiji vya Chunyu, Berege, Mima, Mboli, Lupeta pamoja na Ng’hambi kukosa umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyowasilisha jana wakati wa kujadili Muswada wa Umeme, nadhani tumekubaliana kwamba kimsingi ni kubwa lakini ni sababu ya gharama zenyewe halisi ambazo zinatokana na uendeshaji na pia gharama zinazohusiana. *Cost related* kwenye kuunganisha huo umeme wenyewe.

Kwa hiyo, nakubaliana naye Mheshimiwa Lubeleje kwamba kuna sababu ya msingi kabisa ya kuhakikisha kwamba tunakaa na *TANESCO* na kuangalia kwamba ni nini hasa kinachoweza kufanyika ili kupunguza gharama za umeme. Lakini kusema kweli hili ni tatizo kubwa sana kama mlivyojadili jana tufanye mikakati ya makusudi kabisa ili tuangalie kama tunaweza kufanya uwekezaji wa makusudi kuweza kupunguza gharama za umeme kutokana na uwekezaji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili la bilioni kumi. Kwa kusema kweli bilioni kumi kwa miradi iliyokuwepo *REA* na wajibu wa *REA* ni pesa ndogo nadhani zilikuwa ni fedha za kuanzia. Tukubaliane na Mheshimiwa Malima Lubeleje kwamba kwa kuwa tayari tumeshafanya tathimini tunajua kabisa kwamba kinachotakiwa kufanyika ni nini, basi Wizara yangu tumeshaanza kufanya tathimni kuanzia mwaka huu 2008 na tutaanza kushughulikia suala hilo isipokuwa tutalifanya kwa awamu.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niongezee kwenye majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ameyatoa kuhusu maswali mawili ya Mheshimiwa George Malima Lubeleje, kama ifuatavyo:-

Pamoja na ufafanuzi wa Mheshimiwa Naibu Waziri lakini pia nikumbushe Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla kwamba bei za umeme sasa hivi zinapangwa kupitia mdhibiti wetu wa masuala ya nishati na maji *EWURA.* Kwa hiyo, kinachotozwa pale kinakuwa kimezingatia vigezo ambavyo vimeainishwa ndani ya Mamlaka chini ya sheria ambayo ilianzisha *EWURA.*

Kwa hiyo, ni jambo la msingi kukumbuka kwamba bei zile zina idhinishwa na *EWURA.* Lakini la pili pia ni kwamba zile bilioni kumi zilivyoanza kutumika zisingeweza kutosha miradi yote ambayo imeshabainishwa. Kwa hiyo, tuendelee kuomba Waheshimiwa Wabunge kwamba tuidhinishe fedha za kutosha kwenye Bajeti inayokuja ili pengine miradi ya Mheshimiwa Lubeleje iwemo katika utekelezaji. Kwa sababu kikwazo kikubwa ni kiasi kidogo ambacho kilikuwepo. Lakini nia ipo ya kuweza kuifikia miradi mingi zaidi.

**MHE. DEVOTA LIKOKOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa matatizo ambayo yapo Mpwapwa yanafanana kabisa na matatizo ambayo yapo katika Manispaa ya Songea, ambapo ndiyo Mji Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Songea umeme wake unakatikakatika sana. Vilevile kuna mgao mkubwa wa umeme na Serikali imekuwa ikiahidi mara nyingi kuyashughulikia matatizo hayo na kukomesha kabisa hali ya umeme kukatikakatika Songea na kuwa na umeme wa uhakika. Ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kuunganisha Mkoa wa Ruvuma na gridi ya taifa ya umeme umeshafanyiwa upembuzi yakinifu na ulikamilika 2005/2006. Kwa sasa hivi tunawasiana na tunatarajia kupata msaada wa Serikali ya Sweden kupitia Shirika lake la Maendeleo la Kimataifa la *SIDA.* Mradi huo unatarajiwa usambaze umeme kutoka Makambako hadi Songea halafu ukifika Songea pale uende Namtumbo, Mbinga na Maeneo mengine ikiwemo Peramiho kwako Mheshimiwa Mwenyekiti. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Naibu Waziri alihakikisha wazi kwamba tatizo kubwa nguzo zinaanguka na nguzo hizo zina waya wa umeme; na kwa kuwa wananchi wanapita katika maeneo hayo wakati nguzo hizo zina umeme ni hatari kwamba wananchi kupoteza maisha wakati zinawaangukia, haoni kwamba sasa ni wakati mwafaka kutokujali pesa lakini wajali maisha ya wananchi licha ya kwamba kupata umeme wenyewe.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Mheshimiwa atakubaliana na mimi kwamba Serikali hii inajali sana maisha ya watu na naomba nimhakikishie kwamba suala la nguzo za umeme linashughulikiwa.

Lakini inapotokea tatizo la namna hiyo basi Serikali kupitia *TANESCO* inawajibika moja kwa moja kwenda kushughulikia tatizo hilo hata kwa muda ili liondokane na tatizo la uwezekano wa wananchi kudhurika kwa hizi nyaya zilizoanguka hasa wakati wa mvua. *(Makofi)*

Na. 154

**Ufaulu wa Mtihani ya Darasa la Nne.**

**MHE. JOB Y. NDUGUI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, huandaa Mtihani wa Darasa la Nne, ambapo mwanafunzi hutakiwa kufaulu masomo yote. (Kila somo moja moja) badala ya wastani wa masomo yote kwa pamoja:-

Je, Sera hiyo ina umuhimu gani?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kama ifuatavyo.
Lengo la Mtihani wa Darasa la IV ni kufanya tathmini ya awali ya kitaifa ya maendeleo ya mwanafunzi katika ngazi ya Elimu ya Msingi. Mtihani huu ni muhimu kwa sababu zifuatazo:-

(i) Unapima mafanikio na maendeleo ya mwanafunzi ili kuona iwapo malengo yaliyokusudiwa katika ufundishaji na katika kujifunza yamefikiwa ikiwa ni pamoja na uwezo wa mwanafunzi kufahamu na kumudu stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu na kutumia namba.

(ii) Ni tathimini ya kati ambayo inasaidia wataalam wa elimu kubaini matatizo mbalimbali katika ufundishaji na kujifunza ili kuweza kuboresha mitaala na kurekebisha mapema kasoro zinazojitokeza.

(iii) Humfanya mwanafunzi kutokuwa na woga wakati anapofika kwenye mitihani ya Darasa la saba. Upimaji wa maendeleo ya mwanafunzi katika kila somo ni muhimu kwa sababu kunawapa wanafunzi ari ya kuongeza bidii katika masomo yote. Hata hivyo kuanzia sasa Mtihani wa Darasa la nne utaendelea kuwa na lengo la kutathimini ufundishaji na kujifunza. Kwa wanafunzi na sio kumfanya mwanafunzi kurudia darasa anaposhindwa kufikia alama zilizowekwa katika somo hilo. Wanafunzi watakaoshindwa kufikia alama zinazotakiwa watapewa msaada katika maeneo yanayowapa shida kadri watakavyokuwa wanaendelea na Elimu ya Msingi. Wizara yangu itaendelea kuimarisha ufundishaji na upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia shuleni ili kutoa elimu bora.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa niulize swali la nyongeza. Lakini, nianze na pongezi kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa kutekeleza jambo hili la kubadilisha mtihani wa darasa la nne. Sasa kuwa na kipimo cha tathmini ya ufundishaji na kujifunza kwa wanafunzi na kwa maana hiyo wametekeleza agizo la Rais kuhusiana na mtihani huo wa darasa la nne. Ninalo swali moja tu. Upo mtihani wa kidato cha pili ambapo watoto wanakuwa wamesoma darasa la kwanza hadi la saba kwa Kiswahili kwa masomo mengi. Wanapoingia sekondari zetu hizi za Kata ambazo vitabu ni haba, walimu ni wachache na lugha mpya ya kiingereza, hawajafika hata mwaka wa pili, tayari mtihani wa kidato cha pili. Watoto wengi sana wanafeli. Je, sera hii, Serikali inasemaje kuhusu mtihani huu ambao kwa kweli ni kero? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mtihani wa darasa la nne na mtihani wa darasa la kumi inashabihiana kwa kiasi kikubwa. Kwanza, mitihani yote inaonyesha ni jinsi gani mtaala ambao umewekwa unafanikiwa au unatekelezwa na ni jinsi gani watoto wanafaidika kwa kujifunza katika mitaala hiyo. Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo, mitihani hiyo ni muhimu sana hata kama kuna matatizo ya vifaa katika shule mbali mbali.

Mheshimiwa Spika, ah! Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni nyota njema ya asubuhi eeh! Hata hivyo, Mheshimiwa Spika, ni muhimu ieleweke…. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, Kiti leo kinaongozwa na Mwenyekiti wa Bunge na Mheshimiwa Spika, leo amekalia Kiti chake cha Ubunge, ndani ya Bunge hili. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, usiogope! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo ieleweke kwamba mitihani hii inafanywa katika mazingira mbali mbali kwa wanafunzi na vijana wanaotokea katika jamii tofauti! Aidha, katika jamii za wafugaji ambao wangependa watoto washiriki sana katika kuchunga, wanapofeli mtihani wa darasa la nne, basi wanaona kama ni njia ambayo inawaleta watoto nyumbani wa kuwasaidia na watoto hao hawarudi tena shuleni.

Aidha, katika mtihani wa *form two,* mtihani ule si kwa jamii ya wafugaji peke yao, bali na wakulima wengi wanaona watoto kurudia mtihani ni mzigo mkubwa kwa sababu inaongeza muda wa watoto kukaa shuleni na hivyo kuwa mzigo mkuwa wa kulipia ada ya shule za sekondari na hivyo watoto wanapofeli huachwa wabaki nyumbani. Wizara yangu inayafikiria mambo haya kwa makini na tutaendelea kuutekeleza mtihani wa *form two*. Lakini uwe ni mtihani wa kutathmini utekelezaji wa mitaala, uwe ni mtihani wa kuangalia ni jinsi gani walimu wanafanikiwa katika kufundisha. Lakini pia uwe ni mtihani wa kutufahamisha ni matatizo gani yanayojitokeza na watoto wana matatizo gani ili tuweke mkakati wa kuwasaidia. Mitihani hii haitakuwa mitihani tena ya kuwafanya watoto warudie madarasa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, majibu haya yamekuwa marefu sana. Kwa hiyo, ninaomba tuendelee na swali linalofuata.

Na. 155

**Vyuo Vya Elimu ya Juu Visivyo Vyuo Vikuu**
**Kutoa Shahada**

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA** aliuliza**:-**

Kwa kuwa Serikali imevisitisha Vyuo vya Elimu ya Juu visivyo Vikuu kufundisha na kutoa shahada; na kwa kuwa *NACTE* ipo kwa mujibu wa sheria kusimamia na kuratibu vyuo hivyo ambavyo vinatoa *Competence Based Education*:-

(a) Je, ni sababu zipi zilizofanya Serikali ikataze vyuo hivyo kutoa shahada?

(b) Je, ni lini vyuo hivyo vitaruhusiwa kuendelea kutoa shahada ili kuwepo na taaluma za juu kwenye *Competence Based Education* sanjari na *Academic Education?*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa Serikali imesimamisha utaratibu wa huko nyuma wa Vyuo vya Kati na vile vinavyotoa *Competence Based Education* kutoa mafunzo ya Shahada. Serikali imechukua hatua hii kwa kutambua umuhimu na mahitaji makubwa tuliyo nayo ya watalaam wa ngazi ya kati wanaohitimu kutoka katika vyuo hivyo katika soko la ajira. Aidha, ngazi hii ya wataalam ndiyo injini ya kusukuma na kujenga uchumi wetu. Hivyo, Serikali imesitisha utaratibu wa kuvigeuza vyuo hivyo kuwa vyuo vikuu au taasisi za elimu ya juu. Aidha, kwa sasa kuna upungufu mkubwa wa wahitimu wa ngazi ya kati hususan katika Sekta ya Uhandisi, Ufundi wa Maabara, Uhifadhi wa Maliasili, Utalii na Uendeshaji wa Hoteli.

Katika miaka ya hivi karibuni umejitokeza pia uhaba mkubwa wa watalaam katika sekta ya madini, mafuta na gesi. Hivyo, tunalazimika kuajiri wataalam wa fani hizo kutoka nchi za nje. Lengo la Serikali ni kuvipanua vyuo tulivyonavyo na kuviongezea uwezo wa kutoa elimu ya kati na elimu ya ujuzi wa aina mbali mbali ili kuendeleza uchumi wa nchi yetu.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Bodi ya *NACTE* ikishirikiana na Wizara yangu na wadau husika wanaangalia mitaala ya vyuo vya *VETA*, vyuo vya Teknolojia na vyuo vingine kwa lengo la kuirekebisha ili itoe elimu bora ya ujuzi *(Competence Based*

*Education)* itakayowawezesha wahitimu kuajiriwa na kujiajiri wenyewe na kuwawezesha kuendelea na masomo ya Chuo Kikuu kwa kupata sifa stahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema ikakumbukwa pia kuwa kutoa elimu katika ngazi ya Shahada kunahitaji wataalam mabingwa waliobobea katika fani zao. Mahitaji mengine ni karakana, vifaa, maabara, rasilimali za vitabu, majarida na utafiti wa ngazi ya kimataifa ambavyo mara nyingi havipo katika vyuo vyetu vya Kati.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana! Napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake ambayo yamenitosheleza. Lakini nina swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa, katika vyuo vya elimu ya juu vilivyopo nchini na vyuo vikuu vyote, kuna uhaba mkubwa sana wa walimu; na kwa kuwa vyuo vikuu vinapanuka vinakuwa vingi kwa wakati mmoja. Je, Serikali ina mpango gani wa kuviwezesha vyuo hivi ili viweze kuwa na wataalam waliobobea katika nyanja hasa ya *Ph.D? (Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kila mwaka Serikali inatenga karibu shilingi bilioni 3.5 kwa ajili ya kusomesha wahadhiri na walimu wa vyuo vikuu katika ngazi ya *Masters of Science* au Shahada za Uzamili na Shahada za Uzamivu *(Ph.D.)*

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya mpiga kura wangu aliyenitumia *message* kutaka kujua, naomba swali klake hili la kwamba kwa nini Serikali haitoi mikopo ya Bodi kwa wanafunzi wanaofanya *Masters Programme*?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaanza kutoa mikopo kwa wanafunzi au vijana wanaofanya Shahada ya Uzamili *(Master of Science)* kwa wale ambao wameajiriwa na Vyuo Vikuu kama *Tuitorial Assistants* au *Assistant Lecturers* katika vyuo hapa nchini. Serikali haiwezi kutoa mikopo kwa wananfunzi wote wa ngazi hiyo kwa sababu ya ufinyu wa Bajeti.

Na. 156

**Tatizo la Maji Safi na Salama Nanyumbu**

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA** aliuliza :-

Kwa kuwa Wilaya ya Nanyumbu ina matatizo makubwa ya upatikanaji wa maji safi na salama. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwa na mradi mkubwa wa maji kutoka Mto Ruvuma ili wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu na wa Mkoa wa Mtwara kwa ujumla waweze kufaidika na rasilimali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dunstan Mkapa, Mbunge wa Nanyumbu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Wilaya ya Nanyumbu ina tatizo kubwa la upatikanaji wa maji safi na salama. Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji yenye lengo la kuhakikisha kuwa wananchi wote waishio vijijini wanapata huduma ya maji safi na salama.

Hivi sasa mchakato wa kuwapata wataalam washauri watakaotoa huduma za kiufundi na za uhamasishaji katika kila Wilaya unafanyika na watalaam hao wanatarajiwa kupatikana mwezi Julai, 2008. Wataalam hao watafanya upembuzi yakinifu utakaoainisha hali ya upatikanaji wa maji katika maeneo mbali mbali ya Wilaya ya Nanyumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watalaam washauri watakaoteuliwa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa miradi wakishirikiana na watalaam wa Mkoa, Wilaya na wananchi ndio watakaoainisha vyanzo vya maji kwa ajili ya vijiji mbali mbali. Mto Ruvuma ni moja ya vyanzo vya maji vitakavyochunguzwa kwa ajili ya kuandaa miradi kwa ajili ya Wilaya ya Nanyumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa fedha za utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji hupelekwa moja kwa moja kwenye Halmashauri za Wilaya, Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu ina jukumu la kubuni mipango ya maendeleo ambayo itahusisha miradi yote inayotakiwa kutekelezwa ikiwa ni pamoja na miradi ya maji itakayotumia Mto Ruvuma kama chanzo cha maji na kuitengea fedha ili kunufaika na rasilimali hiyo ya maji.

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana! Nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Mangaka ambayo ni Makao Makuu ya Wilaya ya Nanyumbu, kwanza ilikuwa kwenye mradi wa maji vijijini, lakini baada ya kuwa Makao Makuu ya Wilaya, imepandishwa kuwa mradi wa maji mjini. Lakini kwa bahati mbaya haimo kwenye programu ya maji mjini, wamechagua miji 32 tu. Sasa Je, kutokana na ongezeko la watu wengi pale Mangaka, maji hamna, Serikali inasemaje kuhusu tatizo la maji kwa watu wa Mangaka?

Swali langu la pili. Hivi haya maji ya Mto Ruvuma tuna faida gani nayo sisi Watanzania na hasa watu wa Kusini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mradi huu wa maji ambao unatarajiwa pia kupeleka maji katika Mji Mkuu wa Wilaya wa Mangaka umeanza sasa kutekelezwa; na ukizingatia kwamba Wilaya hii ni mpya, basi Serikali tutakachofanya ni kuangalia miradi ambayo ilikuwa inafaidisha Wilaya hiyo ambayo kwa bahati mbaya au nzuri kutokana na mgawanyiko, imepungua. Basi tutawapa fursa ya kuongeza miradi mingine kufidia ile ambayo tayari imeishaondoka katika mpango uliokuwepo zamani.

Kuhusu jinsi gani watu wa Kusini watafaidi maji ya Mto Ruvuma. Mimi nadhani hili limeanza sasa kutazamwa vizuri na Serikali. Nchi wanachama wa *SADC*, wameliona hili na waliagiza kuanzisha utaratibu wa kusaidia mabonde ya Buzi, Save na Ruvuma katika Tanzania kwa nchi mbili za Tanzania na Mozambique kushirikiana.

Hivi sasa tayari Tanzania na Msumbiji zimeishaanzisha chombo cha kuendeleza Bonde Shirikishi la Ruvuma yaani Bonge la *Shared Water*. Chombo hiki kinaitwa *Joint Ruvuma Basin Commission* na mkataba wa mashirikiano ulitiwa saini huko Pemba, Msumbiji tarehe 11 Oktoba, 2006. Tunatarajia mfadhili awe Benki ya Maendeleo ya Africa. Hivi sasa Tanzania tayari imeishafungua Akaunti kule Mtwara kwa ajili ya maandalizi ya kuendeleza mradi huu.

Kazi iliyobaki mbele yetu katika mradi huu ni mkutano utakaofanyika tarehe 21 mpka 22 Mei, 2008 pale Bagamoyo mwaka huu ambao utazijumuisha nchi hizi mbili kuangalia sasa kutengeneza *Project Document* ambayo itakuwa ni *document* ya nchi zote kwa ajili ya utekelezaji.

Na. 157

**Mradi wa Maji Tove/Mwiramba**

**MHE. YONO S. KEVELA** aliuliza:-

Kwa kuwa mradi wa maji wa Tove au Mwiramba ni mradi mkubwa katika Wilaya ya Njombe, Mkoani Iringa:-

(a) Je, mradi huo unagharimu fedha kiasi gani na utaisha lini?

(b) Je, mradi huo utakuwa na matumizi gani mengine zaidi ya maji safi kwa matumizi ya wanadamu?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mbunge wa Njombe Magharibi, naomba kutoa maelezo yafuatayo :-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa mradi wa maji wa Tove – Mtwango ni mradi mkubwa katika Wilaya ya Njombe unaotegemewa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka 2007 hadi 2010. Ujenzi wa mradi huo umeanza na hadi sasa ujenzi wa vitega maji *(intake)* viwili vya kuchukua maji kutoka Mto Tove na Mto Mnyolo umekamilika. Pia bomba kuu la maji limelazwa kwa umbali wa kilomita 22 kati ya kilomita 80 zinazotakiwa. Ujenzi wa matanki 14 ya kuhifadhia maji unategemea

kuanza mwezi wa tano, 2008. Mradi huo utakapokamilika utahudumia vijiji 14 vyenye wakazi wapatao 39,500. Vijiji hivyo ni Usalule, Igagala, Ulembwe, Mgodechi, Itulike, Nyumbanitu, Mlevela, Mungate, Igima, Mhadzi, Lusisi, Lulanzi, Itunduma na Mtwango. Vyanzo vikuu vya maji vya mradi huo ni vitatu ambavyo ni Mto Tove, Mto Mnyolo na Mto Mlevela. Kwa kifupi, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa maji wa Tove – Mtwango utagharimu fedha kiasi cha shilingi bilioni 3.5 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2010. Wafadhili wa mradi huo ni Umoja wa Nchi za Ulaya *(EU)* ambao watatoa shilingi 2,231,950,000 na Shirika lisilo la Kiserikali la *Association Cooperation Rural Africa (ACRA) l*enye Makao Makuu nchini Italia litatoa shilingi 1,268,050,000. Mradi huo unatarajiwa pia kutoa mafunzo kuhusu usafi wa mazingira na kujenga vyoo bora 3000 kwa matumizi ya wananchi na taasisi mbali mbali kama shule na hospitali.

(b)Mheshimiwa Mwenyekiti, maji yatakayopatikana kweny mradi huu yatatumika pia kwa shughuli za kuboresha mazingira kama vila kupanda miti kwenye maeneo ya vyanzo vya maji. Aidha, miti itapandwa katika vijiji vya mradi ili iweze kuwasaidia wananchi katika shughuli mbali mbali kama kuni na mbao ili kupunguza uharibifu wa vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafsi hii kuwashukuru Umoja wa Ulaya na Shirika la *ACRA* kwa msaada wao huu mkubwa na Kanisa Katoliki ambalo lilibuni mradi huu. Aidha, nawashukuru na kuzipongeza taasisi za dini hususan makanisa ya Kilutheri na Anglikana na Shirika la Kiislam la *D-Nurei* ambayo yamechangia sana kuendeleza miradi ya maji katika Mkoa wa Iringa. *(Makofi)*

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibui Waziri wa Maji na Umwagiliaji; nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

La kwanza ni Kwenye majibu yake ilionyesha kwamba Serikali ya Tanzania hakuna kiasi chochote inachochangia. Je, ni kwa nini katika mradi huu mkubwa Serikali ya Tanzania haionyeshi kwamba kuna mchango fualani inachangia kwenye huu mradi? Swali la pili; kwa kuwa hili shirika la *Association Cooperation Rural Africa (ACRA)* chini Italy linasimamiwa na huyu *Father* Camilo ambaye yuko Parokia ya Kipengele, Kata ya Igosi, Njombe; na kwa vile alikuwa na malalamiko na *TRA* na Bandari kwamba anatozwa kodi na ushuru zaidi ya milioni 30. Je, Serikali ina mpango gani wa kusamehe kodi zote na kumrudishia gharama zote ambazo alikuwa anatozwa kinyume cha taratibu?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi yote inayotekelezwa nchini, inakuwa na maandalizi, inakuwa na *project document* na masharti yake ya utekelezaji. Kama kipengele hiki, hakikutokea kwamba Serikali moja kwa moja ichangie, basi bila shaka ndiyo maana mradi huu unatekelezwa kwa njia hii. Lakini naomba niseme pia kwamba hata kama Serikali haijatoa fedha, lakini hawa wote wanaotekeleza pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali, tujue kwamba hayafanyi

kazi nchini yenyewe, yanafanya kazi kwa ajili ya kutekeleza sera za Serikali. Hata hivyo, mimi nafikiri bado fursa ipo, si kazi ngumu ku-*mainstream* kitu kingine ambacho kitaweza kusaidia kama mradi huu unakwama kwamba. Serikali iko tayari kuangalia upya. Kuhusu huyu *Father* Camilo kutozwa kodi, mimi naomba tu niseme kwamba nitalifuatilia hili kwa kushirikiana na *TRA* tuone kama kuna ukweli, halafu tutatoa majibu kiserikali. *(Makofi)*

Na. 158

**Kujenga Mahakama ya Wilaya na Kupewa Hakimu wa Wilaya ya Nkasi**

**MHE. PONSIAN D. NYAMI** aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Nkasi haina jengo la mahakama ya Wilaya na pia hakuna Hakimu wa Wilaya, na kwamba kesi nyingi huendeshwa na Hakimu wa kujitolea kutoka Wilayani Sumbawanga, ambapo ni umbali wa kilomita 100:-

(a) Je, ni kwa nini Serikali haijengi jengo la mahakama?

(b) Je, kiwanja kitatafutwa lini na ujenzi wake utaanza lini?

(c) Je, ni kwa nini Wilaya ya Nkasi haijawahi kupewa Hakimu wa Wilaya tangu ianzishwe mwaka 1979; na Je, Hakimu huyo ataletwa lini?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ponsian D. Nyami, Mbunge wa Nkasi, kama ifuatavyo:-

(a) Mahakama ya Tanzania ina mpango wa kujenga Mahakama katika Wilaya nchini. Nkasi imo katika mpango wa kujengewa mahakama ya Wilaya.

Lakini ujenzi unakwamishwa na ufinyu wa Bajeti inayopewa Mahakama. Mara Bajeti itakaporuhusu, Mahakama ya Wilaya ya Nkasi itajengwa.

(b) Kuhusu kiwanja; kiwanja cha kujenga jengo la mahakama ya Wilaya ya Nkasi kimepatikana.

(c) Kwa kuwa hakuna jengo la mahakama ya Wilaya ya Nkasi na pia hakuna nyumba ya Hakimu, imekuwa vigumu kumpeleka Hakimu wa Wilaya huko Nkasi. Hata hivyo, Wilaya ya Nkasi hutembelewa na Hakimu Mkazi kutoka Sumbawanga na wala sio wa kujitolea bali hupangwa kufanya kazi huko. Huu ni utaratibu tunaoutumia sehemu zingine zote ambako hakuna Hakimu Mkazi. *(Makofi)*

**MHE. PONSIAN D. NYAMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupewa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Miaka 38 ya Wilaya, haina jengo la mahakama wala Hakimu. Je, ni Wilaya ngapi hapa nchini zenye umri kama huo hazina majengo wala hakimu? La pili; kukosa nyumba ya Serikali imekuwa ni kigezo cha kutokumpeleka Hakimu Nkasi. Je, Mahakimu wote wa Wilaya hapa nchini hukaa katika nyumba za Serikali?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa kama ninavyozungumza, ziko kama Wilaya 40 ambazo ahazijapatiwa mahakama ya Wilaya wala hazina Hakimu wa Mahakama ya Wilaya. Ukweli ni kwamba si Mahakimu wote wanakaa kwenye nyumba za Serikali. Lakini kama Mheshimiwa Mbunge ataweza kuzungumza na wenzake kule kwenye Wilaya yake ya Nkasi, mahakama ikapatiwa nyumba ya hakimu pamoja na jengo la mahakama ya Wilaya, basi Wizara ya Katiba na Sheria haitasita kuhakikisha kwamba anapelekwa kule hakimu wa mahakama ya Wilaya kwenda kutumikia wananchi wa Jimbo la Nkasi.

Na. 159

**Kuondoa Sheria Zinazoonyesha Ubaguzi Katika Katiba na Sheria za Nchi**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA (K.n.y. MHE. HALIMA M. MAMUYA)** aliuliza:-

Je, ni lini kutakuwa na mabadiliko au marekebisho ya sheria na vifungu vya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania vinavyoonyesha wazi ubaguzi na unyanyasaji wa kijinsia na Wabunge kama vile kifungu cha 51 (2) cha Katiba ya Nchi kinachoeleza wazi kuwa Waziri Mkuu atateuliwa kutokana na Wabunge wa Majimbo, Serikali haioni kuwa kifungu hicho kinawabagua wale Wabunge wasio na Majimbo?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Halima M. Mamuya, Mbunge wa Viti Maalum, napenda kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Viti Maalum vilikuja kama *Affirmative Action* ambayo maana yake ni kuchukua hatua maalum kwa muda malum ili kuwezesha kuwepo kwa uwiano sawa na sio suala la kudumu. Nchini Marekani *Affirmative Action* ilikuja baada ya siasa za ubaguzi kuisha ili kuleta uwiano sawa kati ya weusi wenye asili ya kiafrika na wazungu katika nafasi za kazi kisiasa na madaraka. Baada ya kutoa maelezo hayo, napenda kujibu swali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia ya Viti Maalum ilikuwa ni kuwezesha wanawake kupambana na wanaume katika kuwania nafasi za uongozi wa kisiasa. Matarajio ni kwamba baada ya kupata uzoefu, waweze kwenda kugombea majimboni. Hapo mwanzoni wanaume waliokuwa wana uwezo wa kifedha na kutokana na mfumo dume uliokuwepo, ndio waliokuwa wakigombea na kushinda nafasi za uongozi.

Katika kujaribu kuleta uwiano sawa wa kijinsia katika uongozi wa kisiasa Serikali ikaamua kuwa na Viti Maalum ambavyo vitawawezesha wanawake kupata fursa za uongozi wa kisiasa sawa sawa na wanaume.

Nafasi hizi za upendeleo haziwezi kulinganishwa na wale wanaogombea katika majimbo. Waziri Mkuu ni nafasi nyeti ambayo anayepewa wadhifa huo ni vizuri atokane na Jimbo kwa kuchaguliwa na wnanchi.

Hii inamsaidia Waziri Mkuu kuelewa mataizo halisi ya majimbo ana pia kuwajibika vyema kwa wananchi waliomchagua. Ibara ya 51(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haibagui Wabunge wasio na majimbo kwa kuwa nia ya Viti Maalum ni kuwapa wanawake fursa ya uongozi ili kuwawezesha baadaye waweze kugombea katika majimbo.

Lakini, kwa hivi sasa ni vyema nafasi ya Waziri Mkuu ambayo ni moja ya nafasi za juu za kisiasa nchini, ikawa ya mtu aliyechaguliwa na wananchi na hivyo uhalali wa kuwepo pale unatokana na ridhaa ya wananchi.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sna Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutujibu. Lakini ninaomba tu, ninapokuwa Mbunge wa Viti Maalum, siandaliwi kwenda kwenye Majimbo. Hilo naomba aniambie ni sheria gani inayoniweka Mbunge wa Viti Maalum kwamba mnaniandaa kwenda kwenye majimbo?

Kwa sababu sasa tunaelekea kwenye *fifty fifty*, na nina uhakika itapita kwa sababu sisi kwenye Ilani ya CCM tumepitisha. Je, Serikali imeishajiandaa sasa kurekebisha sheria iliyopo ya kuweka kwamba masharti awe mwanaume au vipi?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, suala hili la kuwawezesha wanawake kuweza kugombea majimboni siyo suala la kisheria ila ni utaratibu ambao Serikali iliona kwamba unafaa ili kuwawezesha wanawake baadaye waweze kwenda kugombea kwenye majimbo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**: Swali la pili ni kweli kuna mchakato unaendelea hivi sasa wa kuhakikisha kwamba hapa Bungeni kunakuwa na wanawake asilimia 50 sawa na wanaume asilimia 50. Kuna mchakato unaoendelea hivi sasa na wakati utakapofika nina hakika mapendekezo yatakapoletwa hapa Bungeni ili

tuweze kuona kama kuna haja ya kuwa na Waziri Mkuu atakayetokana na majimbo maalum. Kwa hiyo, naomba mchakato huo ufikie mwisho wake. (*Makofi*)

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge, nafikiri nitoe nafasi ya swali moja la nyongeza na nitamwita Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, ili aweze kuuliza swali la mwisho la nyongeza.

**MHE. ZAINAB A. GAMA**: Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru sana kwa kunipa nafasi, tangu nimeingia Bungeni mwaka 1985, tayari kulikuwa na wanawake ndani ya Majimbo hadi sasa wapo. Je, kutokana na jibu la Mwanasheria Mkuu ina maanisha wanawake hawa wa Majimbo walikuwa hawana uwezo wa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dr. Zainab Amir Gama, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kama anavyosema kuanzia mwaka 1985 kulikuwa na wanawake wanaotokana na Jimbo, lakini ukweli ni kwamba mtu ambaye anatakiwa kupendekeza jina la mtu anayestahili kuwa Waziri Mkuu, ni Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, nadhani wakati utakapofika atapendekeza mwanamke kuwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge kwa kuwa tumebakiza swali moja, busara ya kiti changu inaniambia kwamba inafaa tukalimaliza. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala, ili swali lake la mwisho liweze kuulizwa.

Na. 160

**Shirika la Nyumba la Taifa**

**MHE. MOHAMMED RISHED ABDALLAH (K.n.y. MHE. MUSSA AZZAN ZUNGU)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Shirika la Nyumba la Taifa limeanza kwa kasi sana kuingia ubia na wawekezaji kwa kujenga upya nyumba zao. zoezi linalofanya wapangaji wa sasa kupewa *notice* na kufukuzwa:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa zoezi hilo linawanyanyasa wanyonge na kukaribisha matabaka?

(b) Je, kwa nini Serikali isiwaelekeze *NHC* kuwa waingie ubia kwa kuwapa kipaumbele kwanza wakazi wa zamani kwa kuwapa angalau ghorofa tatu kwenye jengo lenye ghorofa 12 ili wasipelekwe nje ya Mji?

(c) Je, kwa nini shirika hilo haliwauzii nyumba za ghorofa wapangaji walioishi miaka 35 na hata kufidia gharama za ujenzi mara 50?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mussa A. Zungu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kweli kuwa kuingia ubia na wawekezaji kwa kujenga upya nyumba zinazomilikiwa na shirika la Nyumba linawanyanyasa wanyonge na kukaribisha matabaka. Kwa mujibu wa sheria Namba Mbili (2) ya mwaka 1990.

Pamoja na majukumu mengine shirika la Nyumba la Taifa lina jukumu la kujenga nyumba au majengo ya aina mbalimbali ya kuishi, kupangisha au kuuza kwa watu binafsi, taasisi za umma na binafsi.

Aidha, kutokana na matakwa ya Sheria Na. 11 ya mwaka 2005 shirika linatakiwa liendeshe shughuli zake kibiashara. Hivyo ni muhimu kwa shirika kushirikiana na sekta binafsi kwa utaratibu wa *Public –Private Partnership* (*PPP*) kwa lengo la kuongeza mtaji, teknolojia na utaalam.

Kutokana na utekelezaji wa mipango ya shirika ya kuvunja majengo machakavu katika Miji na kujenga upya lenyewe au kwa kushirikiana na sekta binafsi, Serikali imenufaika kama ifuatavyo:-

(i) Kuboresha mazingira na mandhari ya Miji yetu kwa kuondoa majengo chakavu ambayo yanaharibu mandhari ya Miji na kuhatarisha maisha ya wananchi.

(ii) Kuongeza ajira kwa wananchi.

(iii) Kuongeza majengo kwa ajili ya biashara, makazi na huduma za jamii kwenye eneo moja.

(iv) Kuongeza mapato ya Serikali na Shirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya wananchi waliopanga katika nyumba za shirika hawajaondolewa kwenye majengo yaliyomo kwenye mipango ya kuendelezwa, taratibu za kisheria hufuatwa ikiwa ni pamoja na kutoa *notice* ya miezi sita kwa wapangaji ili wapishe ujenzi. jambo hili liko ndani ya mikataba ya upangishaji.

Vile vile wapangaji waliokuwa wakiishi kwenye majengo yaliyobomolewa hupewa nafasi ya kwanza kuwa wapangaji kwenye majengo mapya kwa kuzingatia masharti mapya ya mkataba.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaoingia ubia na shirika la nyumba la Taifa ni wale wenye uwezo na malengo ya kuwekeza, siyo kila mpangaji anauwezo na nia ya kuwekeza katika sekta ya majengo. Aidha, natoa wito kwa Watanzania wenye nia ya

kushirikiana na Shirika la Nyumba la Taifa katika kujenga upya majengo machakavu katikati ya miji au kujenga majengo mapya nje ya miji wanakaribishwa.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa shirika la nyumba la Taifa halina mpango wa kuwauzia wapangaji wanaoishi kwenye majengo ya ghorofa yaani *flats*. Hata hivyo, kwa sasa Serikali inaandaa sheria itakayowezesha wananchi kununua na kumiliki *flats* ambayo itawakilishwa katika kikao kijacho Bungeni hivi karibuni.

Mara sheria hii itakapopitishwa na Bunge, Shirika litafanya tathmini na kuona kama litapata faida kutokana na mauzo ya nyumba za ghorofa kwa wapangaji wake.

**MHE. MOHAMMED RISHED ABDALLAH:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na mipango mizuri ya Serikali ya kuendeleza Miji yetu na kupendeza, Je, Serikali ina mikakati gani ya kushirikiana na Halmashauri husika katika maeneo hayo kuhakikisha kwamba Miundombinu ya maji taka na Maji safi inaenda sambamba na ujenzi wa maghorofa haya katika Miji yetu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Rished Abdallah,Mbunge wa Pangani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la ujenzi wa nyumba Mijini na kupendezesha Miji yetu haliwezi kufanywa na Shirika la Nyumba peke yake wala Serikali Kuu peke yake, ni jukumu ambalo tungependa wadau mbalimbali washiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti wadau hao ni pamoja na Serikali za Miji ama Manispaa na watu binafsi. Kwa hiyo, natoa wito katika Halmashauri yeyote pamoja na Pangani tupo tayari kushirikiana nao. Shirika la Nyumba nalo tutashirikiana nao kama wakitoa viwanja na wakiwa tayari nao kuchangia tupo tayari kushirikiana ili kuboresha Mji wa Pangani na Miji mbalimbali.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali kwa mujibu wa kanuni umepita na kwa kuwa tumeweza kumaliza maswali yaliyopangwa leo isipokuwa lile moja la kimaslahi, naomba tuendelee na matangazo na ajenda zinazofuata.

Waheshimiwa Wabunge ningependa niwafahamishe kwamba baada ya matangazo tutaingia kwenye ajenda muhimu sana ya uchaguzi wa wajumbe katika maeneo makubwa mawili kadri itakavyotolewa maelekezo. Nikianza na matangazo ambayo yapo mezani kwangu katika siku hii ya leo, kwanza kabisa naomba nitambue uwepo wa Mheshimiwa Yusuf Makamba, Mbunge katika ukumbi wetu wa Bunge na leo ameungana nasi katika shughuli zetu za Bunge. ninaomba pia sasa niwatambue wageni wengine ambao wapo ndani ya Bunge letu kwa siku ya leo.

Kuna wageni wa Mheshimiwa George Lubeleje Mbunge wa Mpwapwa, ambao ni Pastor Solomoni Matando, kutoka Mpwapwa na Pastor Sunday Isaya, kutoka Mpwapwa

hao naona ni Wachungaji wenzake na Mheshimiwa Lubeleje, karibuni sana.

Tunakushukuru sana Mheshimiwa Lubeleje kwa kutuletea Wachungaji wenzako *(Makofi/ Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge ninaomba pia nitambue mgeni wa Mheshimiwa Janeth Kahama ambaye ni Bi. Shadya, Katibu Kata kutoka Dar es Salaam. Naomba pia nitambue uwepo wa ujumbe wa Serikali ya Wanafunzi ya Chuo Kikuu cha Waislam cha Morogoro arobaini wakiuongozwa na Rais wao Khamis Rajab, Makamu wa Rais Shekha Ali Khamis, Waziri Mkuu wa Chuo hicho ambaye ni Adam Mollel, Katibu Mkuu Kiongozi Maulid Shibu, Katibu Mkuu wa Usafirishaji ambaye ni Waziri Rajabu. Naomba tutambue uwepo wa Wanafunzi 31 pamoja na Walimu 3 kutoka Dar *U I Muslim Education Centre,* karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge naomba pia mumfahamu mgeni wa Mheshimiwa Jenister Mhagama, Mwalimu mwenzake Bibi Rose Magilima akifuatana na watoto wake wawili John Junior na Justin Katabwa. Karibu sana Bibi Rose, tumesoma naye huko kwenye chuo kimoja tulikuwa pamoja.

Waheshimiwa Wabunge ninazo taarifa za vikao, ninaomba niwape taarifa za kikao kutoka kwa Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo Mifugo na Maji, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo saa sita mchana kutakuwa na kikao katika ukumbi namba 227 ghorofa ya pili katika jengo la utawala.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Wilson Masilingi Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati hiyo leo tarehe 23 mwezi wa nne saa tano asubuhi kutakuwa kikao cha Kamati ukumbi namba 219 jengo la utawala lakini nitaomba Mheshimiwa Masilingi kwa heshima ya Kamati yako labda Kamati hiyo ingekutana baada ya uchaguzi ambao utaendelea hivi punde.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa William Shelukindo, Mbunge na Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini watakuwa na kikao leo saa saba mchana katika ukumbi namba 432 ghorofa ya nne katika jengo la utawala.

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwatangazie pia Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi, leo kutakuwa na Kikao cha Wabunge wote wa (*CCM*) katika ukumbi wa Pius Msekwa.

Lakini kikao hicho kitafanyika mara baada ya kuahirisha Bunge jioni ya leo. Muda wowote Bunge litakapoahirishwa kikao hicho kitaanza katika ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge nina tangazo la semina, nimeletewa tangazo la semina kutoka kwenye ofisi ya Katibu wetu wa Bunge kwamba leo tarehe 23 kutakuwa na semina kwa Waheshimiwa Wabunge wote, semina hiyo itahusu Mkataba wa ubia wa uchumi, *Economic Partnership Agreement* (*EPA*) itaanza saa saba mchana katika ukumbi

wa Pius Msekwa na inategemewa kumalizika muda wa saa 10.15 jioni. Semina hiyo imeandaliwa na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Semina hiyo ni muhimu sana Waheshimiwa Wabunge pamoja na shughuli zingine zote tunaomba muwe na muda wa kuhudhuria semina hiyo.

Waheshimiwa Wabunge nimeletewa tangazo jingine hapa la mgeni, Mheshimiwa Shellukindo ameniomba kwamba na yeye ana mgeni wake ambaye ni Mheshimiwa Charles Ndege, Diwani wa Kata ya Mamba Jimbo la Bumbuli, naomba Mheshimiwa Ndege asimame ili tuweze kumtambua.Baada ya shughuli ya uchaguzi mnakumbuka kwamba jana taarifa mbili za Kamati ziliwekwa mezani na zitajadiliwa leo na tayari nimeshapokea majina 12 ya wachangiaji kwa ajili ya hoja ya Kamati ya Hesabu za Serikali (*PAC*)na hoja ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, (*LAAC*) na kama kuna wengine wanaweza kuomba halafu tutaona kama muda unaturuhusu kwa wachangiaji hao

Waheshimiwa Wabunge ninalo tangazo jingine kutoka kwa Mheshimiwa Kilasi, anawaomba Mheshimiwa Masilingi, Mheshimiwa Mshashu, Mheshimiwa Sendeka, Mheshimiwa Seleli, Mheshimiwa Halima Mamuya, Mheshimiwa Naibu Spika, hayupo wakutane nao kwa ajili ya shughuli maalumu waliyopewa kutoka kwenye Ofisi ya Wabunge wa *CCM* hapa Dodoma.

Waheshimiwa Wabunge ninalo tangazo kutoka Mkoa wa Morogoro, Katibu wa Wabunge wa Mkoa wa Morogoro ameomba niwatangazie Wabunge wa Mkoa wa Morogoro kwa namna itakavyowezekana saa saba, baada ya kusitisha Bunge waone wanaweza wakakutana namna gani kwa kikao maalumu maeneo hayo ya ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge hayo ndiyo matangazo yaliyokuwa mezani kwangu nimeyamaliza naomba nimwite Katibu atuongoze kwa hatua inayofuata. Katibiu endelea na *Order Paper.*

**UCHAGUZI WA WAJUMBE**

(i) Bodi ya Chuo cha Ufundi Arusha; na

(ii) Mbunge mmoja kwenye Bunge la Afrika.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa kanuni zetu za Bunge, Kanuni namba 8 (2) (b) kinasema kwamba katika siku za uchaguzi kutakuwa na taratibu za kupiga kura, kanuni ya 9 inatoa maelekezo ya shughuli ya uchaguzi kwa wawakilishi mbalimbali ndani ya Bunge kwenye vyombo mbalimbali vinavyohusiana na Bunge letu, kadri ya orodha ya shughuli za Bunge leo tutakuwa na chaguzi mbili, tutakuwa na chaguzi ya kwanza ya bodi ya chuo cha ufundi Arusha Mjumbe mmoja na tutakuwa na uchaguzi wa pili wa Mbunge mmoja kwenye Bunge la Afrika.

Waheshimiwa Wabunge ikumbukwe kwamba Mwakilishi mmoja wa Bunge kwenye Bunge la Afrika, Mheshimiwa Dr. Wanyancha hivi karibuni ameteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Naibu Waziri, kwa hiyo nafasi hiyo iko wazi.

Waheshimiwa Wabunge vilevile kama nilivyosema tutakuwa na uchaguzi wa Mjumbe wa Bodi ya Chuo cha Ufundi Arusha, naomba nimwite Katibu atuongoze kwenye suala zima la uchaguzi kwa kadri ya maelezo niliyoyatoa.

**DR. THOMAS D. KASHILILAH - KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Uchaguzi wa Wajumbe, Bodi ya Chuo cha Ufundi Arusha, maelezo ya usimamizi wa Uchaguzi wa ujumbe wa Baraza la Chuo cha Ufundi Arusha.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyowatangazia tarehe 17-4- 2008, leo tarehe 23-4-2008 baada ya kipindi cha Maswali na Majibu na kama ilivyonakiliwa katika orodha ya shughuli za leo kutakuwa na uchaguzi wa Mjumbe Mmoja wa Baraza la Chuo cha Ufundi Arusha.

Mheshimiwa George Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, ndiye peke yake aliyechukua fomu na kurejesha (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taratibu za uchaguzi zinavyoelekeza, mgombea atapigiwa kura ya ndiyo au hapana. Kutokana na maelezo hayo mafupi na kwa mujibu wa kanuni za Bunge zinazohusika na uchaguzi wa Wabunge wanaokwenda kuliwakilisha Bunge katika vyombo vingine na kwa mujibu wa Kifungu namba 8(2) (b) cha nyongeza ya pili ya kanuni za Bunge, mgombea atatakiwa afike mbele ya Bunge hili kujieleza na kuomba kura baada ya kujieleza karatasi za kupigia kura zitasambazwa.

Karatasi ya kupigia kura itakuwa na jina moja la Mheshimiwa Mbunge Simbachawene, unachotakiwa ni kupiga kura ya ndiyo au hapana katika jina la Mgombea, naomba kuwasilisha taratibu za uchaguzi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge naomba nimshukuru sana Katibu wa Bunge kwa kutoa maelekezo ya uchaguzi

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:**Kuhusu utaratibu, naomba nitoe rai kwamba kwa kuwa tuna mambo ya kufanya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kaboyonga kanuni namba ngapi?

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Kanuni namba 68, kwa kuwa ratiba yetu ina mambo mengi ya kufanya na kwa kuwa Mjumbe aliyejitokeza ni mmoja, nashauri tupige kura ya ndiyo au hapana kwa sauti ili tumuidhinishe. (*Makofi*/K*icheko*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kaboyonga nimepokea mwongozo wako wa kuomba utaratibu katika suala hili la uchaguzi wa leo. Lakini Waheshimiwa Wabunge Bunge hili linaongozwa na kanuni. Kanuni ni lazima ifuatwe kulingana na taratibu iliyopo mezani, katika suala la ndiyo ama hapana linagusa maamuzi ya shughuli kadhaa. Lakini si katika eneo la upigaji wa kura. Eneo la upigaji wa kura kanuni sehemu ya 6 kanuni namba 8 kipengele cha 1 na 2 (a) na (b) kinasisitiza suala la kupiga kura. Kwa

hiyo, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge shughuli zilizopangwa leo zimepangwa kulingana na muda tulionao na nitaomba kwa kuwa mgombea wetu ni mmoja haitatuchukua muda mrefu ninaomba tutulie tuende haraka ili tuendane na kanuni yetu ya Bunge.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Kuhusu utaratibu, Kanuni 68, Kwa kuwa kanuni inatungwa na Bunge, na kanuni hiyohiyo inaweza kutenguliwa na Bunge, na kwa kuwa tumekuwa na mazoea ya kufanya hivyo hata tunapopiga kura. Je tukitengua kanuni hiyo ili tuweze kupiga kura ya ndiyo au hapana tutakuwa tumeokoa muda, tutakuwa tumevunja kanuni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba tutengue Kanuni hiyo ili tupige kura ya ndiyo au hapana kwa sauti. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane. Kwa kuwa Kanuni inasema, Mbunge akitoa hoja na hoja hiyo ikiungwa mkono na Wabunge wasiopungua 10, hoja hiyo itaamuliwa kwa maneno na ikikubalika basi Spika au *Residing Officer* yeyote atafanyia utekelezaji kuhusu maamuzi hayo. Sasa nitawahoji wanaounga mkono kutenguliwa kwa muda kwa Kanuni hiyo kulingana na maelezo na hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Nyami na kuungwa mkono na Waheshimiwa Wabunge wasiopungua 10.

**MHE. YAHAYA K. ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Kura ya Ndiyo au Hapana kwa sauti ilipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninaomba nimsimamishe Mheshimiwa Simbachawene pale alipo ili tumuone na tuweze kumpigia kura yetu kulingana na Mwongozo alioutoa Mheshimiwa Nyami. (*Makofi*)

*(Hapa Mheshimiwa George B. Simbachawene Alisimama)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hapa Mhe. George B. Simbachawene alichaguliwa na Bunge kwa kauli moja* kuwa Mjumbe *Mwakilishi wa Bodi ya Chuo cha Ufundi Arusha)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa heshima na taadhima, ninaomba sasa kumtangaza Mheshimiwa George Simbachawene kwamba amechaguliwa na

kupitishwa na Bunge kwa kura zote kuwa Mjumbe Mwakilishi wa Bodi ya Chuo cha Ufundi Arusha kutokea kwenye Bunge letu (*Makofi*)

**DR. THOMAS D. KASHILILAH - KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa desturi anayechaguliwa huwa anatoa shukrani

**WABUNGE FULANI:** Baadaye.

**MWENYEKITI:** Katibu anayechaguliwa huwa anatoa shukrani baadaye tukishamaliza chaguzi zote mbili

**DR. THOMAS D. KASHILILAH - KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti kwa mujibu wa kanuni nikiwa kama msimamizi wa uchaguzi ninaomba kuthibitisha kwamba Mheshimiwa Boniface Simbachawene amechaguliwa kuwa Mjumbe wa Chuo cha Ufundi Arusha(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya usimamizi wa uchaguzi Bunge la Afrika, Waheshimiwa Wabunge kama nilivyowatangazia tarehe 17 Aprili, 2008 kwamba leo baada ya kipindi cha maswali na kama ilivyonakiliwa katika orodha ya shughuli za leo kutakuwa na uchaguzi mmoja kuziba nafasi ya kundi (c) Wabunge wanaume Tanzania Bara iliyoachwa wazi na Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, aliyeteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, aliyekuwa mwakilishi katika Bunge la Afrika.

Waheshimiwa Wabunge waliojitokeza kuchukua fomu walikuwa Wabunge wawili, muda na mwisho wa kurudisha fomu ilikuwa ni jumatatu tarehe 21Aprili, 2008 saa 10.00 jioni muda huo ulipowadia Waheshimiwa Wabunge wawili walirejesha fomu ambao ni Mheshimiwa Mohammed Rished Abdallah na Mheshimiwa Prof. Feetham Banyikwa (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo waheshimiwa Wabunge wote wawili watapigiwa kura na atakayepata kura nyingi ndiye atakayekuwa amechaguliwa, kutokana na maelezo hayo mafupi na kwa mujibu wa kanuni za Bunge zinazohusika na uchaguzi wa Bunge kuwakilisha katika Bunge la Afrika na kwa mujibu wa kifungu cha tisa cha nyongeza ya 5 ya kanuni za Bunge kila mgombea atatikwa afike mbele ya Waheshimiwa Wabunge kujieleza kwa lugha ya kiingereza ambaye ni moja ya lugha zinazotumika katika Bunge la Afrika na kuuliza maswali na kujibu kwa lugha hiyo hiyo, baada ya kujieleza karatasi ya kupiga kura zitatolewa na itakuwa ni moja, kila Mheshimiwa Mbunge atatakiwa kupiga kura katika jina la Mgombea mmoja ili kupata jina moja, naomba kuwasilisha maelezo na taratibu za uchaguzi.

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mwongozo wa Kiti!

**MWENYEKITI:** Mwongozo wa Kiti.

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Kwa kuwa katika Bunge la Afrika kuna lugha tano ambazo ndizo zinazotumiwa: Kingereza, Kifaransa, Kireno, Kiarabu na Kiswahili.

Kwa nini wagombea wasiruhusiwe kutumia lugha yoyote Kiswahili kikiwa Lugha ya Taifa hili? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninaomba nipokee mwongozo kutoka kwa Mheshimiwa Athumani Janguo ambaye pia ni Mbunge wa Bunge la Afrika.

Kwa kuwa Mheshimiwa Janguo, ametuthibishia ndani ya Bunge la Afrika kuwa kuna lugha zisizopungua tano ambazo zinatumika katika Bunge hilo basi ningemwomba Mheshimiwa Janguo, kama anaona umuhimu wa kutumia Lugha ya Kiswahili kama lugha yetu ya Taifa basi angetumia utaratibu wa kutoa hoja na ikiungwa mkono, tungeweza kutengua hiyo Kanuni ya 9 na tukawaruhusu wagombea wetu wakatumia lugha ya Kiswahili kama lugha yetu ya Taifa.

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni zetu, Kanuni ya 68 natoa hoja kwamba ulazima wa kutumia Lugha ya Kingereza utenguliwe kwa muda na wagombea wetu waruhusiwe kutumia lugha zote za Kingereza na Kiswahili katika jitihada za kukiimarisha Kiswahili kama lugha ya Taifa hili. Naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, na katika masuala yanayotuhusu tunaunga kweli mkono hoja hizi. (*Makofi*)

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, bila kupoteza muda ninawaomba wagombea wote wawili wasimame pale walipo. Nitawaomba watoke nje. Waheshimiwa Wabunge, naomba tufuate utaratibu. Ninaomba watoke nje na ataingia mmoja baada ya mwingine ili ajieleze na kuomba kura mbele ya Wabunge. Waheshimiwa Wabunge, mnafikiri tuwape dakika ngapi za kujieleza? (*Makofi*)

**WABUNGE:** Tatu, tano?

**MWENYEKITI:** Wanaosema tatu, tano? Wanaosema tatu wameshinda. (*Makofi*)

Katibu naomba uniitie Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah. Waheshimiwa Wabunge, utaratibu wa uchaguzi hatuanzi kushangilia kabla ya kupiga kura. Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah mbele yako ni Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wako mbele yako kukusikiliza ukiomba wakuchague kuwa miongoni mwa Wabunge watakaoliwakilisha Bunge letu kwenye Bunge la Afrika. Unapewa dakika tatu za kujieleza na utaulizwa maswali kama yatakuwepo. Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah karibu!

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** *Honorable Chair Person, Honorable Ministers, Honorable Deputy Ministers, Honorable colleagues Members of*

*Parliament, my name is Mohamed Rished Abdallah, standing before you, and asking you to vote for me to represent this Parliament at Pan African Parliamentary.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini nina uwezo na uzoefu wa kutosha wa kuliwakilisha Bunge hili ili niweze kuliwakilisha vizuri Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Manaibu na Waheshimiwa Wabunge wenzangu naomba kura zenu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kuna swali?

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Mbunge, *candidate* wa kwenda *PAP* utakapofika *Oliver Tambo Airport* ukatoka *East Gate*, ukafika *Midrand* na ukakiona kibao kimeandikwa *PAP* itakuwa na maana gani?

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mimi nafikiri hili si swali. Kuna swali jingine? (*Makofi*)

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile Bunge la Afrika kama tulivyoambiwa kuna lugha tano zinazozungumza, nilitaka kumuuliza je, mgombea anajua lugha ngapi?

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hilo ni swali la msingi.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, napenda nimjibu Mheshimiwa Ali Tarab Ali, kama ifuatavyo: Nimesoma shule ya msingi kwa lugha ya Kingereza. Nimesoma sekondari yangu kwa lugha ya kiarabu. Nimechukua kozi ya lugha ya Kireno na nimefanya kazi Msumbiji miaka 11 kwa hiyo, Kireno nakifahamu. Lakini vilevile Mungu amenijalia kuwa na lugha ya kuzaliwa ambayo ni Kiswahili. Kwa hiyo, nazungumza lugha nne. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Maswali? Mheshimiwa Rished naomba uchukue nafasi yako.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Waheshimiwa Wajumbe naomba kura zenu.

**MWENYEKITI:** Katibu naomba uniitie Mheshimiwa Prof. Feetham Banyikwa.

*(Hapa Mheshimiwa Prof. Feetham Phillip Banyikwa*
*Aliingia Ukumbini)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tuendelee kufuata utaratibu, haturuhusiwi kupiga makofi kabla aliyeshinda hajatangazwa. Mheshimiwa Profesa Feetham Filipo Banyikwa, mbele yako ni Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wako mbele yako kukusikiliza ukiwaomba wakupigie kura ili

wakuchague uwe mwakilishi wa Bunge letu katika Bunge la Afrika. Mheshimiwa Profesa unapewa dakika tatu za kujieleza na kama kutakuwa na maswali ya msingi utaulizwa ili uyajibu mbele ya Bunge hili. Mheshimiwa Profesa karibu!

**MHE. PROF. FEETHAM P. BANYIKWA:** *Honourable Chairperson Jenista Mhagama, Honorable Prime Minister, currently absent, Honourable Ministers, I think all are present, Honorable Deputy Ministers, Members of Parliament, the person standing in front of you is Professor Feetham Phillip Banyikwa, a Member of Parliament for Ngara Constituency. (Applause)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge naomba nisisitize utaratibu wa makofi, atakayerudia nitatumia kanuni kumtoa nje ya ukumbi.

**MHE. PROF. FEETHAM P. BANYIKWA:** *I stand here to seek your votes so that I can represent this Parliament in the Pan African Parliament. My CV was circulated earlier, Honorable Members of Parliament I have been a Member of Parliament for two years now. I have gathered enough experience and I think I have all the required qualifications to represent you in the Pan African Parliament. It is my sincere hope that you are going to give me all the winning votes so that I can go and represent this House in the Pan African Parliament, thanks a lot.*

**MWENYEKITI**: Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Waheshimiwa Wabunge kuna swali, kuna swali, kuna swali?

**WABUNGE**: Hakuna.

**MWENYEKITI**: Kuna swali pale karibu Mheshimiwa!

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana nataka kumuuliza Mheshimiwa Mbunge. Tarehe 23 Aprili, 2008 ana kumbukumbu gani jambo lililotokea kwenye ukumbi huu wa Bunge hapa Dodoma? *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge hatufanyi uchaguzi wa Bunge hili hapa ndani, sasa kumbukumbu za kuhusu shughuli zilizojitokeza humu ndani mimi nafikiri kwa kweli hilo sio swali. (*Makofi*)

Maswali, Mheshimiwa Kevela, ooh, Mheshimiwa *Bishop*, Mpesya!

**MHE. BENISON M. MPESYA**: *Thank you very much Honourable chairperson, I have the question to ask the learned Professor. Could you please tell us what are the motives that drive you to contest for this particular post?*

**MHE. PROF. FEETHAM P. BANYIKWA:** *Honourable Chairperson, thanks for the question. I have been a Professor for 30 years, 15 years at the University of Dar es Salaam, and 15 years as a research Professor at the University of Central New York, USA. Now, for the past two years I have been a Member of Parliament. What drives me*

*to go further beyond the borders of Tanzania is to check my skills and represent my country at international level. I think I have done enough already in this country. Now I am aspiring to go abroad in the continent of Africa so that I can see to what extend I can represent you and represent my zeal to do the best that is possible before I reach the age of retirement.* (*Applause*)

**MWENYEKITI**: Maswali? Profesa asante unaweza ukachukua nafasi yako. Katibu naomba idadi ya wapiga kura.

*(Hapa Mheshimwa Prof. Banyikwa alikwenda kukaa kwenye nafasi yake)*

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge, sasa tutaanza kazi yetu ya kupiga kura kwa mujibu wa orodha niliyopewa na Katibu wa Bunge. Tuko Wabunge 323, lakini waliopo ndani kwa sasa ni Wabunge 216, kwa hiyo, idadi hiyo inaturuhusu kabisa kuendelea na zoezi letu. Nitawaomba vijana wetu walioko hapa ndani wanaongozwa na meza ya Katibu sasa watugawie makaratasi na tutaanza kupiga kura. Lakini kabla hatujapiga tutapiga kengele angalau kwa dakika tatu kama kuna yeyote ambaye yuko nje aingie ndani na zoezi liweze kuendelea.

*(Hapa Kengele ilipigwa ili walioko nje waweze kuingia ndani)*

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge, ninawaruhusu waanze kugawa karatasi za kupigia kura. Kengele imekwishapigwa na kwa mujibu wa kengele yetu ilivyo sasa hivi inasikika nje na sio ndani ya ukumbi. Kwa hiyo, ninaomba waendelee kugawa karatasi na nitaomba atakayeingia atakuwa ana ripoti kwenye meza ili tuweze kuona idadi ya wapiga kura ni wangapi.

*(Hapa Karatasi za Kura ziligawiwa)*

**MWENYEKITI**: Tafadhali sana unapigia kura jina moja tu. Mheshimiwa Maneno tayari umekwishaingizwa kwenye orodha. Waheshimiwa Wabunge kuna yeyote ambaye bado hajapata karatasi? Bado Waheshimiwa Wabunge naomba myathibitishe maboksi ya kukusanya kura, yako matupu na hayana kitu ili vijana wetu waanze kukusanya karatasi ambazo zimekwishapigwa.

*(Hapa maboksi ya kukusanya kura yalionyeshwa kwa Waheshimiwa Wabunge yakiwa matupu)*

**MWENYEKITI**: Naomba muanze kukusanya.

*(Hapa kura zilikusanywa)*

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge, nimegundua kuna watu hawajapata karatasi za kupigia kura. Nimeuliza kama mtu hajapata anyoshe mkono ili aweze kupewa. Waheshimiwa Wabunge tumeshakusanya karatasi zetu wote. Kwa mujibu wa kanuni ya 8(4) inasema kwamba sanduku la kura litawekwa chini ya usimamizi wa

Katibu pamoja na Wabunge wawili waliochagulia kuhesabu kura mpaka wakati wa kuhesabu kura utakapofika.

Waheshimiwa Wabunge naomba kupendekeza mbele yenu majina ya Waheshimiwa Wabunge wawili ambao watatusaidia kusimamia zoezi la kuhesabu kura mpaka pale tutakapopatiwa matokeo ya uchaguzi huu. Ninampendekeza mbele yenu Mheshimiwa Magdalena Sakaya na Mheshimiwa George Malima Lubeleje. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Kura nyingine hazijakusanywa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa George Lubeleje, Waheshimiwa Wabunge tunawaafiki hawa wakawe wasimamizi wetu?

**WABUNGE WOTE:** Ndiyo!

**MWENYEKITI:** Naomba waje mbele waweze kuongozana na masunduku haya pamoja na Katibu wetu wa Bunge. Waheshimiwa Wabunge wote tumeshakusanya karatasi zetu? Haya kuna ombi kwamba wagombea nao kama wanaridhika na uteuzi wangu.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nampendekeza Mheshimiwa Msambya kama wakili wangu.

**MWENYEKITI**: Haya ruksa Mheshimiwa Msambya.

**MHE. PROF. FEETHAM P. BANYIKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naiamini meza.

**MWENYEKITI**: Nakushukuru sana, Mheshimiwa Msambya naomba uongozane na Mheshimiwa George Lubeleje na Mheshimiwa Magdalena Sakaya na Katibu wa Bunge ili kuhakikisha zoezi hilo linafanyika kwa umakini. Katibu wa Bunge mnaweza kuendelea Katibu hatua inayofuata.

## HOJA ZA KAMATI

## TAARIFA YA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI *(PAC)* YA MWAKA 2005/2006

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tuendelee na ajenda inayofuata ya hoja za Kamati na mara matokeo yatakapokuwa tayari basi tutatangaza utaratibu wa namna gani tutatoa utaratibu wa kutangaza matokeo haya mbele ya Bunge letu. Lakini kwa kuwa zoezi la kuhesabu linaendelea basi ningewaomba tuendelee na hoja za Kamati kama Katibu alivyotoa muongozo.

Waheshimiwa Wabunge hoja za Kamati mbele yetu ziko mbili, tumekubaliana hoja hizo zitawasilishwa kwa pamoja na zitajadiliwa kwa pamoja lakini zitaamuliwa

moja baada ya nyingine. Kwa hiyo, bila ya kupoteza muda nimwombe kwa heshima na taadhima Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali ili aje mbele ya Bunge na kuwasilisha hoja ya Kamati yake, Mheshimiwa John Cheyo!

**MHE. JOHN M. CHEYO – MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 114(15) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali ya Mwaka wa Fedha wa 2004/005 na 2005/2006 ili lijadili na kutoa maamuzi.

Awali ya yote naomba kuwapongeza na kuwashukuru kwa ushirikiano na kazi nzuri waliyofanya waliokuwa wajumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali wakati wa vikao vyote vya Kamati kwa kufanya uchambuzi wa kina na kutoa michango na maoni mbalimbali wakati Kamati ilipokuwa ikichambua na kujadili mafungu (*votes*) mbalimbali ya Serikali, Mikoa na Idara zinazojitegemea. Michango hiyo imesaidia kuboresha na kujenga dhana ya kuwepo nidhamu ya matumizi ya fedha na mali za Serikali kulingana na Sheria, taratibu na Kanuni zilizopo.

Matokeo ya hesabu za Serikali kwamba asilimia ya hati safi imeongezeka kutoka asilimia 56 mwaka 2005/2006 kufikia 74 mwaka 2006/2007 ni ushahidi tosha kwamba kazi ya Kamati ilikuwa nzuri. Aidha, Kamati ilisaidiwa sana na juhudi za Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliposisitiza umuhimu wa Serikali kuwajibika katika kutunza mahesabu ya fedha za umma katika semina za maofisa Wahasibu wote nchini. Kamati inamshukuru sana Rais kwa kuwa makini katika jambo hili muhimu. Kamati inawashukuru Maofisa Masuhuli wote waliotekeleza maagizo ya Kamati na ongezeko la hati safi lililotajwa katika Taarifa ya *CAG* mwaka 2006/2007 ni matokeo ya jitihada za maofisa Masuhuli.

Taarifa inayowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu ni ya Kamati iliyomaliza muda wake Februari, 2006 mpaka Februari, 2008 na ni ya pili katika uhai wa Bunge hili (2005-2010). Kwa heshima kubwa naomba kuwatambua kwa kuwataja majina kama ifuatavyo: Mheshmiwa John M. Cheyo,Mwenyekiti, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Fatma A. Fereji, Mheshimiwa Felista A. Bura, Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu, Mheshimiwa William V. Lukuvi, Mheshimiwa Zubeir A. Maulid, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya, Mheshimiwa Damas P. Nakei, Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami na Katibu Ndugu James J. Warburg.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Wajumbe wa Kamati mpya wamejadili Taarifa hii na kuiridhia. Nawashukuru sana kwa kuibariki na naomba Bunge lako Tukufu liwatambue kwa kuwataja majina kama ifuatavyo: Mheshimiwa John M. Cheyo, Mwenyekiti, Mheshimiwa Zubein A. Maulid, Makamu Mwenyekiti,. Mheshimiwa Mohamed R. Abdallah, Mheshimiwa Alyce B. Kimaro, Mheshimiwa Issa Kassim Issa, Mheshimiwa Hasnain G. Dewji, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mheshimiwa Pansiano D. Nyami,

Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Mheshimiwa Severina S. Mwijage, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Ali Haji Ali, Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, na Mheshimiwa Manju S. Msambya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza kazi zake Kamati ilikuwa ikisaidiwa na Maafisa Waandamizi kutoka Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Mhakiki Mkuu wa Mali za Serikali, na Sekretarieti ya Ofisi ya Katibu wa Bunge. Nawashukuru sana kwa mchango wao wa kitalaamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misingi muhimu inayoongoza utendaji wa kazi za Kamati, katika utendaji wa kazi Kamati iliongozwa na misingi muhimu ifuatayo: Sheria ya Fedha ambayo inamwelekeza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kufanya kazi yake ya ukaguzi kwa niaba ya Bunge.

Kanuni za Bunge ambazo ndiyo sisi tumewekwa kwa Kanuni ya Bunge hili Tukufu kuweza kuangalia Mahesabu ya Serikali.

Kanuni za Waziri wa Fedha ambazo zinamwambia Afisa Mhasibu kwamba yeye anawajibika binafsi kwa shughuli zote ambazo amepewa katika Idara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na misingi hiyo msingi wa kwanza kabisa ni Katiba ya Tanzania, Ibara ya 63, inayotamka kama ifuatavyo: ‘Sehemu ya Pili ya Bunge itakuwa ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka, kwa niaba ya wananchi, kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii’.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya majukumu makuu ya Serikali ni kukusanya kodi na fedha kutoka vyanzo mbalimbali vya walipa Kodi na kutumia fedha hizo kama vile Bunge lako Tukufu lilivyoidhinisha katika Mkutano wa Bajeti. Kazi yetu kama Bunge ni kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali. Bunge lako Tukufu linatoa jukumu hili kwa kutumia Kamati mbalimbali. Kazi ya Kamati ya Hesabu za Serikali ni kukagua mahesabu ya Serikali *(financial audit),* na utekelezaji wa malengo ya bajeti *(performance audit)* na kuishauri serikali katika matumizi bora na endelevu ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashauri Bunge lako Tukufu lijielekeze kwenye Sura ya Saba ya Katiba, Ibara ya 133 mpaka 144 (Masharti kuhusu Fedha za Jamhuri ya Muungano), na kwa msisitizo mambo yafuatayo yaangaliwe kwa makini:-

(a) Fedha za Serikali haziwezi kutumika bila Sheria iliyotungwa na Bunge (Ibara ya 136).

(b) Hakuna Kodi ya aina yoyote itakayotozwa isipokuwa kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge (Ibara ya 138).

(c) Majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (Ibara ya 143) ambayo ni pamoja na kuhakikisha kwamba fedha zitatoka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kwa matumizi yaliyoidhinishwa na Bunge, na angalau mara moja kwa Mwaka kukagua mahesabu yote ya Serikali pamoja na Bunge na kupeleka taarifa ya Ukaguzi kwa Rais. Aidha, Rais anawajibika kuwaagiza watu wanaohusika wawasilishe taarifa hiyo kwenye kikao cha kwanza cha Bunge kitakachofuata baada ya Rais kupokea taarifa hiyo na itabidi iwasilishwe katika kikao hicho kabla ya kupita siku saba tangu siku ile kikao kilipoanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Katiba katika eneo hili umepewa nguvu ya kisheria katika Sheria ya Fedha *(Public Finance Act No.6)* kama ilivyorekebisha mwaka 2004. Tunashauri Waheshimiwa Wabunge wajielekeze zaidi kwenye sehemu ya nne hadi ya saba ya sheria hii. Sheria inasisitiza kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu atafanya kazi yake ya Ukaguzi kwa niaba ya Bunge.

Nanukuu kifungu 31(1): *"the Controller and Auditor General shall on behalf of the National Assembly examine, inquire into and audit the accounts submitted to him under section 25 of this Act and perform any other functions which he is authorized to perform by or under this Act."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria katika ibara ya 44 kifungu cha (2) inatoa nguvu ya kisheria kwa yeyote yule atakayekataa kutoa taarifa au ushirikiano na Bunge hili kupitia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Anaweza kufungwa mpaka miaka miwili, kupewa faini ya shilingi laki tano au vyote viwili kwa pamoja.

Chimbuko la Kamati za Bunge pia linatokana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Toleo la 1977, Ibara ya 96(1) kama inavyonukuliwa hapa: "Bunge laweza Kuunda Kamati za Bunge za namna mbalimbali kadri litakavyoona inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora wa madaraka yake".

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** hivyo kwa mujibu wa Kifugu hiki majukumu ya Kamati ya Hesabu za Serikali yameainishwa katika Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, Nyongeza ya Nane (8) Kifungu cha 10, kama ifuatavyo:-

(a) Kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika Wizara za Serikali yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

(b) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwisha kutolewa na Kamati hiyo yenye lengo la kuondoa matatizo hayo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika Wizara za Serikali; na

(c) Kutoa mapendekezo na ushauri kwa Wizara za Serikali kuhusu matumizi ya fedha za Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Kanuni zilizotengenezwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha chini ya Sheria ya Fedha *(Public Finance Act, No.6 of 2001)* Sehemu ya Pili

zimeeleza uwajibikaji wa Maafisa Wahasibu kwa Kamati ya Hesabu za Serikali *(PAC),* nanukuu: *"Every Accounting Officer shall be personally and pecuniarly responsible and accountable for the collection and receipt of all revenue or for all disbursements of expenditure in his vote, and shall be answerable to the Public Accounts Committee (PAC)."*

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Sheria ya Fedha inamtaka Mlipaji Mkuu wa Serikali *(Paymaster General)* kuteua Afisa wa Serikali atakayewajibika kwa fedha za Serikali katika eneo lake la kazi. Jukumu hili ni binafsi *(personal responsibility)* na sheria pamoja na Kanuni *(regulations)* zinaelekeza kwamba Afisa Mhasibu atawajibika binafsi (*personally held responsible*) kama inavyoelezwa katika Kanuni ya 5:-

*"Any Accounting Officer who authorizes or approves the use of public funds or property contrary to the provisions of the Act shall be accountable for any loss arising from that use and shall be required to make good the loss or be surcharged under these Regulations, even if he has ceased to hold that Office. In exercising his duties under these regulations, the Minister shall have power to:-*

*(a) Upon the recommendation by the Public Accounts Committee surcharge any accounting officer or any public officer as prescribed under the schedule of these regulations.*

*(b) Withdraw the appointment of any accounting officer upon the recommendation by the Paymaster General, where gross negligence in the performance of this duties has been proved by the Controller and Auditor General and confirmed by the Public Accounts Committee(PAC)".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huu kila Afisa Mhasibu anawajibika kufika mbele ya Kamati ya Bunge na kutetea utekelezaji wa bajeti ya Fungu lake na anaweza kuadhibiwa kwa mujibu wa sheria zilizopo. Bajeti ya nchi yetu inategemea fedha kutoka nje kwa asilimia 20 kwa Matumizi ya Kawaida na asilimia 80 kwa matumizi ya maendeleo na kwa hiyo, bajeti yetu ni tegemezi. Fedha hizi ni misaada kutoka nchi rafiki, misaada na mikopo yenye riba nafuu kutoka, kwa mfano: Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* na Benki ya Dunia (*WB)*. Fedha zote hutawaliwa na mikataba inayoitaka Serikali kutumia fedha hizi kwa makusudi na maeneo yaliyokubaliwa na kuidhinishwa na Bunge.

Kwa miaka ya karibuni kumekuwa na wimbi la kuiamini Serikali na kwa hiyo washiriki wengi wanaleta fedha zao moja kwa moja Hazina na Serikali inazipangia matumizi kufuatana na vipaumbele vilivyokubalika. Kwa lugha ya Kingereza mfumo huu wa msaada unaitwa "*General budget support*". Msingi huu unalitaka Bunge lako Tukufu kuwa makini katika kusimamia matumizi ya fedha hizi. Kazi ya Kamati yetu ni kuhakikisha kwamba Serikali inawajibika kwa matumizi ya fedha hizi. Kazi hii ya Bunge kupitia Kamati hii inawapa washirika wetu katika maendeleo ya nchi yetu (*development partners)* imani ya uwajibikaji wa fedha za walipa kodi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** taarifa iliyowasilishwa na Kamati kwenye meza yako ni muhimu sana katika kuonyesha utekelezaji wa jukumu la Bunge la kuisimamia Serikali kutekeleza jukumu lake la kibajeti. Wadau mbalimbali nchini na nje ya nchi wanaangalia ni jinsi gani na kwa ufanisi gani Bunge lako Tukufu linaweza kuisimamia Serikali kibajeti.

Wimbi la Ufisadi la karibuni linafanya kazi ya Bunge lako kuwa gumu sana. Ufisadi unaoletwa na maamuzi mabaya ya serikali katika mikataba ya madini, ubinafisaji wa rasilimali ya Taifa kama vile makaa ya mawe ya kiwira, mikataba ya umeme kama vile ya *Richmond* na malipo yasiyoelezeka ya shilingi bilioni 155 yaliyolipwa na Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania katika Mgodi wa Meremeta, ni ushahidi tosha kueleza umuhimu wa Bunge hili kuwa imara na katika kutekeleza kazi yake ya kuisimamia Serikali kupitia Kamati zake. Taarifa hii itasaidia kuonyesha upungufu uliomo katika mfumo mzima wa utekelezaji wa bajeti.

Ndani ya Kamati tumefanya kazi kwa kuweka mbele utaifa wetu na wananchi wetu na wa nje wanaogharamia matumizi yote ya Serikali kwa kujikamua kikodi au kulipia mikopo mbalimbali. Kwa fedha za walipa Kodi kuna itikadi moja tu nayo ni uwajibikaji kwa matumizi ya fedha za bajeti.

Matumaini ya Kamati ni kwamba Bunge litakemea matumizi mabaya na Ufisadi unaofanywa na viongozi na watumishi wa serikali na kuridhia mapendekezo ya Kamati na pia Bunge litasifu Maafisa Wahasibu pale inapostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** taarifa hii ina sehemu tano, yaani, utangulizi, pili masuala ya ujumla, tatu matokeo ya ukaguzi, nne maoni na mapendekezo ya kamati, tano hitimisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili, masuala ya jumla - mzunguko wa uwajibikaji *(Accountability loop)*, Serikali inapaswa kuwajibika kwa Bunge kwa fedha zote inazopewa na Bunge. Aidha, Katiba inamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukagua na kutoa taarifa kwa Bunge kupitia Ofisi ya Rais. Taarifa ya ukaguzi ndiyo msingi wa kazi za kamati na kwa uzoefu wa kimataifa *(International best practice)* ili Taarifa ya *CAG* iwe msingi wa kutathmini uwajibikaji wa serikali katika mapato na matumizi ya fedha na rasilimali za Taifa, taarifa ya *CAG* inapitia hatua zifutazo:-

Taarifa huwasiliswa Bungeni rasmi na Serikali. Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali siku hiyo hiyo hugawa taarifa kwa wabunge na hutoa taarifa kwa vyombo vya Habari na taarifa ya *CAG* inakuwa wazi kwa watu wote kuijadili na kuitumia ipasavyo. Kamati ya Hesabu za Serikali *(PAC)* huchukua Taarifa hiyo kwa ajili ya kuisoma na kuitafakari kwa kina na kuitolea maoni. *PAC* huwaita Maofisa Wahasibu kwa maelezo zaidi na maagizo. *PAC* huitolea taarifa na mapendekezo katika kikao cha Bunge Zima.

Serikali inawajibika kuyachukuwa mapendekezo ya Kamati kwa ajili ya kuyafanyia kazi na kujibu kupitia Ofisi ya Bunge *(Treasury Note).*

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** hatua ya serikali kujibu mapendekezo ya Kamati ndiyo inakamilisha mzunguko wa uwajibikaji. Kamati inasikitika kutoa taarifa kwamba tangu Mwaka uliopita Serikali iko kimya na haijajibu mapendekezo ya Kamati ya mwaka 2007.Ukimya huu wa Serikali unadhoofisha kazi ya Bunge ya kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake ya kibajeti kwa mujibu wa Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Kamati inasisitiza kuwa mzunguko huu wa Uwajibikaji ni muhimu na wote inabidi tuufuate kama njia ya kuonyesha kwamba wote tunajali na tunawajibika kwa fedha na rasilimali za taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inategemea sana uwezo, utaalamu na umahiri wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG).* Kamati imebaini kwamba ofisi hii inakabiliwa na matatizo ya kimsingi kwa muda mrefu. Kufuatana na uzoefu wa nchi zingine Kamati ilikotembelea kama vile *Denmark*, Uingereza, Namibia, *South Africa*, Australia na Kenya ofisi hii ina sheria yake mahususi inayoihakikishia uhuru *(independence)* wa kufanya kazi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi yetu ya *CAG* imeshikiliwa na Wizara ya Fedha kama mojawapo ya Idara yake. Utaratibu huu haukubaliki kimataifa hata kisheria nchini kwa sababu ofisi hii inaikagua serikali kwa niaba ya Bunge. Katika Sheria ya Fedha *(Public Finance Act, No.6)* kama ilivyorekebisha Mwaka 2004, sheria inasisitiza kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu anafanya kazi yake ya Ukaguzi kwa niaba ya Bunge. Tunanukuu kifungu cha 31(1) : *"the Controller and Auditor General shall on behalf of the National Assembly examine, inquire into and audit the accounts submitted to him under section 25 of this Act and perform any other functions which he is authorized to perform by or under this Act"* .

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha ofisi hii haina uhuru wa kuchagua watumishi wake na ina bajeti finyu inayoidhinishwa na Mkaguliwa wa Kwanza, yaani, Wizara ya fedha. Hali hii inaifanya ofisi ya *CAG* kimataifa ionekane kuwa ya kiwango cha chini *(low rating according to international supreme Audit Institutions Rating).* Nchi yetu inapata misaada mingi kutoka kwa washirika wa kimataifa *(development Partners)* na wengi sasa wanaleta fedha zao moja kwa moja kwenye mfuko mkuu hazina ili kufanikisha bajeti ya serikali *(general budget support).* Katika mikataba na serikali suala la kuwa na sheria mahususi kuongoza ofisi ya *CAG* ni moja ya vipengele vya mashariti ya kupewa hizi fedha kwa ajili ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilijadili umuhimu wa kuimarisha ofisi ya *CAG* kwa kuitungia sheria tarehe 16/18 Agosti, 2006 *Whitesand Hotel*. Katika mkutano wa 9 mwaka 2007 Serikali iliahidi kuwa sheria ingeletwa katika Mkutano wa Kumi wa Bunge hili na mpaka sasa sheria hiyo haijaletwa. Serikali inajua madhara yanayoweza kutokea kibajeti kama sheria hii haiji Bungeni kama vile ilivyo ahidiwa kwa Bunge na kwa washiriki katika bajeti yetu *(Development Partners).* Kamati inashindwa kuelewa ni kwa nini Wizara ya Fedha inachelewesha sheria hii na tunauliza kama suala ni uzembe au

ni makusudi ya kuinyonga ofisi hii ili ishindwe kutimiza wajibu wake kwa niaba ya Bunge.

Mhesimiwa Spika, Kamati inasisitiza kuwa sheria hii iletwe Bungeni kabla ya Mkutano wa Bajeti. Aidha, Kamati inatumia nafasi hii kumpongeza Mdhibiti na Mkaguzi Kuu wa Hesabu za Serikali na watumishi wote kwa kazi nzuri wanazofanya kwa niaba ya Bunge pamoja na mazingira magumu ya ofisi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi na Uwezo wa Kamati ya Hesabu za Serikali *(Capacity Building of the PAC)* kutekeleza majukumu yake kwa niaba ya Bunge ni jambo muhimu sana. Katika kipindi cha taarifa hii njia ambazo zimetumika kujenga uwezo wa Kamati ni pamoja na zifuatazo:

(i) Mafunzo ya wataalamu wa fedha kutoka *CAG*, Mhasibu Mkuu wa Serikali, Mamlaka ya Mapato Tanzania, *PPRA;* (ii)Mafunzo nchi za inje Uingereza, Australia, Denmark; (iii) Mafunzo katika mikutano *(conferences)* ya ushirikiano wa Kamati za Hesabu za Serikali kama vile *Eastern Africa Association of Public Accounts Committees (EAAPAC) na Southern Africa Development Community Organisation of Public Accounts Committee (SADCOPAC);* (iii) Mafunzo kwa kutembelea miradi iliyoombewa fedha Bungeni; na (iv) Uzoefu unaotokana na kuwahoji Maafisa Wahasibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatoa shukrani za dhati kwako na Ofisi yako kwa kuiwezesha kujenga Uwezo wa kutekeleza majukumu yake pamoja na hali ngumu ya kibajeti. Kwa kuwa Kamati ina wajumbe wapya wengi na changamoto zimeongezeka kama itakavyooneka hivi punde nguvu za ziada zinahitajika kuongeza uwezo wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti,, kwa kuzingatia hali halisi, Kamati za Bunge nyingi ulimwenguni sasa zina shughulika na kazi pana zaidi ya kuangalia Taarifa na vitabu vya mahesabu (*financial statements*) mezani. Kazi muhimu inayolikabili Bunge ni kuhakikisha kwamba fedha zilizotolewa na Bunge zimeleta thamani "*Value for money*". Suala hili linawezekana tu kama Kamati zinawezeshwa kusafiri na kuangalia miradi inayotekelezwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya *CAG* pia imepanua shughuli zake ambapo sasa inajikita katika ukaguzi wa thamani ya kazi iliyofanyika (*Value for Money)* na ukaguzi wa mazingira na miradi inayotekelezwa na fedha za wafadhili. Kwa mujibu wa sheria Taarifa zote za *CAG* ni lazima zije Bungeni na hatimaye zishughulikiwe na Kamati ya Hesabu za Serikali, Kamati ya Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa, Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma na Kamati zingine kama atakavyoelekeza Spika. Nchini *Denmark* na Uingereza asilimia 95 ya kazi za Kamati zinahusu maeneo haya ya *"value for money* ".

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mfumo wa bajeti ya serikali unajumuisha Washirika wa Maendeleo *(development partners-DP)* ambao pia wanataka kuhakikishiwa kwamba fedha zao zinasaidia Bajeti ya serikali (*General Budget Support* (*GBS)*, zinawafikia walengwa na miradi iliyokusudiwa. Aidha, wimbi la ufisadi lililoikumba nchi yetu linafanya wafadhili wetu wawe na wasiwasi juu ya fedha zao na

Mabunge yao yanauliza maswali juu ya uhakika wa matumizi wa fedha kupitia *GBS.* Hali hii inahitaji Bunge liwe na uwezo wa kuziwezesha Kamati zake zote hususan Kamati za *PAC*, *POC* na *LAAC* ziwe na uwezo mkubwa wa kutekeleza majukumu ili kukidhi mategemeo ya wadau wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati zinapaswa kuwa na makatibu wenye uwezo na kila Kamati iwe na watumishi wenye taaluma ya utafiti. Uwezo huu ndiyo tuliouona wakati Kamati ilipo tembelea Mabunge ya Uingereza, Australia, *Denmark* na Mabunge ya Afrika ya Mashariki yanaelekea huko. Kwa sasa Uganda wana mradi unaofadhiliwa na Benki ya Dunia wa Kuimarisha Kamati za Bunge kama *PAC.*

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Kamati inaunga mkono jitihada zako za kuhakisha kwamba mswada wa kuliwezesha Bunge kutumia Mfuko wa Bunge *(National Assembly Fund)* unaletwa Bungeni na kupitishwa kama sheria. Jambo hili likikamilika litakuwezesha wewe kutafuta vyanzo vingine vya mapato kwa ajili ya kuimarisha Kamati za Bunge hususan *PAC, POC,* na *LAAC*.

Kamati imeshiriki katika mchakato wa kutafuta vyanzo vingine vya kuimarisha uwezo wa Kamati na imebainika wazi kwamba mashirika kama Benki ya Dunia na Umoja wa Nchi za Ulaya *(EU)* zinaona umuhimu wa kuimarisha Bunge lifanye kazi yake ya kuisimamia Serikali kupitia mfumo wa Kamati za Bunge. Kamati inautakia mafanikio mchakato huu na tunaomba Bunge likuunge mkono katika jitihada zako za kuliimalisha Bunge lifanye kazi yake kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu tatu, inahusu matokeo ya ukaguzi. Dosari zilizosababisha kujitokeza Hoja za Ukaguzi katika Mafungu mbalimbali**.** Katika mafungu yote yaliyojadiliwa na Kamati, kwa muhtasari, hoja nyingi za ukaguzi zilihusisha kuwepo kwa dosari zifuatazo:-

(i) Maduhuli yasiyokusanywa;

(ii) Malipo yasiyokuwa na nyaraka na yenye Nyaraka pungufu;

(iii) Malipo yenye mashaka;

(iv) Malipo yaliyofanywa kwa kutumia Ankara Kifani *(Profoma Invoices);*

(v) Mali na vifaa kutorekodiwa vitabuni;

(vi) Upotevu wa fedha taslimu, mali na vifaa mbalimbali;

(vii) Kuwepo malimbikizo makubwa ya masurufu na mikopo isiyorejeshwa;

(viii) Kutofanyika kwa usuluhisho *(Reconciliation*) wa Hesabu za Benki na vitabuni;

(ix) Udhibiti dhaifu wa ndani katika kufuata taratibu za manunuzi na utunzaji wa mali;

(x) Uzembe wa Maafisa Wahasibu wa kutotunza nyaraka muhimu za mapato na matumizi na ufuatiliaji wa karibu kuhakikisha kama nyaraka zote zipo wakati wa ukaguzi;

(xi) Kufanya malipo nje ya nchi kupitia Balozi kwa ajili ya matibabu na malipo ya Wanafunzi wanaolipiwa na Serikali bila kurejesha nchini nyaraka zilizotumika kulipia malipo hayo;

(xii) Kukosekana kwa nyaraka na michanganuo ya gharama za malipo kwa miradi ya wafadhili pindi wanapokamilisha miradi yao na kuondoka nchini bila kuacha nyaraka na michanganuo husika; na

(xiii) Makusanyo ya maduhuli kufanywa bila kutumia stakabadhi za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** mambo yaliyobainika kutotekelezwa kwa ujumla Mafungu ya Wizara, Idara na Wakala mbalimbali yalionekana kupiga hatua nzuri katika kutekeleza mambo yasiyotekelezwa yaliyojitokeza katika kaguzi za miaka iliyopita. Hata hivyo, jumla ya Wizara, Idara, Wakala/Sekretarieti za Mikoa 26 zilikuwa na mambo yasiyotekelezwa ya mwaka uliopita ya jumla ya Sh.63,403,734,958. Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ikiongza kwani ilikuwa na Hesabu zenye kasoro kiasi cha Sh.13,904,086,980. Dola za Kimarekani 161,841 na *EURO* 17,548 ikifuatiwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi iliyokuwa na Sh. 11,490,278,359 na Idara ya Magereza iliyokuwa na jumla ya Sh.9,591,629,696.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya maoni ya Ukaguzi na mapendekezo yake katika kuainisha maeneo yenye matatizo katika Wizara, Idara na Mikoa ni kuyatafutia ufumbuzi. Hata hivyo, mapendekezo hayo hayakutekelezwa ipasavyo na hivyo kujirudia kwa Kasoro zilizoainishwa na wakaguzi katika miaka inayofuata. Kamati inaamini kuwa hatua madhubuti zitachukuliwa ili kuondoa udhaifu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi mbaya wa Fedha katika Wizara, Idara na Mikoa kumi na sita (16) iliyokaguliwa pamoja na masuala mengi ambayo hayakutekelezwa katika taarifa zao za usuluhisho *(Reconciliation)* wa Mahesabu na hivyo kusababisha ukiukaji wa Sheria na Kanuni za Fedha kama ilivyoelelezwa kwa muhtasari hapa chini:-

(i) Jumla ya Sh.48,987,689,503 ambazo ni mapato yaliyoingizwa katika Daftari la fedha la Wizara na Idara lakini hazikuingizwa katika taarifa za Benki.

(ii) Jumla ya Sh.49,083,765,395 ambazo ni hundi zilizochukuliwa fedha kwa ajili ya walipwaji mbalimbali hazikuwasilishwa Benki mpaka kufungwa kwa Mwaka wa Fedha tarehe 30 Juni, 2006.

(iii) Kiasi cha Sh.2,435,821,717 zilihesabiwa kama fedha inayongojea. Hakuna juhudi zilizofanywa katika mwaka wote wa fedha 2005/2006 kuhakikisha kuwa fedha zinaingizwa Benki.

(iv) Jumla ya Sh.4,118,786 ziliingizwa katika Akaunti za Benki bila ya kutolewa katika daftari la fedha.

(v) Jumla ya Sh. 123,043,632 ziliingizwa katika Daftari la fedha bila kutolewa taarifa za Benki.

(vi) Jumla ya Sh.2,333,076,949 zililipwa na Benki kwa niaba ya Wizara na Idara bila kuingizwa katika daftari la fedha la Wizara na Idara husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** hali hii inaonyesha kuwepo udhaifu mkubwa ndani ya Serikali na hivyo kutoa mwanya wa fedha za umma kutumika isivyokusudiwa. Hadi kufikia Juni 30, 2006 jumla ya masururfu ya Sh. 1,903,058,747 yalikuwa bado hayajarejeshwa kinyume na sheria na Kanuni za Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** katika kiambatisho hicho Wizara na Idara na Mikoa iliyoongoza kwa kutorejesha masurufu ni Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa kimataifa Sh. 641,237,768/=, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii Sh.510, 323,836/=, Katibu Tawala, Mkoa wa Ruvuma Sh.196,188,989/=, Katibu Tawala, Mkoa wa Manyara Sh.159,749,288/= na Idara ya Mahakama sh.92,570,241/=. Jumla ya maduhuli ambayo hayakukusanywa mpaka tarehe 30 Juni, 2006 yalikuwa Sh.13,089,608,638. Hata hivyo, kwa mujibu wa Taarifa za Ukaguzi kiasi cha Sh.235,937,160/= hakikujumuishwa katika maduhuli yaliyoonyeshwa hapo juu. Hivyo jumla ya maduhuli yasiyokusanywa mpaka tarehe 30 Juni, 2006 ni sh.13,325,545,797.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kiambatisho hicho Wizara, Idara na Mikoa iliyoongoza kwa kulimbikiza maduhuli ni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Sh.7,165,269,228/=, Wizara ya Nishati na Madini Sh.2, 184,070,572/=, Wizara ya Fedha Sh.1,764,785,841/=, Ofisi ya Waziri Mkuu Sh. 1,509,012,243/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** inaonekana kuwa kuna uangalizi mdogo kwenye tathmini ya makusanyo halisi ya maduhuli ya Serikali kitu ambacho kinachangia nakisi katika bajeti ya mwaka ya Serikali. Hatua za makusudi zinahitajiwa na Maofisa Masuhuli wahusika kurekebisha hali hii. Vivyo hivyo, Hazina inahitaji kuwakumbusha wapokeaji wa maduhuli husika kuhusu jukumu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upotevu wa fedha taslimu na vifaa katika Mwaka 2005/2006 kulikuwa na upotevu wa fedha taslimu na vifaa kiasi cha Sh.1,512,568,122.65 na Sh.740,965,824.88 kwa mfuatano huo uligundulika na kutolewa taarifa katika Wizara, Idara na Mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** katika kiambatisho hicho Wizara, Idara na Mikoa iliyoongoza katika upotevu wafedha taslimu na vifaa ni Wizara ya Kilimo na Chakula Sh.593,066,192/=, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii Sh.419,480,228/=, Idara ya

Mahakama Sh.268,170,814/=, Wizara ya Usalama wa Raia Sh. 200,591,503/= na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Sh.155,575,000/=

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** upotevu huu ni mkubwa na unachangia kuongeza umaskini katika nchi yetu. Kamati inashauri kwamba uchunguzi ufanywe ili kujua kiasi halisi cha upotevu na kuchukua hatua zinazofaa dhidi ya upotevu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** malipo yenye shaka Mwaka wa Fedha wa 2005/2006, Wizara kumi na mbili (12), na Mikoa Kumi (10) zilifanya malipo ya Sh.67,842,326,800. Hata hivyo, malipo hayo yalikosa taarifa muhimu na za kutosheleza kuelezea uhalali wa malipo hayo na hivyo gharama sahihi za matumizi hayo hazikujulikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** katika kiambatisho hicho Wizara, Idara na Mikoa iliyoongoza katika malipo yenye shaka ni Wizara ya Nishati na Madini sh.46,627,234,518/=, Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia Sh. 10,462,651,725/=, Idara ya Mahakama Sh.3,115,879,222/=, Wizara ya Fedha Sh.2,951,260,775/= na Ofisi ya Waziri Mkuu Sh.2,203,326,774/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utunzaji mbaya wa Hesabu za Maduhuli, Wizara na Idara za Serikali zimekuwa hazizingatii Sheria na Kanuni za fedha katika utunzaji wa maduhuli kama inavyoonyesha katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya sh.80,054,93.50 kutoka Idara ya Mahakama zilikusanywa katika vituo tofauti kati ya mwezi Juni, 2003 na Juni, 2006 lakini hazikuingia Benki wala kutolewa maelezo namna zilivyotumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosekana kwa taarifa ya marejesho ya maduhuli katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ukaguzi kiasi cha Sh.761,947,180 cha maduhuli yaliyokusanywa na shule mbalimbali kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005 hakikuweza kuthibitishwa kutokana na kukosekana kwa taarifa ya marejesho kutoka kwenye shule husika.

Kutoingiza kwenye daftari la wakusanya maduhuli jumla ya makusanyo ya Sh.50,204,276 katika Idara ya Mahakama hayakuingizwa katika kumbukumbu za daftari la Wakusanyaji wala kuthibishwa na mpokeaji wa maduhuli hayo.

Kutokuwasilisha Maduhuli Ubalozi wa Berlin ambao uliuza jengo lake kwa Sh.1,053,380,000 (*Euro* 620,0000). Hata hivyo, mapato ya mauzo hayo hayakuwasilishwa Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokulipa ada ya Uchambuzi wa madini Ofisi ya *TANSORT* iliyoko *London* ilikusanya ada ya uchambuzi wa madini iliyofikia dola za Kimarekani 2,128,733.5. Hata hivyo, haikuthibitishwa kwamba kiasi hicho kililipwa Makao Makuu ya Wizara. Kitendo hiki kinaweza kusababisha uwezekano wa ufujaji au kuchepua wa fedha za umma kwa malengo ambayo hayakudhamiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya Sh.221,695,795 zilichepuliwa kutoka kiasi cha Sh.1,121,695,793 katika Wizara ya Nishati na Madini bila ya maelezo yoyote**.** Fedha hizi zilipaswa kulipwa kwenye Ofisi za *TANSORT London* .

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokuthibitisha thamani ya madini yayozalishwa, Wizara haina usimamizi wa karibu na utaratibu wa udhibiti katika machimbo ya madini kujua kiasi halisi cha Almasi iliyozalishwa. Almasi iliyosafirishwa kati ya Januari, 2004 na Oktoba, 2005 ya uzito wa jumla ya karati 473,051.9 yenye thamani ya Dola za Kimarekani 56,934,749.09 (Sawa na Sh.71,343,795,390) haikuweza kuthibitishwa dhidi ya uzalishaji halisi na almasi iliyosafirishwa nje ya nchi. Ni wazi kwamba maduhuli yaliyopatikana kutokana na malipo ya Almasi na Madini mengine kwa Serikali hayakuwa halisi kutokana na ukosefu wa takwimu za kuaminika kutoka kwenye migodi husika kutokana na usimamizi hafifu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutumia fedha baada ya mwaka wa fedha kupita (*deferred payments)* jumla ya malipo yanayofikia Sh 1,815,129,791 yalilipwa Mwaka wa Fedha 2004/2005 baada ya mwaka fedha husika kupita na kulipwa katika mwaka unaokaguliwa kuepuka matumizi zaidi. Utaratibu huu ni kinyume na Sheria na Kanuni za Fedha. Wizara zilizokuwa na Matumizi ya aina hii ni Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Sh.1,712,910,851/= na Wizara ya Usalama wa Raia Sh.102,218,940/=. Matumizi yasiyo na Hati za malipo ni yale yasiyokuwa na ushahidi wa maandishi kuthibitisha uhalali wa matumizi yake. Jumla ya Sh.1,299,696,563 zilitumiwa na Wizara, Idara na Mikoa bila kuwa na kumbukumbu.

Matumizi yasiyo na hati za malipo katika Wizara, Idara na Mikoa kwa mwaka 2004/2005, Wizara, Idara na Mikoa iliyoongoza kwa kuwa na matumizi bila ya kuwa na Hati za Malipo ni Wizara Afya na Ustawi wa Jamii Sh.771,322,380/=, Katibu Tawala wa Mkoa wa Manyara Sh.120,025,244/=, Wizara ya Nishati na Madini Sh.118, 886,125/=, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo Sh.66,790,486/= na Katibu Tawala waMkoa wa Mwanza Sh. 66,242,286/=. Kuwa na matumizi yasiyo na hati sahihi za malipo mwaka 2005/2006 jumla ya Sh.36,665,182,261 zililipwa bila kuwa na hati sahihi za malipo *(voucher)* kinyume na taratibu za fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Wizara na Idara zilizoongoza kuwa na matumizi yasiyo na hati sahihi za malipo ni Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia Sh.16,992,299,049/= ,Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Sh. 7,440,382,230/=, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Sh. 7, 058,429,875/=, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo, Sh. 1,209,947113/= na Idara ya Mahakama Sh.754,738,209/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutorejesha Hazina mishahara ambayo haijalipwa sheria ya fedha inataka mishahara yoyote isiyolipwa irejeshwe kwa Mhasibu Mkuu na hatimaye kwa mlipaji mkuu wa Serikali *(Paymaster General).* Mishahara yenye jumla ya Sh. 33,457,169 ambayo haikudaiwa na wahusika haikurejeshwa kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara na Mikoa iliyoongoza kwa kutorejesha Hazina mishahara ambayo haijalipwa ni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

Sh.23,791,717/= Katibu Tawala waMkoa wa Mwanza Sh.6,673,710/= na Katibu Tawala waMkoa wa Kagera Sh.2, 991,742/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufanya malipo kwa Ankara kifani *(Profoma invoice)* jumla ya malipo ya sh.1,115,227,298 yalifanywa kwa ankara kifani kabla ya upokeaji wa bidhaa na huduma. Hiki ni kinyume cha sheria na hatua madhubuti zichukuliwe kudhibiti utaratibu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara, Idara na Mikoa iliyoongoza kwa kufanya malipo kwa Ankara kifani *(Profoma invoice)* ni Idara ya Magereza Sh.494,178,192/=, Wizara ya Nishati na Madini sh.149,872,835/=, Jeshi la Kujenga Taifa sh.105,056,244/= na Ofisi ya Waziri Mkuu sh.89,247,527/= .

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi yasiyo na manufaa (*nugatory expenditures)* ni matumizi ambayo hayana thamani kulingana na bidhaa na huduma zilizopokelewa kutokana na matumizi hayo. Jumla ya sh.218,713,667 za matumizi ya Wizara, Idara na Mikoa yalikuwa matumizi yasiyo na manufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara zilizoongoza kuwa na matumizi yasiyo na manufaa (*Nugatory Expenditures)* ni Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii Sh.150,259,400/=, Wizara ya Nishati na Madini Sh.45,900,267/= na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo, Sh.19,554,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufanya matumizi ya Ziada bila kibali, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ililipa Sh.204,126,542.90 kwa ajili ya Balozi za Nje kwa ajili ya malipo ya deni lililosalia bila kuwa na tengo la bajeti kwa mwaka unaokaguliwa. Aidha, ubalozi wa Tanzania ulioko Addis Ababa ulitumia kiasi cha Sh.40,904,546, zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa bila kibali maalumu. Utaratibu huu unakiuka sheria na Kanuni za Fedha na hivyo kufanya zoezi la kuwa na bajeti kuwa halina maana yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikopo kwa Mashirika ya Umma kutorejeshwa, jumla ya mikopo 19 iliyotolewa na Serikali ikiwa ni malimbikizo inayofikia Sh.63,241,256,898, wakati wa Ukaguzi, mikopo hiyo haikuwa imerejeshwa na mashirika husika yanayonufaika. Aidha, hakuna maelezo yoyote yaliyotolewa kwa madeni kuwa kwenye malimbikizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwa na ugawaji mbaya wa Fedha Sh.1,461,968,400, jumla ya Sh.1,724,210,400 zilitolewa na Hazina kwa ajili ya ununuzi wa magari ishirini ya kawaida na gari moja la Zimamoto kwa Jeshi la Kujenga Taifa. Hata hivyo, baadaye magari sita (6) tu yenye thamani ya Sh.262,242,000 ndiyo yaliyonunuliwa na kubakiza Salio la Sh.1,461,968,4 ambazo zilipangiwa shughuli nyingine bila idhini ya Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi huu mbaya kama ilivyoelezwa hapo juu ni lazima urekebishwe ili fedha za umma zitumike kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za fedha kwa maendeleo ya nchi na ustawi wa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hesabu zilizojadiliwa na Kamati kulikuwa na ukiukwaji mkubwa wa taratibu na mchakato wa ununuzi wa bidhaa na huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** kila afisa mhasibu ana wajibu wa kufuata sheria ya ununuzi anaponunua vifaa au huduma. Aidha, imebinika kuwa Wizara, Idara na Mikoa mingi katika nyanja za ununuzi zina upungufu katika maeneo yafuatayo:- (i) Ukosefu wa mipango kwa ajili ya miradi ya ununuzi; (ii) Bodi za zabuni zisizofanya kazi kwa ufanisi; (iii) Uhifadhi wa kumbukumbu za ununuzi usiotosheleza; (iv) Vitengo vya kusimamia ununuzi kutofanya kazi kwa ufanisi au kutokuwepo kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu kuhakikisha kwamba nyaraka zote zinazohusiana na miradi zinahifadhiwa katika jalada moja kwa ajili ya urahisi wa rejea na usimamizi wa miradi. Utaratibu huu unawezesha upatikanaji wa habari kutoka Wizara na Idara na watu wote wanaotaka kujua kuhusu kandarasi husika. Hata hivyo, nyaraka za miradi zenye thamani ya Sh. 5,693,953,413/= hazikuweza kuonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara na Idara zilizoongoza katika Uhifadhi wa Nyaraka za kandarasi usiofaa ni Wizara ya Usalama wa Raia Sh.2,711,241,279/=, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa (Makao Makuu) Sh. 312,260,173/=, Ubalozi wa Tanzania nchini Uingereza Sh.128,512,000/=, Ubalozi wa Tanzania nchini Zambia Sh. 56,618,914/= na Idara ya Magereza Sh.40,000,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokutolewa bidhaa na huduma zilizolipiwa, aidha, bidhaa na huduma zenye thamani ya jumla ya Sh. 48,489,737,331 hazikujulikana kama zimetolewa au kufanyika pamoja na ukweli kwamba zilikuwa zimelipiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara na Mikoa iliyoongoza kulipia huduma na bidhaa ambazo hazikutolewa ni Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii Sh. 36,422,791,347/=, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Sh. 691,253,534/= (matengenezo), Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Sh.10,816,332,450/=(Kununua magari), Wizara ya Nishati na Madini Sh. 18,563,200/= na Wizara ya Kilimo na Chakula Sh.9,800,000/=. Wizara na Idara zilifanya malipo kwa ajili ya ujenzi, ununuzi wa bidhaa na huduma yenye thamani ya Sh.2,004,069,693 bila kuwa na Zabuni za Ushindani**.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara na Idara zilizoongoza kwa ununuzi wa bila Kuzingatia Zabuni za ushindani ni Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Sh. 783,310,331/=, Wizara ya Usalama wa Raia Sh.235, 603,293/= ,Wizara ya Mambo ya Ndani Sh. 221,684,400/=, Idara ya Uhamiaji Sh.217,373,040/= na Wizara ya Maliasili na Utalii Sh.47,386,170/=. Aidha, ununuzi wa bidhaa au huduma zenye thamani ya sh. 1,315,123,051 ulifanywa bila idhini ya Bodi za Zabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara na Idara zilizoongoza kufanya ununuzi bila idhini ya Bodi ya Zabuni ni Wizara ya Usalama wa Raia Sh. 708,034,156/=, Ofisi ya

Waziri Mkuu Sh.305,463,564/=, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo Sh.182,664,060/=, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Sh. 60,980,646/= na Tume ya Uchaguzi Sh.24,699,560/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutofuatwa kwa Sheria na Kanuni ya Ununuzi kunaweza kusababisha matumizi mabaya ya fedha za Serikali. Ni vema hatua zikachukuliwa ili kudhibiti mapema udhaifu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoingiza vifaa kwenye leja taratibu zinazoongoza upokeaji wa vifaa kutoka kwa wagavi kwenda kwenye Bohari yolote ya Serikali lazima kulenge kuhakikisha kwamba malipo yanayofanywa tu kwa kiasi halisi kilichopokelewa katika hali nzuri na kukidhi ainisho lililohitajika na kuingizwa kwenye leja. Mwaka 2005/2006 bidhaa zenye thamani ya Sh.4,635,051,714 hazikuingizwa kwenye leja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara na Idara zilizoongoza kwa kutoingiza vifaa kwenye leja ni Wizara Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Sh. 901,137,055/=, Wizara ya Maji Sh.430,225,353/=, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Sh.165,864,199/= na Katibu Tawala wa Mkoa wa Tanga Sh.111,850,946/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusimamia vibaya vifaa na bidhaa, maeneo ya ununuzi wa mafuta, sare, viandikia *(stationery)* na bidhaa nyingine zitumiwazo ambavyo kwa kawaida vimetafutwa kienyeji kwa kutumia masurufu maalumu ni njia rahisi ya kufuja fedha za umma. Ni muhimu kuwa mfumo wa udhibiti wa ndani kuhusu vifaa lazima uimarishwe kwa kufuata Sheria na Kanuni za Ununuzi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo haya yameorodheshwa katika karatasi yangu hapa, ripoti yetu na tunaomba kwamba hii ripoti ichukuliwe kama ilivyo, iweze kuwekwa katika *Hansard.* Kuwa na matumizi yasiyokuwa na hati na yenyewe ni shilingi bilioni 36, fedha nyingi. Kutorejesha Hazina mishahara shilingi milioni 33.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia haya matatizo ambayo tumeorodhesha hapa ni dhahiri kabisa kuna udhaifu katika Serikali katika kuangalia vitabu vyake. Lakini hapa ningependa kutoa angalizo kwamba vitabu hivi ndivyo vilivyoonekana kwenye ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, baada ya kukaa na *PAC* mambo yamekuwa ni tofauti kidogo kuwa kwamba nyaraka zimepatikana. Lakini kazio hapa watu wasingoje hoja, watu wazuie hoja. Ndiyo kitu ambacho Kamati hii inajaribu kusisitiza kuliko vitu vyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuchambua udhaifu uliopo katika kudhibiti matumizi ya Serikali, Kamati inatoa maoni na mapendekezo kama ifuatavyo:-

Sheria itakayotawala ofisi na shughuli za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iletwe Bungeni na Wizara ya Fedha kabla ya Mkutano wa bajeti wa 2007/2008 ijadiliwe na kupitishwa na Bunge.

Ili kuboresha utendaji na kurudisha nidhamu ya matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia Sheria za Fedha na Sheria za Ununuzi kama miongozo ya kufanyia kazi, Wizara na Idara za Serikali zinazopata Hati Chafu, Maafisa Wahasibu husika wachukuliwe hatua zaidi ya kupewa Tozo ikiwemo kushushwa cheo kwa vile adhabu ya Tozo haiwezi kufidia fedha zilizopotea. Serikali ifanye juhudi kupunguza matumizi ya kawaida *(Recurrent Expenditure)* katika bajeti ya nchi badala yake iongeze bajeti ya maendeleo ili kuimarisha utekelezaji wa miradi na kupunguza utegemezi kutoka kwa wafadhili.

Kamati inapongeza kazi nzuri inayofanywa na Mamlaka ya Mapato ya Tanzania kukusanya mapato mengi, hata hivyo, bado kuna fursa ya kuboresha ukusanyaji wa mapato kwa kupanua uwigo wa kodi . Vyanzo ambavyo bado kuangaliwa vizuri ni sekta za Madini,Misitu, Utalii na Uvuvi. Mamlaka ya Mapato Tanzania ibuni mkakati maalumu wa kukusanya mapato katika sekta hizi.

Wizara na Idara za Serikali zitekeleze Kanuni Na.8 (5) kwa kuweka wazi mikakati ya bajeti, mipango yao, mapato na matumizi, na kadhalika. Kanuni hii ni muhimu katika kuimarisha uwazi, uwajibikaji na utawala bora. Wizara na Idara za Serikali zitekeleze Sheria za Manunuzi ngazi zote katika mchakato wa manunuzi, ziimarishwe kitaaluma *(Capacity Building).* Aidha, Mamlaka ya Kusimamia Ununuzi wa Umma *(Public Procurement Authority –PPRA)* yaimarishwe ili iweze kusimamia ununuzi nchi nzima.

Nyaraka mbalimbali zinahusu malipo kwa wastaafu ziandaliwe mapema ili kupunguza makosa katika mahesabu, kwa kukosekana nyaraka.

Maasifa Uhasibu wajijengee uwezo wa kuzuia hoja kuliko kutegemea kujibu hoja kabla ya vikao vya *PAC.* Aidha, wajibu hoja zote za ukaguzi kwa umakini unaostahili ili katika taarifa zijazo mafungu yote wanayoyasimamia yaweze kupata hati safi ya ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuwe na utaratibu madhubuti wa kutunza vifaa na mali wanazozisimamia. Aidha, kuwepo na udhibiti wa ndani kwa kuboresha vitengo vya ukaguzi wa ndani, kwa kuwa na Wafanyakazi waliofuzu wenye vitendea kazi vya kisasa kama vile Kompyuta. Vilevile Wizara na Idara za Serikali zipange safu za Watendaji katika sehemu na vitengo mbalimbali kulingana na sifa na uzoefu. Aidha, pale penye upungufu jitihada za makusudi zichukuliwe za kuwasiliana na mamlaka zinazohusika ili kupata watumishi wanaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini udhaifu wa utendaji kwa baadhi ya Maafisa Wahasibu unaotokana na ufinyu wa Bajeti inayotengwa kwenye mafungu wanayosimamia. Aidha, mafungu ambayo yamekumbwa na tatizo hili mengi yao ni yale yanayotoa huduma za kijamii kama vile Afya, Mahakama, Elimu Kazi na Ajira na kadhalika. Kamati inashauri Serikali ijitahidi kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya mafungu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipokuwa ikijadili Taarifa ya Utendaji na Hesabu za Mafungu ya Mikoa, bado imebainika kuwepo kwa *"Double Accounting System"* katika utoaji wa fedha za maendeleo pale zinapopelekwa moja kwa moja kwenye Halmashauri mbalimbali hapa nchini na baada ya kutumika fedha hizo nyaraka zote za kihasibu hupelekwa kwa Afisa Mhasibu wa Mkoa anayewajibika kuzitolea maelezo *(Account for)* kwa Kamati ya Hesabu za Serikali *(PAC)* na Afisa Mhasibu wa Halmashauri *(DED)* kuwajibika kuzitolea maelezo kwa Hesabu hizo hizo kwenye Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC).*

Hali hii imesababishia Maafisa Wahasibu wa Mikoa kutokuwa na maelezo na nyaraka za matumizi ya fedha hizo, hivyo kubaki hoja za ukaguzi vitabuni na hatimaye kupata hati zenye dosari za ukaguzi. Kamati inashauri itafutwe namna ya kurekebisha dosari hii. Serikali ianzishe utaratibu wa kujibu mapendekezo ya Kamati ya *PAC* katika mfumo wa ”*treasury notes*” .

Serikali ilete kabla ya Bajeti ya 2008/2009 muswaada Bungeni wa kumwezesha Spika kutumia mfuko wa Bunge (*National Assembly Fund)* na vyanzo vingine vya mapato kujenga uwezo wa Bunge na Kamati zake hususan *PAC, POC* na *LAAC* kuisimamia Serikali kwa mujibu wa katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha, napenda kutumia fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali kuhusu utekelezaji wa shughuli zake kwa mwaka 2006 na 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine naomba kukupongeza wewe binafsi, Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Mheshimiwa Anne Makinda, (Mb.), Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Jenista Mhagama, (Mb.) ambaye leo upo hapa. Mheshimiwa Job Y. Ndugai, (Mb.) na Mhesimiwa Zuber Maulid, (Mb.), kwa uongozi wenu mahiri katika kuliongoza Bunge letu Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge Hesabu za Serikali waliopo sasa na waliofanya kazi ninayoiwasilisha leo kwa kutekeleza majukumu mbalimbali yaliyoihusu Kamati hii kwa moyo na uadilifu mkubwa. Aidha, nawapongeza kwa kushiriki kikamilifu katika maandalizi ya Taarifa hii na kunipa heshima ya kuiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, napenda kumshukuru aliyekuwa Katibu wa Bunge, Ndugu Damian S.L. Foka, Kaimu Katibu wa Bunge, Dk. Thomas D. Kashililah, kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Aidha, nawapongeza Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Angumbwike Lameck Ng'wavi na Ndugu Ernest Zulu kwa kuratibu shughuli zote za Kamati hii kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na kuijadili na hatimaye lipitishe mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali kwa taarifa yako na hoja ambayo umeiweka hapa mbele. Kabla sijamwita Mheshimiwa Dakta Wilbrod P. Slaa, ili na yeye aje kutoa taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, kwa faida ya Waheshimiwa Wabunge ambao wako nje ya ukumbi wa Bunge kwa sasa, matokeo ya uchaguzi yako tayari na nimeshakabidhiwa hapa Mezani. Lakini nitayatangaza kabla ya kusitisha shughuli za Bunge leo mchana. Kwa hiyo, kwa Waheshimiwa wote ambao wako nje ya ukumbi wa Bunge, wale ambao wangependa kuja kuyasikiliza matokeo hayo ndani ya ukumbi wa Bunge, naomba tu nitangaze kwamba nitayatangaza kabla sijasitisha shughuli za Bunge leo mchana. Baada ya kusema tangazo hilo, basi naomba sasa nimwite Mheshimiwa Dakta Slaa, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, ili na yeye aje kusoma taarifa yake ya Kamati na kuiweka Mezani hoja yake. Karibu sana Mheshimiwa Slaa! *(Makofi).*

**MHE. DR. WILBROAD P. SLAA – MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa juu ya taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iliyowasilishwa katika Bunge lako Tukufu mwezi Machi, 2007, kuhusu hesabu za Majiji, Manispaa, Mamlaka za Miji, na Halmashauri za Wilaya zilizokaguliwa kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006.

Kabla sijaanza kutekeleza Kanuni ya 114, Kanuni ndogo ya 15 ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, niruhusu kwa niaba ya Kamati yangu kutumia nafasi hii kuelezea huzuni na masikitiko yetu makubwa kutokana na msiba uliowakumba wananchi wa Kiteto na Taifa kwa ujumla kufuatia kifo cha Mheshimiwa Benedict Kiroya Lusurutia. Marehemu Losurutia alikuwa Mbunge wa Jimbo la Kiteto, lakini pia Mjumbe wa Kamati yetu ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Marehemu alifariki tarehe 16/12/2007. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Kamati hii yameainishwa kwenye Nyongeza ya sita, fasili ya 12 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2007 na kwa mwaka wa taarifa hii Kamati ilifanya kazi zake katika namna kuu mbili, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya kwanza ilihusisha kujadili hesabu zilizokaguliwa za Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji. Kazi hiyo imefanywa kwa Halmashauri zote 124 zilizokuwapo mwaka 2005/2006 katika vikao vilivyofanyika Dar-es-Salaam na Dodoma. Awamu ya pili ilihusisha Kamati kwenda kwenye baadhi ya Halmashauri, kukagua miradi iliyotekelezwa kwa kutumia fedha za

umma. Halmashauri zilizokaguliwa kwa njia hii ni pamoja na Halmashauri za mji wa Babati na Kondoa, Halmashauri za Wilaya za Babati, Mkuranga na Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila Halmashauri iliyofika mbele ya Kamati ilitakiwa kuwasilisha mambo yafuatayo: Taarifa ya Wilaya yenye maelezo ya shughuli zote zilizomo katika Halmashauri ya Wilaya husika, Taarifa ya mapato na matumizi ya kawaida, Taarifa ya mapato na matumizi ya miradi yote inayotumia ruzuku ya Serikali, Wahisani, Halmashauri na Wananchi.

Taarifa ya uchambuzi wa matumizi ya miradi yote iliyotekelezwa na Halmashauri ikionesha matumizi ya fedha kuanzia na matumizi ya fedha kuishia mwaka unaohusika na ukaguzi yaliyohakikiwa na ukaguzi, majibu ya hoja za ukaguzi yaliyohakikiwa na ukaguzi, majibu ya hoja na maagizo ya Kamati ya *LAAC* yaliyotolewa kwa kila Halmashauri wakati wa vikao vya nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeendelea kuwashirikisha Wastahiki Mameya na Wenyeviti wa Halamashauri kwa lengo la kuwaelimisha juu ya shughuli za *LAAC*, kuwapa nafasi ya kusikia majibu ya watendaji juu ya nidhamu yao katika matumizi ya fedha na mali za umma ili wakirudi kwenye Halmashauri zao wawaeleze madiwani juu ya hali halisi ya mahesabu ya Halmashauri zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mambo ya jumla, katika mahojiano na Halmashauri mbalimbali Kamati ilibaini changamoto ambazo Serikali inatakiwa kuzipokea na kuzifanyia kazi kwa manufaa ya Watanzania. Changamoto hizo tumezitaja kuanzia ukurasa wa nne hadi ukurasa wa nane wa taarifa yetu ambayo ni taarifa kubwa. Hapa ninasoma *summary* yake tu. Kubwa kati ya yote ni Halmashauri kunyimwa ruzuku ya maendeleo kwa sababu ya kuwa na hati chafu ya ukaguzi.

Katika hili Kamati ya *LAAC* inapingana na dhana ya Serikali kuiadhibu Halmashauri nzima yaani wananchi kwa kosa lililofanywa na watendaji. Vigezo vyote vinavyoangaliwa katika kutoa ruzuku ya maendeleo viko mikononi mwa watendaji na si wananchi. Lakini ruzuku inayonyimwa wanaoumia mara nyingi ni wananchi na si watendaji kwani mishahara yao iko palepale. Kamati inaitaka Serikali iangalie upya kigezo hiki katika kutoa fedha za maendeleo, yaani *Local Government Capital Development Grant,* kwa sababu anayeziletea Halmashauri hati chafu ni Menejimenti ya Halmashauri. Inapothibitika hivyo basi Menejimenti hiyo ndiyo inapaswa kuwajibika kwa utendaji wake badala ya kuwaadhibu wananchi wasio na hatia wa Wilaya nzima. *(Makofi).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ni pale ambapo Halmashauri zimebinafsisha ukusanyaji wa mapato. Kamati imegundua kuwa katika baadhi ya Halmashauri, mawakala si waaminifu, wanachapisha vitabu vya makusanyo wenyewe badala ya utaratibu wa kawaida wa halmashauri kuchapisha vitabu hivyo ili kurahisisha udhibiti, mawakala kutowasilisha kikamilifu makusanyo kwa mujibu wa mikataba na kadhalika. Taarifa ya *CAG* inaonesha kuwa mwaka 2005/2006 jumla ya shilingi 217,502,861 hazikuwasilishwa na mawakala katika Halmashauri 14. Halmashauri hizo ni

za Wilaya za Mkuranga, Bariadi, Shinyanga, Sengerema, Magu, Nzega, Ukerewe, Kilolo, Ludewa na Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yetu pia imebaini kuwa manunuzi yanayofanywa na baadhi ya Halmashauri hayafuati taratibu zilizopo. Hii inatokana kwa sehemu kubwa na kutokuwa na ufahamu wa kutosha juu ya Sheria ya Manunuzi ya Mwaka 2004 kwa upande wa watumishi wa Halmashauri au Bodi za zabuni na hata Madiwani. Taarifa ya *CAG* ya mwaka 2005/2006 ilionesha kwamba Halmashauri tisa zililipa jumla ya shilingi 126,173,650 kwa ajili ya vifaa. Lakini vifaa vilivyolipiwa, aidha havikuwasilishwa vyote au havikuwasilishwa kabisa.

Halmashauri hizi ni za wilaya ya Mufindi, Kasulu, Geita, Tarime, Mbinga, Urambo, Tabora, Handeni na Halmashauri ya Mji wa Lindi. Halmashauri saba zililipa jumla ya shilingi 797,470,844 kwa ajili ya kununua vitu mbalimbali bila kufuata utaratibu wa ushindani. Halmashauri husika ni za wilaya za Iringa, Kigoma, Misungwi, Kibaha, Mkuranga, Mji wa Babati na Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro. Halmashauri tano zililipa jumla ya shilingi 380,222,234 kwa ajili ya manunuzi bila idhini ya Bodi ya Zabuni.

Nazo ni Halmashauri za Wilaya ya Nkasi, Bagamoyo, Kisarawe, Mafia na Wilaya ya Rufiji. Halmashauri 46 zililipa jumla ya shilingi 683,687,105 kwa ajili ya manunuzi mbalimbali. Vifaa vilivyonunuliwa havikuingizwa katika daftari na hivyo matumizi yake kutokuwa wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado pana changamoto katika Halmashauri kuhusiana na masuala ya kuandaa bajeti zilizo sahihi na zinazotekelezeka. Mfano katika taarifa ya *CAG* ya mwaka 2005/2006 Halmashauri tano zilishindwa kutumia ruzuku iliyotolewa na Serikali Kuu ya shilingi 2,665,196,801 na hakuna sababu kubwa ya msingi iliyothibitika kutotumia fedha hizo mbali na kusema zilichelewa kupokelewa, wakati huo huo wananchi wanateseka kwa kukosa maendeleo. Halmashauri kutokuwa na sera madhubuti za kudhibiti fedha zilizo katika Halmashauri yenyewe, yaani *Cash Management Policy,* na hivyo kuwa na changamoto ya kutafuta namna bora ya kulinda fedha hizo zisipotee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli za Kamati hii kama nilivyokwishasema hapo awali hufanyika katika namna kuu mbili. Namna ya pili ni ile ya Kamati kufanya ziara za ukaguzi wa ufanisi (*performance audit)* kwa lengo la kuchochea maendeleo ya Taifa na nidhamu ya matumizi ya fedha na mali ya umma kwa ujumla. Ukaguzi huo huiwezesha Kamati kufanya mahojiano na Maafisa Masuhuli (*Accounting Officers)* wakiwa katika eneo ambapo mradi unaojadiliwa upo. Hii ni tofauti na njia ya kwanza ambapo ni taarifa tu zinazoletwa mbele ya Kamati. Mara nyingine baadhi ya miradi huandikwa kwenye taarifa wakati kwenye maeneo ya utekelezaji haipo kabisa, ama ipo lakini sio kwa ubora, ukubwa, kiwango na hata idadi ambayo ilioneshwa kwenye taarifa. Katika ziara hizi Kamati hulenga kujiridhisha na maendeleo ya miradi mbalimbali ambayo Serikali Kuu, nguvu za wananchi, Halmashauri na Wahisani mbalimbali wamechangia. Miradi hiyo ni katika meneo kama yafutayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo mojawapo ni Miundombinu. Barabara zilizoko chini ya Halmashauri, mfano barabara zinazotengenezwa kwa fedha za mfuko wa barabara (*Road Fund)* na ruzuku mbalimbali kama *Capital Development Grant, (CDG)*. Katika elimu tunakagua vyumba vya madarasa na nyumba za walimu katika shule za msingi na sekondari, kupitia fedha za *MMEM, MES, TASAF,* nguvu za wananchi na Halmshauri zenyewe. Afya, ujenzi na ukarabati wa zahanati, vituo vya afya na hospitali kwa fedha kutoka mfuko wa afya, yaani *Basket Fund*, *TASAF*, *CDG* na mifuko mingine. Kilimo, miradi yote pamoja na ya umwagiliaji ambayo imegharimiwa kupitia Halmashauri za Wilaya kwa fedha za Wahisani, Halmashauri au Serikali Kuu kupitia *CDG*. Maji, miradi ambayo imetekelezwa kwa kutumia fedha za Halmashauri, Serikali Kuu, Wahisani na wananchi.

Miradi mingine yoyote ambayo kwa namna moja au nyingine imetekelezwa na Halmashauri kwa fedha za Wahisani mbalimbali, katika kutekeleza wajibu huu, Kamati ilipata fursa ya kukagua miradi ya maendeleo katika Halmashauri za Wilaya za Bagamoyo, Mkuranga, Kondoa, Babati na Halmashauri ya Mji wa Babati. Katika kila Halmshauri tuliyotembelea tulitoa maelekezo na ushauri kama ambavyo tumezionesha kuanzia ukurasa wa nane hadi 26 wa taarifa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa mifano michache kama ifuatavyo. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo shule ya Sekondari ya Chalinze, Kamati iligundua kutokuwepo utaratibu maalumu Kiwilaya na Kitaifa, wa kuwaendeleza watumishi, idadi kubwa ya waalimu walijiondokea kila walipojipatia, kwa njia zao wenyewe nafasi ya elimu ya juu. Jambo hili linahatarisha ubora wa shule na kufanya shule isiwe na mipango ya muda wa kati wala ya muda mrefu. Katika Kituo cha Afya Lugoba, Kamati haikuridhika na nidhamu ya matumizi ya fedha shilingi 15,699,300 zilizotumika kwa ukarabati wa chumba kimoja cha upasuaji. Kamati ilielekeza Sekretarieti ya Mkoa wa Pwani na Mkaguzi Mkazi wa Mkoa kuchunguza matumizi ya fedha hizo na Kamati ijulishwe kuhusu hatua zitakazochukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri ya Mkuranga Kamati iligundua katika Mradi wa Maji wa Mipeko, pampu mbili za maji zilizogharimu zaidi ya shilingi milioni 7, zimetelekezwa. Aidha, mifuko 400 ya saruji iliyotolewa na mfuko wa *EOTF*, wa mama Anna Mkapa, iliachwa na kutelekezwa mpaka ikaharibika. Kamati inaelekeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, nashukuru yuko hapa, afuatilie na kuliarifu Bunge sababu zilizofanya mali nyingi kiasi hiki kutelekezwa na watakaobainika kuhusika na uharibifu huu wachukuliwe hatua hasa kwa vile uharibifu huo wa saruji umekwamisha ukamilishaji wa wodi ya watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika wilaya ya Kondoa Kamati ilipata nafasi ya kutembelea, pamoja na mengine, shule ya ya msingi ya Churuku, ambapo Kamati ilikuta mahusiano kati ya walimu na wanakijiji kuwa tete kiasi cha wanakijiji kuwatimua walimu kwa mishale. Hii si tu ni hali ya uvunjaji wa amani, bali iliathiri sana maendeleo ya taaluma. Mathalani kati ya wanafunzi 168 waliofanya mtihani wa darasa la saba ni wanafunzi wawili tu walifaulu na kupata nafasi ya kujiunga na shule ya sekondari. Kamati ilitoa maelekezo kwa *DC* na *DED* kuhakikisha malumbano hayo yamefikia

mwisho haraka iwezekanavyo na isitoshe wanakijiji walitahadharishwa kuwa maendeleo ya shule hiyo na ya watoto wao yako mikononi mwao na walimu wao, hivyo hawana budi kushirikiana na kushikamana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilikuta tatizo zito katika Wilaya ya Kondoa na Mamlaka ya Mji wa Kondoa ambapo kulikuwa na mgogoro kati ya *TAKUKURU* na watendaji wengine wa Serikali. Kamati iligundua kuwa migogoro ya aina hiyo hukwamisha miradi ya maendeleo na shughuli za kawaida za jamii. Hata hivyo, *DC* aliahidi kuchukua hatua zinazostahili katika jambo hili. Kamati ilisisitiza kila chombo kifahamu na kuheshimu mipaka yake kwa mujibu wa sheria za nchi. Mgogoro huo unaweza kuuona kwenye taarifa yetu kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Manispaa ya Babati, Kamati ilipata nafasi ya ukaguzi wa ufanisi (*performance audit)* ambapo *CAG* alikuwa ametoa taarifa yake ya kwanza ya aina hii kwa nchi nzima kuhusiana na maafa ya mafuriko ya ziwa Babati, Wilayani Babati. Kamati inaitaka Wizara ya Miundombinu na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kuyaangalia kwa makini mapendekezo ya *CAG* na kuyafanyia kazi kwa haraka inavyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilisikitishwa na hali iliyoikuta katika Kituo cha Afya cha Magugu ambapo ilikuta huduma zimedorora kiasi cha kutosha. Watumishi walio wengi sio waajiriwa, hawalipwi posho za kujikimu, kituo hakina mashuka, vyoo vimechakaa sana, hakuna chumba cha kuhifadhia maiti, na wala Kituo hakinufaiki na Mfuko wa Afya, (*Health Basket Fund)*, kama mwongozo unavyotaka. Kamati ilielekeza Ofisi ya Mkaguzi Mkazi kufanya uchunguzi na kubaini namna ruzuku ya afya inavyogawiwa na kutumika kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005 na 2005/2006 na kutoa taarifa kwa *LAAC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipokea ombi la Mkuu wa Mkoa wa Manyara ambalo ni la siku nyingi kusaidia kusukuma upandishaji wa hadhi hospitali ya Dareda ili haspitali ya sasa iliyoko mjini Babati iwe kwa ajili ya Mji wa Babati na hospitali ya Dareda iwe Hospitali Teule chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Babati. Hii itaondoa mvutano ulioko hivi sasa kuhusu umiliki wa hospitali iliyoko mjini Babati. Kamati ilitembelea hospitali ya Dareda ambayo ina majengo mazuri ya kutosha na eneo kubwa pamoja na wataalamu wa kutosha. Kamati inaitaka Serikali kuangalia kwa uzito unaostahili maombi ya Mkuu wa Mkoa wa Manyara, na kupandisha hadhi hospitali ya Dareda kuwa hospitali teule kama ilivyoombwa. Jambo hili litaongeza kiwango cha huduma kwa wananchi wa Wilaya ya Babati. *(Makofi.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilishtushwa pale ilipojionea mfano halisi wa matumizi mabovu ya rasilimali, fedha na nguvu za wananchi, ilipotembelea shule ya msingi ya Qares. Shule hii iliyoanza kujengwa mwaka 2004, ina vyumba vinne vya madarasa yote yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi hadi lenta. Majengo hayo yametelekezwa, hayajapauliwa, hayana madirisha wala sakafu. Shule hii ipo chini ya shule mama inayoitwa Nakwa. Kamati iliiagiza Halmashauri ya Wilaya ya Babati ichukuwe hatua za haraka kupauwa majengo hayo ili nguvu za wananchi zisipotee bure

na kupunguza haraka msongamano ulioko katika shule mama ya Nakwa na *LAAC* itaarifiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie Maoni na Mapendekezo ya jumla ya Kamati. Kutokana na changamoto zilizoko katika Halmashauri na ili kuimarisha uwajibikaji, yafuatayo ni mapendekezo ambayo Kamati inataka yafanyiwe kazi na Serikali:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Menejimenti ya Utendaji, hasa Wakurugenzi Watendaji, Waweka Hazina, Maafisa Mipango na Wakaguzi wa Ndani watakaosababisha Halmashauri kukosa fedha za maendeleo kwa sababu ya hati chafu ndio wanaostahili kuwajibishwa kwa sababu vigezo vyote vinavyoangaliwa katika kutoa hati hiyo viko mikononi mwa Menejimenti hiyo. Jamii nzima ya Halmshauri isihukumiwe kwa uzembe wa mtu ama watu binafsi. Na mara nyingi hata Madiwani hawahusiki sana.

Katika Halmashauri ambazo kuna uhaba mkubwa wa wataalamu, Serikali Kuu iingilie kati kwa kuwapeleka au kuwaajiri wataalamu hao katika nafsi muhimu hasa katika Idara zinazohusika na Menejimenti ya fedha, afya, elimu, maji na kilimo, yaani maeneo yote yanayogusa maisha ya mwananchi moja kwa moja. Hapa ndipo huduma hasa kwa wananchi inakokuwa. Serikali iongeze kasi ya kufanya marekebisho muhimu ya sheria na kanuni za usimamizi wa fedha katika Mamlaka ya Halmashauri. Sheria na kanuni zinazotumika ni za zamani na hivyo kupitwa na wakati. Mfano sheria za Halmashauri hazitambui kuwepo kwa Kamati za Ukaguzi (*Audit Committees).* Na sheria nyingine tumezitaja kwenye taarifa yetu ndefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mlipaji Mkuu (*Paymaster General),* na Mhasibu Mkuu wa Serikali (*Accountant General),* wawe na Mamlaka ya kusimamia fedha za umma zinazotengewa Mamlaka za Serikali za Mitaa lakini bila kupunguza uhuru wa Halmashauri kujitawala na kujiendesha. Kama ilivyokwishafanyika kwa Serikali Kuu, Serikali itunge kanuni za kutekeleza masharti ya kifungu cha 51 cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Namba 9 ya 1982, kinachohusika na kutoza, yaani adhabu, kuhusiana na hitilafu na upotevu wa mali. Kanuni hizo zieleze wazi ni makosa gani, ni nani mwenye uwezo wa kutoza na hatua zipi za kuchukuliwa.

Katika Serikali Kuu Kanuni za fedha za umma yaani tozo na adhabu za mwaka 2005, zinaeleza wazi aina ya kosa la kutozwa, aina ya tozo, na mwenye uwezo wa kutoza. Hii haipo kwenye Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho haya yatachangia kuboresha nidhamu ya matumizi ya fedha kwa watumishi wa Serikali za Mitaa. Kamati inashauri pia vitengo vinavyoshughulika na manunuzi katika Halmshauri viimarishwe kwa kuajiri watumishi wenye sifa zinazostahili. Pawe na mafunzo ya mara kwa mara kwa wote wanaohusika na manunuzi katika ngazi mbalimbali katika Halmashauri ili uelewa wao katika kutekeleza wajibu wao uende na wakati.

Serikali iangalie namna ya kuimarisha usimamizi wa mikataba mbalimbali, mfano Halmshauri zinazowatumia mawakala katika kukusanya mapato kutoka vyanzo vya ndani, kuhakikisha mapato yanakusanywa na yanawasilishwa katika Halmashauri kwa usahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *TASAF* iongeze ufanisi katika kuzipatia ruzuku Halmashauri kwa kuzingatia muda muafaka ambao Halmashauri zenyewe zinapendekeza katika maombi yao. Halmashauri zilizo nyingi zinalalamika kuchelewa kupewa ruzuku hiyo, hivyo baadhi ya miradi kushindwa kutekelezwa kwa wakati hasa miradi ya ujenzi ambayo mara nyingi utekelezaji wake hutegemea sana muda. Kiasi cha fedha kinachopelekwa katika shule za msingi kwa ajili ya *capitation* hakifikii dola za kimarekani 10 kama ilivyo katika mwongozo. Kamati inaitaka Serikali kufuatilia suala hilo na kutoa maelezo ni kwa nini kiasi hicho cha ruzuku kinatolewa pungufu tofauti na mwongozo ulivyoelekeza na Bunge lilivyojulishwa.

Kamati inaona ni vema Halmashauri zetu zilizo na wataalamu wa kutosha ziendeshe zenyewe zoezi la kukusanya kodi mbalimbali zinazotozwa katika maeneo yao kuliko kuwatumia mawakala ambao wanaonesha kutokuwa waaminifu. Kamati inaagiza vitabu vya kukusanyia ushuru vinavyotumiwa na mawakala mbalimbali katika baadhi ya Halmashauri, vitengenezwe na Halmashauri zenyewe. Kamati inashauri vitabu vya kukusanyia ushuru vinavyotumiwa na mawakala mbalimbali katika baadhi ya Halmashauri vitengenezwe na Halmashauri kutoka kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na si vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla miongozo na viwango vingi vya ruzuku zinazopelekwa Halmashauri vimepitwa na wakati, ni vema ikapitiwa upya na kufanyiwa marekebisho. Baadhi ya sheria na miongozo hiyo ni pamoja na Sheria ya Fedha ya Halmashauri, kitabu cha mwongozo wa hesabu (*Local Authority Accounting Manual), Memorandum* ya fedha ya Serikali za Mitaa (*Local Authority Financial Memorandum)* ambayo ni ya mwaka 1997. Ni vema pia miongozo hiyo ikatafsiriwa katika lugha ya Taifa ili kuwa na wigo mpana wa watumiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nihitimishe kwa kusema kwamba Kamati ina matumaini makubwa kwamba maudhui ya Taarifa hii yakichanganywa na michango mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge watakaochangia hoja hii yatatengeneza njia sahihi ambayo Serikali ikizingatia na kuifuata itazifikisha Serikali za mitaa ambapo angalau asilimia hamsini ya Halmashauri zitaweza kujiendesha zenyewe ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati kabisa ninaomba kutambua utekelezaji thabiti wa majukumu ya Kamati hii kama ulivyokwisha kukamilishwa na wajumbe waliotutangulia katika Kamati iliyopita, ambayo ilikuwa chini ya uongozi wa Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, aliyekuwa Mwenyekiti, Mbunge.

Mheshimiwa Msindai kwa sasa ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati yetu. Naomba nitumie fursa hii pia kuwatambua Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa Kamati ya sasa

kama ifuatavyo: Mheshimiwa Mgana Msindai, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Zabein Mhita, Mheshimiwa Halima Kimbau, Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mheshimiwa Ahmed Ali Salum, Mheshimiwa Juma Ngasongwa, Mheshimiwa Grace S. Kiwelu, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa Laos Mhina, Mheshimiwa Dastan Mkapa, Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Benadeta Mushasho, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Iddi Azzan, Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mheshimiwa Dakta Zainab A. Gama na Dakta Wilbroad Slaa ambaye ndiye ninayezungumza Mwenyekiti wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Katibu wa Bunge, Ndugu Damian S. L. Foka, kwa kuhakikisha kuwa Kamati inakamilisha kazi zake bila vikwazo. Naipongeza na kuishukuru pia Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hasa *Division* ya Ukaguzi wa Hesabu za Halmashauri na Mikoa na Maofisa kutoka Hazina, Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali. Maafisa kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu na Tawala za Mikoa, Idara ya Uratibu wa Serikali za Mitaa, kwa ushirikiano wanaotupatia katika kukamilisha majukumu ya Kamati hii yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati kabisa Makatibu wa Kamati: Ndugu John N. Joel na Ndugu Dickson Bisile. Ninafanya hivyo kwa sababu ya ushirikiano na umahiri wao katika kuandaa, kuratibu na kuihudumia Kamati hasa katika kutoa ushauri wa kitaalamu juu ya namna ya kuendesha shughuli za Kamati yetu kwa kufuata misingi ya kanuni zilizowekwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2005/2006 pamoja na mapendekezo na maoni yaliyomo kwenye Taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi.*

**MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Mwenyekti, naafiki.**

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI.** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ametoa hoja na ninaona Waheshimiwa Wabunge Wajumbe wa Kamati kwa umoja wao kabisa wameunga mkono hoja hiyo. Sasa Waheshimiwa Wabunge ninaziweka hoja hizo zote mbili mezani tayari kwa kujadiliwa. Na nilikuwa naomba tu niseme kwamba hoja hizi zitajadiliwa na Waheshimiwa Wabunge wafuatao:- Mheshimiwa Hamad Rashid, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani ataanza, Mheshimiwa Zubeir Maulid, Mwenyekiti wa Bunge, atafuatia, Mheshimiwa Asterina Kilasi, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Omar Kwang, Mheshimiwa Fatuma Fereji, Mheshimiwa Benadeta Mshashu, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, lakini ninayo orodha inayoendelea. Nitaendelea kuwataja kadiri muda utakavyoendelea kuturuhusu.

Kwa hiyo, bila kupoteza muda naomba nimwite Mheshimiwa Hamad Rashid, aanze kuchangia mada hizi zote mbili na anayefuata Mheshimiwa Zubeir Maulid ajiandae.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza ili niseme kwanza naunga mkono mapendekezo yote yaliyotolewa na Kamati zote mbili *PAC* na *LAAC*, na ninaomba Waheshimiwa Wabunge tuyaunge mkono na tuyasimamie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza la jumla kwa upande wa Serikali. Wakati Mheshimiwa Cheyo anawasilisha taarifa hii alizungumzia suala zima la *Tansolt.* Kamati ya *PAC* mwaka 2004 ilifanya uchunguzi wa *Tansolt* na hatimaye ikawasilisha taarifa Bungeni, na mpaka leo Serikali haijatekeleza. Sasa huu ni ushahidi tosha kwamba pamoja na kazi nzuri zinazofanywa na Kamati, na mapendekezo yanayotolewa na Kamati zetu lakini bado Serikali haijatilia maanani katika kutekeleza yale yaliyopendekezwa na Kamati na hatimaye Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, la kwanza ambalo naliomba sana kwa Serikali na hasa Ofisi ya Waziri Mkuu, kuanzia sasa tutataka tupate utekelezaji wa maamuzi ya Kamati zetu za Bunge kwa kila kipindi kinachofuatia. Kwa sababu sasa hivi tunakuta maagizo mengi Kamati inatoa lakini hakuna utekelezaji wake. La kwanza ninaloomba la jumla ni kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu sasa iratibu vizuri maamuzi ya Bunge hili na maamuzi hayo yawasilishe kwenye vikao vya Bunge kwa kusema kwamba Kamati fulani imetoa maagizo fulani na Serikali imeyatekeleza kiasi fulani. Kwa utaratibu huo tutakuwa hatuwezi kurudia mambo yale yale. Hilo lilikuwa la kwanza. *(Makofi).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni suala la adhabu ya jumla inayotolewa kwa Halmashauri. Nakumbuka katika nchi yetu adhabu ya jumla ilikuwa ya wezi wa mifugo. Katika vijiji huko kukatokea wizi wa mifugo, ng’ombe wakiibiwa wanapomalizia nyayo basi watu wote wa kijiji walikuwa wanaadhibiwa. Wakati huo ilikuwa Mambo ya Ndani, sijui kama sheria hii nafikiri bado ipo. Lakini *capital punishment* kwa ajili ya maendeleo ni hatari sana.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza naomba sana Waheshimiwa Wabunge tupitishe azimio tukatae kabisa *capital punishment* kwa ajili ya Halmashauri zetu. Maafisa wanaokosa ndio wachukuliwe hatua haraka iwezekanavyo. Ni dhambi kuwaadhibu watu wetu kwa sababu ya watu wetu wanaolindwa na utaratibu wa utawala halafu maendeleo hayapatikani katika sehemu hizo. Kwa hiyo, naomba kabisa hili tulimalize. Bunge hili hili tulimalize, utaratibu wa *capital punishment* kwa Maafisa ambao wanajulikana kwa makosa waliyoyafanya lakini wanaadhibiwa watu wengine waliokuwa hawahusiki na hasa suala lenyewe la maendeleo hii ni dhambi kubwa tunayoifanya, na si vizuri tuikubali kuendelea. *(Makofi).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, naziomba Kamati zote kwamba kumekuwa na mambo ya jumla kwamba hesabu hazitunzwi kwa sababu hakuna utaalamu lakini si

kweli. Mimi siami kabisa kama *Central Bank* kunakosa utaalamu wa kujua kama mradi wa mwananchi *gold mines* utakaozalisha kilo moja ya dhahabu *Central Bank* itoe shilingi bilioni 8 kuwakopesha eti kwa sababu hawana wataalamu, si kweli hata kidogo! Si kweli kwamba Alex Stuwart tu apewe mkopo *no,* apewe tenda ya shilingi bilioni 60! Na taarifa yao naambiwa ni nzuri lakini wananchi hawajui namna ya tenda ilivyofanya halafu tuseme hakuna utaalamu.

Kwa hiyo, yako maeneo ambayo hayana utaalamu ambayo na ni vizuri sasa Kamati zetu za Bunge zote kwa ujumla tu-*identify* lile tatizo ambalo lipo badala ya kukubali maneno ya jumla. Mimi siami kama Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje itumie shilingi bilioni halafu iseme haina utaalamu. Nyinyi wataalamu wote mlioko wahasibu wazuri waliopelekwa nje wote wazuri tu hakuna aliyepelekwa *below standards* lakini bado matumizi ya Serikali ni mabaya.

Kwa hiyo, suala la kutumia neno la jumla halitusaidi hivyo naziomba Kamati watakapopewa sababu yoyote turudie utaalamu wa Kamati za zamani, huku tulikuwa tunasema ofisi fulani ina *accountant* mwenye *grade* fulani, kwa hiyo, huyo hafai kwa sababu ya uwezo wake mdogo lakini hili neno la jumla halitusaidii sana na matumizi ya Serikali yataendelea kuwa mabaya kwa sababu ya kisingizio ambacho hakipo, hili lilikuwa la Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, Wizara ya Elimu, sehemu zote mbili, elimu ya juu na elimu ya ufundi ukitazama *page* 23 na 27 utakuta zaidi ya bilioni 27 kwa elimu ya juu pekee yake wakati wanafunzi wetu wana matatizo ya fedha za kusomea, matatizo ya vifaa na kadhalika. Kwa hiyo ukiziangalia matumizi mabaya yaliyomo ndani ya taarifa hizi za mdhibiti mkuu utakuta si chini ya asilimia 30 ya bajeti imekwenda hewani hivi hivi katika recurrent hii ni hatari. Kwa hiyo, ili tatizo hili liondoke kuna haja sasa Bunge lako lipewe uwezo wa kutosha, hivyo ile programu tuliyoiandaa Bunge iwe *funded* vizuri iweze kusimamia mambo haya ya kuisimamia Serikali kwa mujibu wa Katiba na sheria za nchi. (*Makofi*)

Chombo pekee ambacho kitaisaidia Serikali kufanya kazi vizuri na kutumia pesa za nchi vizuri ni Bunge letu la Tanzania hasa kwa kupitia kwenye Kamati zetu. Utaona Kamati ya *LAAC* imeweza kutembelea kufanya *performance audit* katika maeneo machache sana kama wilaya tano, sita tu. Sasa ukitizama idadi ya Wilaya zilizoko na maeneo ambayo tungeweza kufanya *performance auditing* ni maeneo makubwa sana. Mimi nafikiri inahitaji Wabunge kwa pamoja tuangalie namna gani Bunge letu litakuwa na uwezo wa kuisimamia Serikali na kifungu kile ambacho cha fedha tunachopewa ambacho hakitoshi basi tukipate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa hili nataka kuongeza kitu kimoja. Wananchi wengi wanafikiri kwamba zile fedha tunazoomba za ziada tunaomba marurupu ya mishahara, hapana huwa hatuombi mishahara, tunachoomba ni fedha za kwenda kuwasimamia fedha zao na maendeleo yao wananchi. Kamati zinatakiwa zizunguke kila mahali, hazina uwezo kuzunguka kwa sababu ya bajeti ni finyu. Na Sasa hivi wananchi

mmeshuhudia kazi ambayo inafanywa na Wabunge wenu. Tunahakikisha kabisa mkitupa uwezo zaidi Serikali itazidi kuwajibika na nyinyi mtapata maendeleo zaidi. (*Makofi*)

Sasa kama kuna wasiwasi labda Wabunge tunachohitaji kikubwa basi *Auditor General* yupo afanye uchunguzi wa mahitaji yetu na mimi nina hakika kabisa kile tunachokiomba kinawezekana kabisa kikaonekana kidogo zaidi kuliko mahitaji halisi ambayo tunayahitaji.

Kwa hiyo, nafikiri kuwa wananchi watupe hiyo baraka tufanye hiyo kazi na naamini kama kuna wasiwasi nasema *External Auditor* atafutwe afanye uchunguzi aone kama kweli mahitaji halisi ya Bunge ili Bunge lifanye kazi zake na Serikali itupe kiasi hicho. Mimi naamini Bunge linalokuja Wabunge tutasimama kidete tuhakikishe kwanza tunapata fedha za kutosha za kuweza kusimamia utendaji wa Bunge letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la *performance auditing* lazima kunahitajika elimu ya kipekee, moja ni katika suala zima la *procurement*. Manunuzi ukitizama hizi taarifa zote za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, kama tunavyofahamu asilimia kubwa ya bajeti yetu inatokana na manunuzi na bado sheria zetu za manunuzi pamoja na kwamba ni nzuri hazieleweki wala hazifuatwi. Nafikiri kuna haja, na hili tumeishauri Serikali mara nyingi suala la kuwa na orodha ya mahitaji kama Halmashauri zote zinahitaji magari 200 basi magari hayo 200 yanunuliwe mahali pamoja, kuiachia kila Halmashauri ikanunua haiwezekani. *(Makofi)*

Kwanza gharama za ununuzi zinakuwa kubwa. Pili, hatuna hakika kama wanunuzi watalipwa. Kuna taarifa humu JKT wamepewa fedha kununulia magari hayakununuliwa magari kama yalivyotakiwa. Fedha zingine hazijulikani zimekwenda wapi kama shilingi 1.5 bilioni. Sasa hii sio hali nzuri. Kwa hiyo, Serikali sasa itusikie Wabunge kwamba tunahitaji orodha ya *procurement* kwa ajili ya Halmashauri, kama ni magari, kama ni vifaa vyote ili twende kwenye *international tender* ambayo itatusaidia kutupunguzia gharama za manunuzi si chini ya asilimia 30. Kwa bajeti tegemezi kama ya kwetu tunahitaji kufanya jambo hili. Wabunge tumekuja mara nyingi kulalamika Bungeni lakini bado Serikali haijataka kusikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bunge lako Tukufu hili tumeomba taarifa ya Alex Stuwart kwa bahati mbaya mpaka leo pamoja na ahadi zote za Mawaziri Wakuu waliokuja hapa kuniahidi hawajatoa lakini hata taarifa ya *Auditor General* nayo haipo, sasa unajiuliza hizi shilingi bilioni 60 zilizotumika kwa kazi ya *audit* ya dhahabu kwa nini haionekani katika vitabu vya Mkaguzi Mkuu wa Serikali? Kwa nini hatuoni shilingi bilioni 80 ilizopewa mwananchi *gold mines* katika vitabu vya ukaguzi wa Serikali na nyingine nyingi. MEREMETA ni kichekesho mara uambiwe kampuni ni ya Serikali wengine waseme si ya Serikali wakati mamilioni ya fedha yamekwenda na kwenye *audit report* hazipo. Sasa mimi nafikiri Serikali inahitajika itueleze wazi hizi fedha ambazo zimetumika za wananchi nyingi hazionekani kwenye vitabu vya ukaguzi wowote, sasa ziko wapi? Taarifa zake ziko wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili Waziri yoyote anayehusika atakayekuja hapa tunaomba atujibu hayo masuala mazito, ukaguzi kwenye taarifa zote za *audit* nimezipitia hamna kabisa, hizi pesa zimekwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, namalizia kwamba Ofisi ya Waziri huwa inatenga fedha kwa ajili ya shughuli za Wabunge, ofisi za Wabunge na kadhalika. Kwa upande wetu Zanzibar tumeambiwa zinapelekwa Ofisi ya Waziri kiongozi. Na nina hakika kwa upande wetu sisi wengine sijapata kuona hata senti tano iliyokuja kwenye Jimbo langu kusema hizi ni kwa ajili ya *furniture* au chochote kile. Naitaka Ofisi ya Waziri Mkuu ifanye *special audit* kwa ajili ya kujua hasa fedha zilizopelekwa Ofisi ya Waziri Kiongozi kwa ajili ya Wabunge Zanzibar. Naomba *special audit* na tupate taarifa hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja, asante sana. (*Makofi*)

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia hoja mbili hizi ambazo zimewekwa mbele yetu hapo na Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwanza niseme ni mjumbe kwenye Kamati ya Hesabu za Serikali na hivi sasa ni Makamu Mwenyekiti kwenye hii Kamati ya Hesabu za Serikali. Lakini ripoti inayotolewa sasa kwa wakati ule nilikuwa ni mjumbe wa kawaida kwenye Kamati ya Hesabu za Serikali. Kwa hiyo, naendelea kuwa mjumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali, hivyo, ni ripoti ambayo pia inanihusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza kuchangia kwanza kwa kuonyesha furaha kwamba ile kazi ngumu tuliyokuwa tunaifanya hivi sasa imeanza kupata mwanga kwani katika shughuli ambazo Serikali au samahani Bungeni limeorodhesha ni pamoja na kusomwa kwa mara ya kwanza kwa *Public Audit Bill* ya 2008 ambayo haijasomwa bado lakini katika shughuli inayoonekana kwamba itasomwa. Kwa hii itasaidia sana katika utendaji wa kazi wa ofisi hii ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu kwa kweli umechelewa lakini kwa kuwa unakuja tuna furaha. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wakati utakapokuja Muswada tutachangia kwa kiasi kirefu na kujaribu kuuboresha ili kuona namna gani tutaweza kuzifanya shughuli zetu. Lakini ofisi hii kwa kipindi kirefu sana imekuwa ikifanya kazi chini ya Wizara ya Fedha. Kwa kifupi uhuru wake upo haueleweki (*questionable)* kidogo kwa kuwa wanafanya kazi chini ya Wizara. Walikuwa hawako uhuru kiasi ambacho tunadhani ilikuwa ipo haja ya kuleta Muswada ili waweze kujitegemea na waweze kufanya kazi bila ya kumhofia mtu mwingine yeyote kuwa juu yao. (*Makofi*)

Nikiacha hilo kwa sababu litakuja tutalizungumza kwa kirefu, nizungumze suala jingine ambalo kidogo lilikuwa tata, linajilotokeza ni suala *double accounting* ambalo nafikiri Mheshimiwa Mwenyekiti wa Hesabu za Serikali pia ameeleza kwenye ofisi yake

kwamba kuna hizi fedha ambazo zinapelekwa kwenye Halmashauri. Fedha hizi zinapelekwa moja kwa moja kwenye zile Halmashauri za Wilaya lakini katika Kamati ya Hesabu za Serikali tunaonana na mikoa na kuwapa hati chafu au safi. Kwa kweli hapa tunawaonea kwa sababu wao zile fedha hawazigusi kabisa, watumiaji ni wengine lakini tunam-*access* mtu mwingine ambaye yeye kabisa zile pesa hazigusi. Yeye anapata taarifa tu kwamba pesa zimekwenda na hatimaye kupata hati chafu au hati safi kulingana na matumizi yalivyotumika kule kwenye Halmashauri. Sasa nadhani hili kidogo lilihitaji marekebisho, lilihitaji liwekwe sawa ili tusimwone yule ambaye halimhusu na msalaba ubebwe na yule ambaye unamhusu na kama sifa nzuri apewe yule ambaye inamhusu kweli na kama sifa mbaya pamoja na adhabu basi aadhibiwe yule ambaye ameyafanya yale makosa, kwa hiyo, hili litahitaji kurekebishwa.

Jambo kubwa hasa nilitaka kulizungumza lilihusu hizi fedha za wahisani kwenye miradi ya maendeleo. Katika ukurasa wa 10 wa ripoti ya Mheshimiwa Mwenyekiti wa Hesabu za Serikali nafikiri ameeleza kwamba bajeti yetu ni tegemezi kwa asilimia 20 katika Matumizi ya Kawaida na asilimia 80 kwenye Matumizi ya Maendeleo. Hii kwa ujumla wake maana yake au tafsiri yake ni kwamba kile tunachokichuma kama nchi tunatumia zaidi ya kile tunachokichuma. Yaani kile tunachokichuma tuna utegemezi zaidi kuliko makusanyo yetu sisi wenyewe halisi. Lakini ukienda kwenye matumizi halisi ukiangalia yale mahesabu unakuta kinyume chake kingi tunachokitumia ni chetu wenyewe kuliko hata hicho tunachosaidiwa.

Lakini sasa pana utata hapa kidogo kwamba mara nyingi inaposomwa bajeti, bajeti yetu inaonekana ni kubwa na hasa hii miradi ya maendeleo na hasa fedha tunazochangiwa na wahisani. Sasa hapa kidogo tunatakiwa tuwe wazi na tuanze kujizoesha kidogo kidogo kujiondosha katika utegemezi wa watu wengine na hasa kwenye shughuli zetu za maendeleo. Kwa sababu kinachojitokeza sasa hivi ni kwamba wahisani wanajitokeza wengi wanaahidi.

Wanayoahidi Mheshimiwa Waziri wa Fedha anasoma bajeti hapa, mwisho wa kusoma bajeti zinatolewa, sifa katika mataifa yale kwa mataifa na hasa *bilateral country* zinazungumza uhusiano wa nchi kwa nchi ukiacha haya mashirika ya kimataifa. Wameahidi kusaidia kiasi kadhaa lakini katika uhalisia hukuti pesa ambayo imetolewa. Mwisho wa mwaka unakuta ni sifuri kabisa maana yake hawakuchangia lakini wanakuwa na sharti kwamba fedha za ndani pia zichangiwe ili kuweza kusaidia zile zao wanazotoa katika shughuli ile ile ya maendeleo.

Lakini kinachojitokeza ni kwamba sisi wenyewe tunamudu kuchangia kile ambacho tunatakiwa tuchangie lakini wenzetu hawaleti kile ambacho wanaahidi. Sasa hapa pana tatizo, Serikali pamoja na Mawaziri ambao wanaenda ku-*negotiate* hii misaada waanze utaratibu wa sasa hivi wa kuwa na uhakika. Wapewe uhakika kabisa kwamba hizo fedha zitakuja ndiyo waziweke kwenye bajeti, wasiahidiwe ile ahadi wakaileta kwenye bajeti kwa sababu ahadi ile inawapa matumaini. Pamoja na tamaa wananchi hatimaye kile ambacho wana matumaini nacho hawakipati kwa uhalisia, inakuwa kama hadithi ya mtu ambaye analima kwa kumtumia mnyama kama ng’ombe au punda

umemfunga jembe amelima, mwisho wa nguvu zake amechoka hawezi tena kuendelea, unamtafutia kitu cha kumdanganya, unamfunga na karoti inamning'inia mbele. Sasa anaona kama anaipata ile karoti atakula baadaye lakini kila akienda analima zaidi lakini karoti pia haifiki.

Sasa tuache huu utaratibu tusiingize fedha ambazo tunaahidiwa na hatuna uhakika kwa sababu mwisho wa mwaka ukiuliza kwa nini fedha hizi hazijaletwa maelezo yanayotoka kwa Makatibu kwamba pengine kuna masharti. Kwa hiyo, hii misaada yenye masharti sijui muwafunge wala rushwa kumi masharti haya wasikubali kabisa na isiingizwe kwenye bajeti na si hilo tu. Mambo mengine ambayo wanaeleza ni kwamba bajeti zao ziko tofauti na zetu sasa pale walipoahidi walikuwa hawalijui hili kwamba bajeti zao zinaishia Aprili au zinaishia Disemba na yetu sisi inaishia Juni. Kwa hiyo, haya wayaangalie wakati wanapo-*negotiate* misaada ili hatimaye kama kweli mtu ana lengo la kutusaidia ile misaada ifike na hatimaye iweze kusaidia katika zile shughuli za maendeleo na wananchi waweze kufaidika na kile ambacho kinatamkwa ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa nililotaka kulizungumza lilikuwa ni hili. Kwa hiyo, naishauri Serikali na kwa kweli ripoti hizi ziliposomwa ingependeza sana Serikali ikawepo, ikasikiliza kila Wizara ikawepo ikachukua yale yanayowahusu, kwa sababu hizi ripoti mbili zimegusa karibu Serikali nzima. Kwa hiyo, wakachukua yale maeneo ambayo yanawahusu pamoja na ushauri ambao umetolewa basi baadaye wakaeleza ili wananchi wakajua ni nini kinajiri katika haya masuala. Tunaichoshauri Serikali hivi sasa tuanze kujizoesha kujitegemea, tuanze kujivua kidogo kidogo kwenye kusaidiwa. Kwa sababu pamoja na kwamba tunapewa tamaa na hicho wanachotuahidi hakififiki kama wanavyoahidi, kwa hiyo, pamoja na kwamba tunaendelea kuomba tusaidiwe lakini kidogo kidogo, tuanze kujizoesha hatimaye baada ya miaka kama 10 pengine tutafika pahali na kwa kweli hili linawezekana.

Kwa sababu ziko nchi hazisaidiwi na nchi maskini kama sisi lakini maisha yanakwenda, na mifano ipo na tunakumbukumbu hata kile kipindi cha mwaka 1995-2000 kule Zanzibar misaada ilikuwa imeondoka kabisa kutoka kwa nchi wahisani na watu walikuwa wanaishi. Mambo yalikuwa yakifanyika kwa kujitegemea, hicho hicho kidogo ulichonacho unajibana kwenye hicho hicho, ni bora tuwe nacho kidogo tugawane kuliko kuahidiwa kingi ambacho hakiji na hatimaye tunaishia tunakufa njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu mkubwa ulikuwa ni huo tuangalie sana kuja kusoma bajeti ambazo baadaye tunakuwa tunazungumza vitu siyo vya kweli kwa sababu kile ambacho tunaahidi kwamba tutaletewa wahisani wahusika wanakuwa hawaleti. Na wanakuwa na masharti, wakiwa na masharti ni bora tumaliziane nao kwenye meza kunywa chai na kahawa tukacheka lakini huku ndani kwenye Bunge tusome bajeti ambazo ni za uhalisia kwa sababu hatutaki kuonyesha kwamba bajeti yetu ni kubwa sana lakini hatimaye haiendi kwa mujibu wa kile ambacho kinasomwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, langu lilikuwa hilo, ni hayo machache kwa hiyo, napenda kukushukuru sana kwa hii nafasi na naziunga mkono hotuba zote mbili ambazo

zimesomwa na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali pamoja na ile ya Hesabu za Serikali za Mitaa, naomba kuishia hapo. (*Makofi*)

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani *microphone* yangu haitoi sauti. Naomba nikushuru sana kwa kunipa nafasi ya dakika hizi chache na mimi niweze kuchangia hoja hii ya Kamati ya *LAAC* na *PAC*. Lakini na nitajikita zaidi kwenye Kamati ya *PAC* kwa sababu ndiko nilikokuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Naomba nianze kwa kuwapongeza Kamati na Mwenyekiti kwa kuwasilisha vizuri. Lakini nipongeze uongozi wa kwako Mwenyekiti, hasa ni mara ya kwanza kuona kwa miaka mitano ambayo nimekuwa kwenye Kamati pale ambapo Kamati zinasita kufanya kazi taarifa nazo zimekuwa haziwasilishwi Bungeni.

Hii nafikiri ni mara ya kwanza kwamba Kamati inaendelea na taarifa zake kuzitolea Bungeni. Lakini la pili na mimi nasikitika kidogo kwa sababu huo mpango tuliosema shughuli za Serikali zianze halafu shughuli za Kamati zitolewe baadaye, maana yake inaonekana kazi zetu ambazo tunazifanya siku 60 kwa mwaka mzima ni kama hazina maana. Kwa sababu sisi Wabunge tunakaa kusikiliza shughuli za Serikali na tunategemea Serikali nayo ikae hapa yote kwa ujumla itusikilize yale ambayo tumeyaona huko. Kwa hiyo, hilo ningeomba kwa kweli nitoe angalizo, linatukatisha moyo kufanya kazi za Kamati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na hoja ya muhimu moja. Nimekuwa kwenye Kamati ya *PAC* miaka 7. Mambo ambayo tumekuwa tukiyatolea taarifa ndani ya Bunge hili ni yale yale. Lakini mategemeo yetu kwamba tunapotoa taarifa hapa Waziri mhusika anakuwepo na kwa maana ya Wizara nzima, wanasikiliza hoja zetu kwa sababu tunafanya kazi kwa niaba ya Mawaziri wenzetu huko. Mambo mengi hawayajui huko yanayofanyika, sisi ndiyo tunayaona. Kwa hiyo, tunachotegemea sasa pale Mawaziri wanapojibu hapo wanapochangia kwamba Serikali itakuja kuleta majibu Bungeni, kwa sababu Kamati ikileta hapa maana yake ni maazimio ya Bunge zima. Sasa yametekelezwa vipi na yamejibiwa vipi tunategemea Serikali ije itoe kauli humu ndani kwamba taarifa za Kamati, maazimio yalikuwa kama 10, 20 basi yasomwe na utekelezaji ili Wabunge wajue kweli kazi tulizozifanyia kazi zimetekelezwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo linanigusa kwa sababu tulikaa hapa mwaka jana tumetoa taarifa Waziri wa Fedha mwenye dhamana wakati huo akasema majibu yataletwa na nilikuwa nategemea kabla ya kuwasilisha bajeti yake na nawaomba Waheshimiwa Wabunge, Mawaziri, watupe kwanza taarifa ya yale ambayo sisi tumeyauliza. Kwa sababu (mtu tumempa) Wizara tumeipa bajeti ya shilingi bilioni 40 kwa mfano, Elimu ya Juu inatuletea kwamba malipo ya shilingi bilioni 16.7 yamelipwa bila kuwa na nyaraka na hazijapatikana na hatuna hakika kwamba hayo malipo ni halali au hayakufanywa kihalali. Unakujaje kutuomba bajeti tena tupitishe wakati zile nusu ya zile bajeti tulizokupa mwaka jana hujatuhakikishia kama zimetumika vizuri? Kwa hiyo, hilo ningependa Serikali iwajibike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti la pili, Mawaziri wao kwa niaba ya Serikali wanasoma bajeti lakini matumizi wanawaachia Maafisa Wahasibu, sijui wanapata muda gani wa

kuyapitia yale matumizi. Je, zile hesabu wanazipitia? Zile hoja za Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali wanazipitia ili walinganishe kwamba tulichokiomba ndicho kilichotumika. Sasa nafikiri sisi Kamati ya *PAC*, *LAAC* na *POC* ni jicho lao ndiyo tunaowasaidia, waungane na sisi na ikibidi siku zingine kwenye majadiliano wakipata nafasi waingie tunapohoji hizi hesabu waweze kuona ni vitu gani Maafisa Wahasibu wanajibu na taarifa ambazo wanazitoa. (*Makofi*)

Lakini la tatu, kunajitokeza hoja binafsi nyingi, kwa mfano, ukiangalia hizi ratiba tulizozipata sasa zote zilikuwa zimeibuliwa na Kamati ya *PAC*, uuzaji wa nyumba za Serikali tulileta taarifa hapa tukaomba maelezo. Sasa Waziri mwenye dhamana wakati huo angewajibika akatueleza, akatoa mlolongo mzima, sidhani kama kungekuwa na Mbunge yeyote wa kuja kuleta hoja binafsi tena ndani ya Bunge kwa sababu tungekwishaelewa.

Tumetumia fedha nyingi sana, tumekwenda mpaka Uingereza karibu shilingi milioni 40 kwa ajili ya *Tansort*. Mambo ya madini tulitegemea leo hii katika miaka miwili, mitatu tungeweza kupata majibu kamili. Maduhuli ya mapato ya madini tumezunguka na wakati huo nilikuwa kwenye Kamati. Mwenyekiti akiwa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, amekuja Mheshimiwa John Cheyo, tumeileta Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imesababisha mpaka Mheshimiwa Rais akaunda kamati kubwa ya kutembelea kukagua kujua ni kiasi gani tunakipoteza kwenye madini. Kumbe wenzetu wa Wizara inayohusika ingeleta mchanganuo na taarifa kamili tusingeendelea tena kupoteza fedha kwa ajili ya kuunda kamati kumsumbua Rais tena aunde kamati. Kwa hiyo, hilo nilikuwa natoa msisitizo kwamba basi wenzetu Mawaziri muone kwamba hizi *Watchdog Committees* zinafanya kazi kwa niaba ya kwenu na yale mambo ambayo yanatolewa hapa yatolewe majibu kwa kadri ambavyo inabidi.

Nimebahatika kwenda kwenye kamati za aina hii nchini Uingereza na amesema Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* na Demark. Unaposikia Afisa Mhasibu au Waziri ameitwa na *PAC* nchi nzima inashituka kwamba ameitwa kufanya nini kwa sababu zile kamati zimepewa meno, zimepewa uwezo. Kama kuna hoja imetokea kwamba umeitwa na Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* mtu anafikiri hivi naitwa kufanya nini kule? Lakini sasa *PAC, POC, LAAC* zimekuwa kama ni *routine* tu kazi za kawaida. Nakumbuka huko nyuma walisema mnafufua maiti kwa sababu watu walishakula fedha.

Lakini msingi wa Kamati hizi ukifanya kazi vizuri maana yake unamfanya yule mtu kesho asirudie tena yale makosa. Kwa hiyo, nafikiri kuimarishwa kwa Kamati hizi ni muhimu na kubadilika kama kamati zingine zinavyobadilika si vizuri sana. Kwa mfano, Denmark wanaseama hii Kamati haibadiliki, walitupa na muundo wa Kamati nzima ya *PAC*. Kuna wengine ni wajumbe ambao siyo Wabunge, vyama vya kisiasa mbalimbali vimeleta mjumbe mmoja mmoja kuja kujiunga na Kamati ya *PAC*. Wanakuwa na ofisi yao na sekretarieti yao na ripoti inaandikwa kwa pamoja na Ofisi ya *CAG*.

Kwa hiyo, moja kwa moja *CAG* anakuwa na *PAC* na taarifa inatolewa Kiserikali, kwa hiyo, ndiyo maana mtu anakuwa mwoga kwamba nimeitwa *PAC*, nimeitwa *LAAC*

kuna jambo zito na zinatolewa taarifa na wananchi wanafahamu. Kwa hiyo, nafikiria vilevile muundo na uwezo wa kamati hizi uwezeshwe. Kama muundo wetu ni huu tulionao lakini angalau tupewe meno. Kwa nini nasema hivyo? Tumekuwa tukitoa mapendekezo hapa ya toza, adhabu, lakini kama *PAC* huwezi kumpa Afisa Mhasibu adhabu kwa vile huna uwezo huo, unatakiwa upendekeze kwa Waziri wa Fedha, Waziri wa Fedha kwa mamlaka aliyopewa ndipo ampe adhabu. Lakini tunapataje *feedback* kwamba yule mtu amepewa adhabu, hatujawahi kupata kwa miaka yote ambayo nimekuwa kwenye Kamati hii.

Kwa hiyo, ndiyo maana watu hawaoni hata unapomwita kwenye *PAC* kujiandaa kama adhabu haipo. Kwa sababu tunafanya *in camera* hawatangazi kwenye vyombo vya habari yanaishia mle na ikiwekwa kwenye *shelf* ile taarifa imekwisha. Sisi tunakuwa na kazi ya kuuliza mmetekelezaje lile tuliloagiza juzi, mmefanyaje na Katibu anakuwa hana woga wa kuja kuwajibu kama Kamati. Kwa kweli nafikiri hilo tulizingatie zaidi, tuziimarishe Kamati tuzipe uwezo. Ikibidi hizi Kamati siyo lazima zibadilike kila baada ya miaka miwili na nusu ziwe na wajumbe wa kudumu ili waweze kufuatilia kwa miaka yote ya maisha ya uhai wa Bunge kusudi tufuatilie yaliyojitokeza huko nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuwa na Mfuko wa Bunge. Wenzangu wamezungumza sana Mfuko wa Bunge. Hizo *Watchdog Committees* zimekuwa zikipata wafadhili. Lakini tumekuwa na matatizo, fedha nyingi kwa mfano *World Bank* walitaka kutusaidia sana kwenye mafunzo, fedha haziwezi kuja Bunge moja kwa moja inabidi ziende kwenye akaunti ya *CAG* halafu yeye ndiye atupe sisi tupate mafunzo. Lakini kama tutakuwa na mfuko wetu fedha hizo za wahisani zitakuja moja kwa moja kwenye akaunti ya Mfuko wa Bunge.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge utakuja muswada wa hii sheria ya kupitisha Mfuko wetu, naomba tuunge mkono kwa pamoja tuhakikishe kwamba tunakuwa na bajeti yetu na tuwe na uwezo wa kujiwezesha kama Kamati. Kwa kuwa hili Bunge linafanya kazi sana. Na naamini wananchi wanaposema tunataka kujiongezea mishahara si sahihi, tunafanya kazi katika mazingira magumu sana ukilinganisha na wenzetu. Ni wewe Mbunge usome miswada binafsi, hoja mbalimbali, unaletewa taarifa saa tano, saa sita uchangie. Mwenyekiti, unakaa kuandika ripoti taarifa ya Kamati, huna sekretari, huna mtafiti (*reseacher)*, huna mtu yeyote lakini wananchi wakitaka matunda mazuri kutoka kwa Wabunge wangetuunga tu mkono kwamba Wabunge wawezeshwe wawe na ofisi zao na hata ile *CDF* tunaiomba ingekuja haraka kusudi kuwawezesha Wabunge kufanya kazi vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niliguswa sana na mambo hayo, kwa kweli nilikuwa nataka kuishauri Serikali ituunge mkono sisi wajumbe wa *Watchdog Committees* ili tuweze kuwasaidia kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa naomba kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Kilasi kwa mchango wake. Lakini Waheshimiwa Wabunge, naomba mtambue uwepo wa

Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali (*CAG)* yuko ndani ya Ukumbi huu wa Bunge. Tunakukaribisha sana na naamini wewe ni mdau mkubwa kweli katika hoja hizi mbili zinazojadiliwa leo na tukupongeze tu kwa kazi kubwa ambayo umekuwa ukiendelea kuifanya katika Taifa letu. Karibu sana, tunashukuru sana kwa ujio wako. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba mniruhusu nitangaze matokeo ya uchaguzi. Matokeo ya uchaguzi, wapiga kura ambao waliojitokeza walikuwa 224 na ndizo kura zilizopigwa, kura tatu zimeharibika. Nafikiri wengine miwani hawakuivaa vizuri ama labda ni matatizo fulani. Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah amepata kura 103 sawa na asilimia 46 ya kura zote zilizopigwa, na Mheshimiwa Prof. Feetham Filipo Banyikwa amepata kura 118 sawa na asilimia 53 ya kura zote zilizopigwa. Sasa ninayo heshima kubwa ya kumtangaza Prof. Feetham Pilipo Banyikwa kuwa mwakilishi wetu kwenye Bunge la Afrika. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa muda wetu umebaki kidogo, naomba mniruhusu niwape nafasi Waheshimiwa Wabunge hao wawili ambao tumewachagua leo kwa maana ya Mheshimiwa George Simbachawene na Mheshimiwa Prof. Feetham Banyikwa watoe shukrani zao leo jioni. Na naamini Waheshimiwa Wabunge wengi watakuwa ndani ya Ukumbi wa Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, lakini naomba niwakumbushe sana kwamba baada ya Shughuli za asubuhi hii, tutaendelea na Semina katika Ukumbi wa Pius Msekwa, na orodha yangu ya wachangiaji nimtaje tu msemaji wa kwanza. Atakayeanza jioni ni Mheshimiwa Mgana Msindai na wengine watafuatia kulingana na orodha nitakayokuwa nimetayarishiwa hapa mezani. Kwa hiyo, nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 Jioni.

(*Saa 7.00 Mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, habari za mchana! Naomba sasa tuendelee na shughuli za leo. Lakini kabla hatujaendelea na shughuli za mchana wa leo, nimepokea taarifa ya dharura kutoka Serikalini na hivyo naomba niwapitishe kwenye Kanuni kabla sijaruhusi taarifa hiyo iweze kuletwa mbele yetu.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni Namba 2, fasili ya 2 inasema kwamba: “Iwapo jambo au shughuli yoyote haikuwekewa masharti katika Kanuni hizi, Spika ataamua utaratibu wa kufuata katika jambo au shughuli hiyo kwa kuzingatia Katiba, Sheria nyingine za nchi, Kanuni nyingine zilizopo. Maamuzi ya awali ya Maspika wa Bunge pamoja na mila na desturi za uendeshaji bora wa shughuli za Bunge na uamuzi huo utaingizwa katika Kitabu cha Maamuzi ili kuongoza mwenendo wa baadaye wa uendeshaji wa shughuli za Bunge.“

Waheshimiwa Wabunge, lakini naomba pia kabla sijaruhusu Serikali kutoa taarifa hiyo niendelee kusoma Kanuni namba 48, Kanuni ndogo ya 3 (a) na (b) na fasili ya (4).

Kanuni ya 48(3) inahusu masharti ya kutumia kuhusu jambo la dharura, sasa fasili ya (3) inasema: "Jambo linaloletwa kwa hoja chini ya Kanuni hii litahesabiwa kuwa ni jambo la dharura iwapo: (a) Athari zake ni dhahiri na linaweza kutokea wakati wowote; (b) limetokea siku hiyo au siku za karibuni na limeletwa bila kuchelewa." Fasili ya (4) ya Kanuni hiyo inasema kwamba: "Jambo lolote litahesabiwa kuwa ni lenye maslahi kwa umma iwapo utatuzi wake utategemea hatua zaidi kuliko zile za utekelezaji wa kawaida wa Sheria peke yake." Baada ya kuwasomea Kanuni hizo nimepokea taarifa kutoka Serikalini kuhusu jambo la dharura lililotokea na sasa namwita Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi ili aweze kutupa taarifa hiyo ya Serikali na kilichotokea mbele ya Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Waziri tafadhali!

## MGOMO WA WANAFUNZI - CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM *(UDSM)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa ya vurufu za wanachuo zinazoendelea katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam sehemu ya Mlimani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukushukuru sana kwa kunipa fursa hii nilieleze Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla juu ya vurugu za wanachuo zinazoendelea katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam sehemu ya Mlimani. Kiini cha vurugu hizi ni wanachuo wa Chuo Kikuu hicho kushinikiza uongozi wa Chuo kuwarudisha chuoni: Kwanza, wanachuo 15 waliosimamishwa masomo na kuondolewa chuoni kutokana na uhalifu walioufanya katika vurugu zao tarehe 17 na 22/2/2008. Wanachuo hawa wako mikononi mwa polisi.

Pili, kusimamishwa kwa muda udahili wa mwanachuo Odong Kefa Odwar kwa kukosa sifa za kuwa mwanachuo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Tatu, wanachuo watano wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam walipelekwa Polisi kwa kukutwa na madawa ya kulevya aina ya marijuana.

Nne, wanachuo wanne waliosimamishwa masomo na kuondolewa chuoni kwa kufanya mgomo haramu, kuingilia na kuvuruga madarasa ili kushinikiza mgomo unaoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanachuo 15 waliofukuzwa kwa vurugu tarehe 17 na 22/02/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 17 Februari, 2008 ulitokea upungufu wa maji katika mabweni ya wanachuo Mabibo. Wanachuo wakaombwa kuchukua maji katika matanki makubwa yaliyopo katika mabweni hayo.

Usiku huo kundi la wanachuo likaanza vurugu kwa kusingizia ukosefu wa maji. Katika vurugu hizo wanachuo hao wakavunja milango 7 ya vyumba vya wasichana ambao ni wanachuo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kuwadhalilisha isivyofaa kueleza.

Pili, wakavunja milango 6 ya wahudumu wa mabweni ya wasichana (*janitors)*, wakavunja *TV* zao, vyombo vingine vya nyumbani na kuwamwagia ndoo nyingi za matope katika *flats* zao.

Tatu, wakavunja *cafeteria* iliyopo hapo kwenye bweni na kuchukua vinywaji zikiwemo soda, bia na pombe kali wakapeleka katika mabweni yao.

Mwisho, wakawazuia wanachuo wa kike kuchota maji na waliokaidi wakawadhalilisha kwa kuwalowesha maji au kuwachania nguo zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 22/2/2008 Jumuiya ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ilijulishwa na *DAWASA* kuwa usiku huo hakutakuwa na maji chuoni kutokana na matengenezo katika bomba linaloleta maji chuoni hapo. Hata hivyo, kundi la wanachuo wapatao 50 walikusanyika usiku wa manane kuandamana na kufanya vurugu kama ifuatavyo wakishinikiza na kusingizia ukosefu wa maji:-

Kwanza, waliandamana mpaka nyumbani kwa Makamu Mkuu wa Chuo (*Vice Chancellor)* kudai maji, wakavunja *gate*, wakavunja mlango wa nyumba, wakaingia ndani na kuharibu mali nyingi za umma na zake mwenyewe.

Pili, walikwenda kwenye jengo la *annex* ya *Hall 4* wanapoishi Viongozi wa *DARUSO* yaani Viongozi wa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wakajaribu kuchoma moto jengo hilo bila kufanikiwa.

Tatu, walivamia bweni au *Hall 7* la wasichana, wakavunja vyumba vya wasichana 21, wakawateka nyara wasichana waliokuwepo na kuwapeleka moja kwa moja wanachuo hao katika eneo la *swimming pool* na kuwalazimisha kuogelea. Katika vurugu hizo mwanafunzi mmoja aliyekuwa anafanya vurugu Ndugu Deogratius Dominic alizama na kufa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi hao pia walivamia kantini ya chuo wakanywa pombe na vinywaji vya kila aina vilivyokuwemo humo na vingine wakavichukua mabwenini kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya vurugu hizo Kamati ya Wakuu wa Vitivo na Wakurugenzi wa Taasisi za Chuo Kikuu iliitishwa ili kujadili tatizo hilo.

Kutokana na athari mbaya na matokeo ya vurugu hizo Jumatatu tarehe 25/2/2008 Kamati ya Utendaji ya Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam *(Executive Committee of the University Council)* ilifanya kikao cha dharura na kujadili suala hilo. Miongoni mwa maamuzi yaliyofikiwa ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, Kamati ililaani vitendo vya uvunjaji wa Sheria vilivyofanywa na makundi hayo ya wanachuo waliofanya vurugu. Kamati iliunda Tume ya Uchunguzi ili kuchunguza kiini cha vurugu zile na kubaini waliohusika katika kupanga na kutekeleza vitendo hivyo vya kihuni. Pili, kutathmini athari za vurugu hizo.

Tatu, kutoa mapendekezo ya hatua na jinsi ya kung'oa mizizi ya tabia ya kinyama miongoni mwa wanachuo.

Baada ya hapo, katika kikao chake cha kawaida cha tarehe 13 Machi, 2008, Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam lilijadili na kupitisha maamuzi yaliyotolewa na Kamati ya Utendaji ya Baraza hilo na kuagiza utekelezaji wake ukamilishwe haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Timu ya Uchunguzi iliyoundwa na Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam iliongozwa na Jaji wa Mahakama Kuu, Mheshimiwa Emilian Mushi wa Mahakama Kuu ya Tanzania. Timu hiyo ilifanya kazi vizuri sana na kuwasilisha ripoti ambayo imeelezea machafuko hayo kwa ufasaha na ufundi mkubwa. Katika ripoti hiyo wanachuo 16 (mmoja wao yule aliyefariki katika *swimming pool)*, wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam walipatikana na makosa ya jinai waliyoyatenda tarehe 17/2/2008 katika bweni la Mabibo na tarehe 22/2/2008 katika Chuo Kikuu eneo la Mlimani.

Wanachuo hao ni Gachuma Makere, mwanafunzi wa *Engineering* mwaka wa pili, Mwangata Paul Issa, mwanafunzi wa *BA* mwaka wa pili, Hilu Ernest wa mwaka wa kwanza anayefanya shahada ya Sayansi, Mwalukasa Elisha, mwanafunzi wa mwaka wa kwanza, Gastor Florence, mwanafunzi wa *Ardhi University* anayefanya shahada ya *Land Management* mwaka wa nne, Mwakolo Daniel, mwanafunzi wa Kitivo cha Sayansi ya Jamii mwaka wa pili, Muhela Geofrey, Leonard Makweta, Musali Abdulrahman, Muhako Daniel, Dominic Deogratius (ambaye alifariki katika *swimming pool)*, Silinde David, Chagulani Adams, Shirima Deogratius, Igogo Dadi na Damson Judith. Wanafunzi hawa 15 wako Polisi kwa utaratibu wa Sheria kufuata mkondo wake.

Aidha, kwa kutozingatia Sheria wanafunzi wachache wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam sasa wanafanya vurugu zaidi wakishinikiza watuhumiwa hao warudishwe chuoni kushughulikiwa kwa utaratibu wa Sheria ndogo ndogo za Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema wanachuo wote wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Vyuo vyote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania waelewe kuwa wanapotenda makosa ya jinai na kuvunja sheria za nchi wataadhibiwa kufuata hizo. Aidha, wakati Sheria ikichukua mkondo wake wanachuo hao hawataruhusiwa kurudi chuoni au kudahiliwa na Chuo Kikuu chochote. Hivyo, wanachuo hao 15 wameondolewa chuoni na wataweza kuomba wadahiliwe upya pale tu Mahakama itakapowaona kuwa hawana hatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilitoa mapendekezo kadhaa muhimu na ninaviagiza Vyuo Vikuu vyote Tanzania kuwa sheria ndogo ndogo (*students by-laws)*

zinazosimamia kusoma na kuishi kwenye vyuo vikuu zisimamiwe kwa karibu na yeyote atakayezivunja sheria hizo achukuliwe hatua mara moja.

Pili, wanachuo watakaobainika wanafanya makosa ya jinai ikiwa ni pamoja na wizi, uharibifu wa makusudi wa mali za umma au mali ya watu binafsi, unyanyasaji wa kijinsia wa wanachuo wa kike na wa jinsi hiyo ripoti itolewe Polisi mara moja na wanafunzi hao wapelekwe Polisi. Wanachuo watakaobainika kuwa wanatumia madawa ya kulevya ikiwa ni pamoja na bhangi na marijuana pia wachukuliwe hatua za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nitoe maelezo kuhusu mgombea wa urais wa *DARUSO*, Ondong Kefa Odwar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *semester* ya pili  ya kila mwaka wa masomo, chama cha wanachuo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (*Dar es Salaam University Students Organisation – DARUSO)* wanafanya uchaguzi. Nafasi zinazogombewa ni nafasi ya Rais wa wanachuo yaani Rais wa Wanafunzi, Makamu wa Rais wa Wanafunzi, Wawakilishi wa Vitivo, Wawakilishi wa Mabweni na Wanachuo wanaoishi nje ya Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa uchaguzi unasimamiwa na Kamati ya Uchaguzi ya *DARUSO*. Kamati hiyo inachaguliwa na wanachuo wenyewe  na ina mwangalizi *(observer)* kutoka Ofisi ya *Dean of Students*.

Katika uchaguzi wa mwaka huu waliojitokeza kugombea urais na kupitishwa ili waweze kugombea nafasi hiyo ni pamoja na Mwanafunzi Juma Faustine ambaye ni Mtanzania, Pasheni Mlowe ambaye ni Mtanzania na Odong Kefa Odwar ambaye ni Mganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchaguzi uliopangwa tarehe 11 Aprili, 2008 uchaguzi wa Rais haukufanyika kwa sababu wagombea urais wawili kutoka Tanzania walimlalamikia mwenzao Odong Kefa Odwar kwa kufanya kampeni chafu dhidi yao na kuwapaka matope. Malalamiko hayo yalifikishwa mbele ya Kamati ya Rufaa ya Uchaguzi ya wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo Kamati ya Rufaa ilijiuzulu ikilalamika ukosefu wa fedha za kushughulikia kazi hiyo na mambo mengine ambayo hayakuthibitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa uchaguzi, Utawala wa Chuo Kikuu huchukua fursa hiyo kuhakiki nyaraka zote za wagombea ili kujiridhisha kama wagombea wote wana sifa stahili na ni wanafunzi halali wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Katika uhakiki huo Utawala wa Chuo Kikuu uligundua kuwa uanafunzi wa Odong Kefa Odwar una kasoro kama ifuatavyo:-

Kwanza, kulingana na Sheria ya Udahili, Odong Kefa Odwar alipata udahili wa muda kwa kutoa barua kutoka katika shule yake ya Kidato cha Sita huko Entebe Uganda

na kuwa angeleta Cheti halisi kutoka Baraza la Mitihani la Uganda akirudi kutoka likizo baada ya *semester* ya kwanza.

Wanafunzi wote kutoka Uganda wanapewa udahili wa muda wakitakiwa kuleta vyeti halisi baada ya *semester* moja. Hata hivyo, rekodi za chuo zinaonyesha kwamba Odong Kefa Odwar hajaleta cheti halisi tangu apewe masharti hayo Septemba, 2006 hivyo yeye siyo mwanafunzi halisi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utawala wa Chuo uligundua kwamba Mwanafunzi Odong Kefa Odwar alighushi nyaraka za kuwa Mwanafunzi Mtanzania, akaomba apewe mkopo na kapata mkopo huo kwa udanganyifu mwaka jana. Baada ya Bodi ya Mikopo kujua taarifa hiyo akapelekwa kwenye Kamati ya Nidhamu, akakiri makosa yake na kurudisha mkopo huo. Kamati ya Nidhamu ikasikiliza maombi yake na kumhurumia kama mwanafunzi na kumruhusu aendelee kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata baada ya kubaini kasoro hiyo Utawala wa Chuo Kikuu ulimpa mwanafunzi Odong Kefa Odwar barua ya tarehe 12 Aprili, 2008 ikimtaka alete cheti halisi cha Bodi ya Mitihani ya Uganda kikionyesha ufaulu wake huo na kuwa cheti hicho kifikishwe Utawala ifikapo saa 6:00 mchana siku ya Jumatatu tarehe 14 Aprili, 2008. Aliposhindwa kuleta cheti hicho Bwana Ondong Odwar aliagizwa aondoke Chuoni hapo mpaka atakapoleta vyeti vinavyoonyesha kwamba ana sifa ya kusoma katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Aidha, kama siku 30 zitapita bila kuleta vyeti hivyo Bwana Odong Kefa Odwar atafutwa kabisa katika chuo hicho. Niongeze kusema tu kwamba leo ni siku ya 12 na Mwanachuo huyo hajaweza kuleta vyeti hivyo.

**MWENYEKITI:** Tunaomba Mheshimiwa Waziri umalizie kwa sababu muda tuliokupa sasa umekamilika. Nakupa dakika moja tu umalizie.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vurugu tangu Jumatatu tarehe 21 Aprili, 2008 zilikuwa kama ifuatavyo:-

Juzi Jumatatu tarehe 21/4/08 kama saa nne asubuhi kikundi kidogo cha wanafunzi kilianza kuzunguka madarasani, katika maktaba na sehemu nyingine wakiimba na kuitisha mgomo na kushinikiza wote waliosimamishwa masomo warudishwe shuleni. Ilipofika saa sita kikundi hicho kiliongezeka kikafikia wanafunzi 250, baadaye jioni kundi lilitawanyika na masomo yakaanza japo kwa hofu.

Jana tarehe 22 Aprili, 2008, Kamati ya Wakuu wa Vitivo na Wakurugenzi wa Taasisi za Chuo Kikuu ilikutana ili kuangalia athari za vurugu hizo. Wakati inakutana wanafunzi kama 400 walijikusanya wakazunguka jengo la Utawala la Chuo Kikuu hicho wakipiga kelele. Wakifanya vurugu na kuwachapa na kuwaondoa wanafunzi wengine madarasani, kuwachapa na kuwaondoa wanafunzi waliokuwa wanajisomea katika Maktaba, kuwachapa wanafunzi ambao walikuwa kwenye karakana mbalimbali za Chuo Kikuu na kufanya vurugu ambazo hazifai kuelezea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo Utawala wa Chuo Kikuu uliomba msaada wa Polisi ambao walikuja wakawaomba wanafunzi hao watawanyike. Wanafunzi walipokataa walijaribu kuwalazimisha kutawanyika na katika kufanya hivyo Polisi wawili walijeruhiwa, mmoja alivunjwa mguu na chupa iliyotupwa na wanafunzi hao na mwingine alikatika kwenye mguu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo wanafunzi 39 walikamatwa kwa sababu wanafunzi hao walikataa kabisa kutawanyika na kuondoka. Baraza la Chuo Kikuu ambalo lilikuwa linakutana jana usiku likatoa agizo kwamba mpaka ikifika leo saa sita mchana wanafunzi hao wawe wamerudi madarasani na hali ya Chuo iendelee kama kawaida. Na kama kuna mwanafunzi ambaye ataendelea na mgomo basi atakuwa amejifukuzisha moja kwa moja kwenye Chuo Kikuu cha Dare es Salaam.

Lakini mpaka ninazungumza sasa wanafunzi hao bado wamegoma katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na bado wanatishia hali ya amani na hali iliyopo kwenye Chuo Kikuu cha Dar es Salaam inatisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imevumilia sana na kuwavumilia sana hawa wanafunzi na haiwezi kuendelea kuruhusu kikundi cha watoto 300 wavunje amani na kuharibu maisha ya watoto 15,500 ambao wanasoma katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na sababu hiyo wanafunzi wote ambao walikamatwa jana 39 wamefutiwa udahili na wataondolewa katika Chuo Kikuu ili kuleta amani katika chuo hicho.

Pili, wanafunzi ambao wamefanya fujo leo kutwa nzima wamefutwa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na wataondolewa kwenye chuo hicho na hawataruhusiwa kudahiliwa kwenye chuo kingine cha umma hapa Tanzania.

Tatu, Baraza la Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu limeagizwa kwamba watoto wote hao ambao wameondolewa katika Chuo Kikuu wafutiwe pia mikopo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nitoe angalizo kwa wanafunzi wote wa Vyuo Vikuu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba wamekwenda kwenye Vyuo kusoma na kupata elimu na siyo kuvunja sheria za nchi au sheria ndogo ndogo za vyuo vyao. Wote watakaokaidi watachukuliwa hatua kali za kinidhamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa!

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme kwamba kama kuna hayo yote aliyoyasema Waziri mimi siungani nayo, kwa hiyo, nayalaani hasa yale yote ya udhalilishaji.

Lakini nitumie Kanuni ya 47 Fasili ya (4) ambayo ndiyo ilihalalisha hoja ya Waziri itolewe na yeye ametumia Kanuni ya 48(3).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa suala lililozungumziwa ni zito, linahusu watoto wa Taifa hili, linahusu maisha ya vijana wetu, linahusu maadili ya Taifa letu, naomba kwa fasili ya (4) sasa hoja hiyo ijadiliwe kwa muda ambao kiti chako kitaamua.

Alichofanya Waziri siyo kutoa kauli ya Serikali ambayo kwa mujibu wa Kanuni ya 49 isingeweza kujadiliwa. Kwa kuwa ametumia Kanuni ya 48, naomba Bunge lako Tukufu lipate muda wa kujadili kwa sababu maamuzi aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri ni mazito na yasipopata kuchangiwa ndani ya Bunge hili itaonekana Bunge lako Tukufu linapokea maelekezo kwani na sisi pia kutoka kwenye vyombo vya habari na taarifa mbalimbali, tuna taarifa zinazopingana na Waziri. Ninapenda lijadiliwe ili tupate uamuzi wa Bunge lako tukufu ili tujue ukweli wa suala hili uko wapi.

Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba yaliyotokea katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, lakini nina taarifa kwamba mgogoro wa aina karibu hiyo hiyo umetokea *CBE*, SAUTI Mwanza na kumekuwa na migogoro kutokana na uchaguzi. Sasa nisingependa kuwahukumu watu walio nje kwa kauli ya Serikali na kauli hiyo kwa kuwa imeletwa ndani ya Bunge. Ni lazima kauli hiyo ijadiliwe ili taratibu za kidemokrasia zipate nafasi yake kuliko kupata maelekezo ya Serikali ndani ya Bunge ambayo yangetolewa kwa njia ya Kauli nisingekuwa na sababu ya kuhoji, kwa kuwa haikutolewa kwa njia ya Kauli naomba Demokrasia itumie nafasi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakaponiruhusu nitaomba nichangie.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa umezungumza Kanuni aliyotumia Mheshimwa Waziri kwa ruhusa yangu, ni Kanuni Namba 47(4).

Mimi nimemruhusu Mheshimiwa Waziri kwa kutumia Kanuni Namba 48 fasili ya (3) (a) na (b) na fasili ya (4) na si Kanuni ya 47 fasili ya (4).

Lakini kwa kuwa umesema au umetoa hoja hiyo na mimi natumia pia Kanuni namba 48 fasili ya (4) inayosema kwamba: “Spika anaweza papo hapo kutoa uamuzi wake juu ya jambo la utaratibu lililotajwa au kuahirisha uamuzi ili afikirie zaidi jambo hilo na kutoa uamuzi baadaye na kutoa sababu za uamuzi huo kwa vyovyote atakavyoona na atakavyoamua.” Kwa hiyo, naomba suala hili uniachie na nitatoa maamuzi yangu kulingana na Kanuni hii, na sasa nitamwomba Katibu aendelee na ratiba inayofuata. Katibu!

## HOJA ZA KAMATI

### Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge baada ya kupokea taarifa ambayo niliiruhusu ambayo kulingana na Kanuni ambazonimezisoma naomba sasa tuendelee na mjadala wa hoja ambazo ziliwekwa mbele yetu leo asubuhi na nitamwita msemajiwa kwanza Mheshimiwa Mgana I. Msindai na Msemaji anayefuata Mheshimiwa Omar Shabani Kwaangw.'

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie taarifa za Kamati hizi mbili yaani *PAC* na *LAAC*.

Lakini kwa vile kauli ya Serikali imekuta mimi ndiyo nasimama kuchangia, mimi sipingani na Serikali kwa uamuzi iliyotoa lakini Waswahili wanasema: "Mwanao akichafua mkono wako huukati," basi itafutwe suluhu haya mambo yaishe.

Wale waliohusika wachukuliwe hatua za kinidhamu pale chuoni na chuo kiendelee. Mimi naomba hivyo na nina imani Wabunge wengi wanaungana na mimi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msindai naona unakwenda nje ya hoja ninaomba urudi kwenye hoja ambayo iko kwenye meza yetu hatujaiweka hoja hiyo ili ijadiliwe. Tafadhali naomba uendelee.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mimi nianze kuchangia Kamati zote mbili kwa kuwapa pongeza sana Wenyeviti wote wawili.

Nimpongeze vilevile msemaji wa Kambi ya Upinzani na wenzangu wote waliochangia. Kwa kweli hizi taarifa mbili ni muhimu sana na zitatusaidia kujua mienendo ya Halmashauri zetu na Serikali Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia kwenye taarifa ya *LAAC* pale kwenye dibaji. Taarifa hiyo nzuri sana imeandikwa kwamba Kamati ya *LAAC* ilianza mwaka 1997/1998 ikiwa na Halmashauri 111 na kipindi hicho Halmashauri 15 tu zilipata hati safi, 55 zilipata hati yenye shaka na 41 zilipata hati chafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu mimi ni miongoni mwa waanzilishi wa Kamati hii kuanzia mwaka huo, nilikuwa ndani ya Kamati hii. Kwa hiyo, mabadiliko yote yanayotokea nimepata bahati ya kuyaona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo Kamati ilikuwa inafanya kazi kwenye Kanda; wanafanya kazi Dar es Salaam wanaita Mikoa yote ya jirani, wanahama wanakwenda Arusha wanaita Mikoa ya jirani, wanakwenda Mwanza wanafanya hivyo hivyo na kazi hiyo ilikuwa inakwenda vizuri sana.  Kwa sababu walikuwa wanakagua

vitabu na pale wanapotilia shaka, wanakwenda kuona miradi yenyewe. Utaratibu huo ulikuja kufutwa baada ya miaka miwili na sababu iliyofanya utaratibu huo ufutwe ni ukosefu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea kukagua mahesabu hayo Dar es Salaam na Dodoma, sasa hivi karibu Halmashauri zote zinajitahidi sana kufanya vizuri. Mwaka jana kati ya Halmashauri 124; Halmashauri 53 zilipata Hati Safi, Halmashauri 67 zilipata Hati yenye Shaka na Halmashauri nne zilipata Hati Chafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa nilizonazo ni kwamba, mwaka huu tulionao, hakuna Halmashauri iliyopata Hati Chafu. Kwa hiyo, ni maendeleo makubwa sana kwa kazi hii tunayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunakagua vitabu, lakini kule kwenye miradi hatuendi na kama Mwenyekiti wangu alivyosema, sasa hivi tunatakiwa tufanye *value for money audit* na *performance audit,* ambayo inatulazimu kwenda kwenye maeneo husika. Pamoja na kujibana bana, tumejaribu kutembelea maeneo mengi. Mwaka jana tulitembelea Mikoa saba na mwaka huu tumetembelea Wilaya nne; mambo yanayoonekana kule *site* ni tofauti na yaliyopo kwenye vitabu. Vitabu vinaonekana vizuri, lakini miradi mingi haiendi kama inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejionea kwenye vitabu tunaambiwa Kituo cha Afya kimekamilika au darasa limekamilika, lakini tukienda huko mambo ni mabaya kabisa. Sasa ni lazima tuungane na *CAG;* yeye sasa hivi anafanya *performance audit* na *value for money.* Sasa kwa sababu yeye anafanya kazi kwa niaba ya Bunge hili; Kamati hizi zinazohusika na mahesabu haya ni lazima sasa tuanze kwenda *site*.

Vitabu wameanza kuvipanga vizuri lakini twende kushuhudia miradi yenyewe. Tumekwenda shule nyingine tunaambiwa madarasa yamekamilika, kumbe hayajakamilika na hata hospitali nyingine unakuta mambo ya ajabu sana. Kwa hiyo, hii iwe kazi yetu sisi Kamati hizi mbili, kuisaidia Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawapongeza sana Madiwani wetu, wanafanya kazi kubwa sana katika mazingira magumu, hawana usafiri na posho yao ndiyo hiyo. Sisi bado tunaiomba Serikali, iwaangalie Madiwani na iwafikirie, kwa sababu ndiyo wawakilishi wa wananchi walioko kwenye Kata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya nyingi, Madiwani hawapewi nafasi ya kwenda kutembelea miradi na hasa tukizingatia kipindi hiki. Zamani Madiwani walikuwa kwenye *Tender Board* sasa hivi hawapo na mimi ninaungana na Serikali kwamba, kazi yetu Waheshimiwa Wabunge na Madiwani, siyo kuwa kwenye *tender.* Sisi ndiyo wasimamizi wa hiyo miradi; ni lazima tupewe jukumu la kwenda kuangalia kama barabara hizo zinatengenezwa na ni kwa kiwango gani. Kuna Halmashauri nyingi sana hazifanyi hivyo. Kwa hiyo, ningeiomba Serikali itoe agizo ili hizo kazi zianze kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kule tunakotembelea bado kuna upungufu mkubwa sana wa wafanyakazi wenye sifa. Bado Halmashauri nyingi hazina Wahasibu wenye sifa. Juzi tulikwenda Kondoa, hakuna Wahasibu, Babati Wahasibu hawatoshi. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali iendelee kusaidia ili Wahasibu hao wapatikane kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna watumishi wanakaa katika Kituo kimoja zaidi ya miaka kumi; wapo tumewakuta Manispaa ya Iringa, Wilaya ya Hai na Halmashauri nyingi sana. Sasa hebu Serikali ipitie, iangalie mtumishi anapokaa mahali zaidi ya miaka kumi; unafikiria atakuwa anafanya nini? Amekwisha kuanzisha miradi yake, anafanya kazi kwa mazoea na hao ndiyo akipelekwa Mkurugenzi mpya, wanawaambia kwamba walishapita wenzio kumi, mimi nipo hapa hapa na wewe ni wa kupita tu! Kwa hiyo, hilo tuliangalie sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi fedha nyingi sana zinakwenda kwenye Halmashauri zetu, ukarabati wa zahanati wanatengewa shilingi milioni 14, Kituo cha Afya wanatengewa zaidi ya shilingi milioni 20, lakini ukienda kuangalia kazi zinazofanyika pale ni za ajabu sana. Bado Halmashauri zetu zinawapa kazi Makandarasi wasio na sifa na ndiyo maana zahanati, madarasa yetu, Vituo vya Afya na barabara vinatengenezwa chini ya kiwango kinachotakiwa. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali ihakikishe inawapeleka watumishi wenye sifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaziambia Halmashauri zetu zitengeneze *by-laws* ili ziweze kujipatia mapato ya kutosha. Mpaka ninavyozungumza, hivi sasa kuna *by-laws* nyingi sana zipo Ofisi ya Waziri Mkuu, hazijatiwa saini zirudi zikafanye kazi huko. Kwa hiyo, ninamwomba Waziri wa TAMISEMI, washauriane na Waziri Mkuu ili wamalize hilo tatizo. *By-laws* nyingine zimekaa zaidi ya mwaka, kwa hiyo, tunazinyima nafasi hizo Halmashauri kukusanya mapato yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na vilevile bado kuna Halmashauri nyingi hazina Hospitali za Wilaya. Tunaiomba Serikali iangalie, kwa mfano, Halmashauri ya Misungwi mpaka leo haina Hospitali ya Wilaya na ujenzi wa hiyo hospitali hauendi kama unavyotakiwa. Kwa hiyo, ninaiomba sana Serikali isaidie katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie waliyosema wenzangu; ni makosa makubwa kuiadhibu Halmashauri kutokana na utendaji mbovu wa Mkurugenzi, Mweka Hazina au Mkuu yeyote wa Idara. Kuna Halmashauri zipo hazina *Internal Auditor* amehamishwa na Serikali, lakini wale wakaguzi wakienda wanawanyima fedha kwa sababu hawana *Internal Auditor.* Kwa hiyo, ningeomba hayo makosa yasahihishwe, wananchi wasiadhibiwe kwa makosa yanayofanywa na viongozi wabovu.

Vilevile watendaji hata Wakurugenzi, hivi karibuni tumeajiri Wakurugenzi wengi sana na wengi hawana sifa. Hebu tupitie tuwaangalie ili wale wenye sifa wabakie na wale ambao hawana sifa, wapelekwe katika maeneo mengine wafanye kazi nyingine siyo za Ukurugenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa kuligusia ni Mtendaji wa Halmashauri, anaharibu kabisa katika Halmashauri A badala ya kuchukuliwa hatua pale, anahamishwa anapelekwa kwenye Halmashauri nyingine. Hivyo ni vitendo ambavyo haviwezi kuvumilika, kwa sababu hapo ameharibu hata akipelekwa kwenye Halmashauri nyingine ataharibu tena. Sasa tutaendelea na hali hiyo mpaka lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni uhamishaji wa matumizi ya fedha ambazo zimekisiwa na Halmashauri; hairuhusiwi kuhamisha fedha kienyeji kuna utaratibu wake. Sasa hivi tumekuwa na hiyo kasi ya kujenga shule za sekondari, kuna fedha zimehamishwa kienyeji badala ya kutengeneza mradi unaohusika zinaenda kujenga shule za sekondari bila kufuata utaratibu uliowekwa. Tunasema Bunge likishaidhinisha fedha, hebu kule wanaohusika waende na hilo. Kama wanaona kwamba mwaka husika, wao wanataka kujenga shule ya sekondari tu si walete hayo maombi. Mtu anahamisha fedha za maji zinakwenda kujenga shule za sekondari, anahamisha hela za hospitali zinakwenda kufanya kazi ya maji! Kwa kweli kwa kufanya hivyo hatutafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme shule za msingi na za sekondari tumejenga nyingi, lakini walimu hakuna. Tunaona nia ya Serikali kwa kweli wanajitahidi, lakini ijitahidi zaidi ili wanafunzi wetu wapate elimu inayostahili. Vilevile, sasa tujitahidi kujenga nyumba za walimu; walimu wengi wanapangiwa shule, wakienda huko hakuna nyumba wanarudi walikotoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna tatizo la walimu na watumishi wengine, kufuata mishahara Wilayani, wanapofuata hiyo mishahara wanatumia fedha zao na hawarudishiwi.

*(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge hiyo ni kengele ya pili.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimwia Mwenyekiti, ninaunga mkono Taarifa hizi mbili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mgana Msindai, ninakushukuru. Ninaomba nimwite Mheshimiwa Omar Kwaangw' na Mheshimiwa Fatma Fereji, ninafikiri atakuwa msemaji wetu wa mwisho.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nitumie nafasi hii, kukushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nichangie kwenye taarifa hizi mbili; Kamati ya Hesabu za Serikali na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Vilevile niwapongeze Wenyeviti; Mheshimiwa John Momose Cheyo na Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, kwa kuleta taarifa zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa za Kamati hizi ni muhimu sana, lakini muda tunaopewa hapa Bungeni kuzijadili na sasa hivi umesema Mheshimiwa Fatma Fereji ni msemaji wetu wa mwisho; ni mdogo mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya Bunge ni kuisimamia na kuishauri Serikali. Sasa kama kazi hiyo ya kuisimamia na kuishauri Serikali tunaifanya kwa saa chache tu (saa mbili tu); hivi tutawezaje kuisimamia na kuishauri Serikali hii vizuri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jambo hili ni lazima tulione sisi Waheshimiwa Wabunge kwenye Kanuni zetu. Lazima Taarifa za Kamati, zipate muda wa kutosha wa kujadiliwa. Kamati moja itoe taarifa yake, Waheshimiwa Wabunge waijadili kama ni siku nzima au hata siku mbili, tujue mambo yote yanayotendeka ndani ya Serikali na hakuna namna ya kujua mambo yaliyopo ndani ya Serikali kama hatutapata muda na kama kazi hizo hazifanywi na Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitaka kwanza nitoe hilo angalizo ili mwelekeo wa *CAG* (Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali), kwa sasa unaelekea kwenye *performance audit.* Sasa kama mwelekeo ni huo, kwenye *performance audit,* yaani ukaguzi ambao unaleta ufanisi au ukaguzi wa ufanisi ni lazima Kamati ziende zikaone shughuli hizo ili ule ufanisi uonekane kule. Tumeambiwa hapa asubuhi kwenye taarifa, wenzetu waliopo Uingereza, Denmark huko wanachofanya asilimia 95 ya kazi za Kamati zinafanywa kwa kwenda kuona huko *value for money*. Sasa Kamati za Bunge za nchi yetu kwa nini zisipewe muda wa kutosha? Zipewe muda wa kutosha kwenda kuona na kujadili ili wananchi wapate taarifa kamili na mimi nina uhakika, wananchi leo wangependa kupata taarifa za kutosha juu ya maelezo ya taarifa hizi mbili, lakini kwa sababu muda ni mfupi basi haiwezekani. Kwa hiyo, ninaomba wakati ujao, jambo hili lirekebishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapata tabu sana kwenye vigezo, ambavyo anatumia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa sababu hii inayosema Hati Safi au inayoridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako, niseme maoni machache ambayo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliyoonyesha kwenye vitabu. Kwenye hati inayoridhisha alisema hivi na nitasoma machache tu; ameonyesha maoni yake kwenye baadhi ya Halmashauri zetu amesema: "Udhaifu katika utoaji kazi za ujenzi wa barabara huyo amepata Hati Inayoridhisha. Ucheleweshaji katika ukamilishaji wa miradi ya barabara huyo amepata Hati Safi. Udhaifu katika usimamizi wa miradi huyo amepata Hati Safi. Kutokutumia fedha za maendeleo na wengine karibu milioni 500 inaonekana wapo kwenye Hati Safi au inayoridhisha au walioshindwa kutumia fedha za ruzuku zaidi kabisa ya shilingi milioni 600 hao nao wapo kwenye Hati Inayoridhisha. Malipo katika Mikataba yenye shaka wapo katika Hati Inayoridhisha. Bakaa isiyotumika zaidi ya shilingi milioni 500 wapo kwenye eneo la Hati Inayoridhisha. Salio kwenye benki ambayo imeonyesha upungufu zaidi ya shilingi milioni 900 kwenye Halmashauri nyingine nao wapo kwenye Halmashauri zenye Hati Nzuri. Maswali ya

ukaguzi yasiyojibiwa zaidi ya shilingi milioni 400 kwenye Halmashauri moja nimeona ipo kwenye Hati Inayoridhisha."

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninapata tabu, hata matumizi yasiyokuwa kwenye bajeti nayo Halmashauri hizo zimepata Hati Inayoridhisha. Kwa hiyo, ninapata tabu kidogo. Ninadhani hatujafikia hasa kutoa Hati Safi, kwa sababu kama tunakwenda kwenye kuangalia *performance audit*, *value for money* hatujafikia hapo, hizi Hati Safi zinatoka wapi maana bado hatujafika huko? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, angalizo langu ni hilo. Katika zile Halmashauri ambazo zimepata hati zenye shaka, tofauti na Halmashauri nyingine maana maelezo karibu ni yale yale isipokuwa kuna tofauti kidogo tu. Hao wamesema kutokuwasilisha kwa mfano, kwa vitabu vya ukaguzi, ushuru wa mabango haukukusanywa, hao wamepata hati ambayo ina shaka. Kazi zilizotolewa bila idhini hiyo nayo ipo huko huko, maduhuli yalipelekwa benki labda pungufu, matumizi yaliyozidi makisio, matumizi yenye nyaraka pungufu, hao nao wamepewa hati yenye shaka, tofauti kubwa na wale waliopata Hati Safi siioni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitaka eneo hili kwa kweli tulirekebishe tuone kabisa isemwe hali halisi na kwa sababu sasa mwelekeo ni kule ninadhani twende huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tu nitoe changamoto kidogo fedha za Serikali zinakaguliwa na nitasema baadaye kidogo hapa. Zinakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, lakini ni nani *CAG* anayekagulia fedha za wananchi, yupo wapi *CAG* wa wananchi? Wananchi wanachanga fedha nyingi sana kwenye shule, zahanati na kwenye vitu vingine, lakini *CAG* wa fedha za wananchi yupo wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo muda sasa tuanze kufikiria, lazima tuwe na mkaguzi wa nje kwenda kuangalia fedha zinazokusanywa na wananchi, maana kule vijijini kwa sasa hivi zinakaguliwa labda na watu wa Ushirika au *Internal Audit*. Mkurugenzi ndiyo anampeleka mtu wa namna hiyo kule kusipokuwa na ukaguzi ambao ni thabiti pale chini, wananchi wanachanga fedha nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili tuliangalie sana ni lazima tuwe na mtu ambaye sasa atakuwa *serious* kwenye ukaguzi wa fedha za wananchi. Maana malalamiko ni mengi sana, ukifanya ziara kwa wale ambao tunafanya ziara kule vijijini, utakuta karibu kila kijiji unaambiwa mapato ya matumizi hawajasomewa na kila mahali iko hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja niliangalia kipindi cha kipima joto kinachorushwa na *ITV,* walikuwa wamesema kwamba, viongozi ambao wanashindwa kutoa taarifa ya mapato na matumizi kwa wananchi wafanywe nini? Sikumbuki vizuri, lakini ilikuwa ni zaidi ya asilimia 90 walisema kwamba, wafilisiwe hao viongozi ambao hawatoi taarifa ya mapato na matumizi. Hii inaonyesha jinsi ambavyo wananchi walivyo

*serious* kwamba, wanataka mapato na matumizi yao yakaguliwe na wasikie taarifa ya mapato na matumizi na vilevile taarifa za fedha zao zikaguliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilidhani wakati umefika kwa Bunge hili kuona jambo hili na kama Serikali haitaki kupeleka *CAG* wa kukagua fedha za wananchi, sasa tunayo ruhusa Waheshimiwa Wabunge kutunga sheria; tutunge na sisi Sheria ili tuhakikishe kwamba, tuna watu wanaoweza kuangalia shughuli za wananchi huko chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninajaribu kuangalia ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwenye viambatanisho vya Serikali Kuu. Kwa kweli hali siyo nzuri hata kidogo. Kwenye viambatanisho nimejaribu kuangalia kidogo maana kila kitu hapa ni mabilioni, hakuna kitu ambacho kipo chini ya mabilioni. Kutorejesha masurufu shilingi bilioni 1.9, malimbikizo ya maduhuli shilingi bilioni 13.3, upotevu wa fedha shilingi bilioni 2.2, malipo yenye shaka yenyewe shilingi bilioni 67.8. *This is serious*! Ukishasema malipo yenye shaka, basi kuna mashaka ya kweli pale. Matumizi yasiyo na hati shilingi bilioni 1.2, matumizi yasiyo sahihi shilingi bilioni 36.6, malipo kwa ankra kifani shilingi bilioni 1.1, jumla karibu shilingi bilioni 124, ambazo zinatakiwa sasa ziwe *verified*, lazima itafutwe sababu kwa nini tumefika huko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiendelea mambo mengine ni magumu kidogo, ugawaji mbaya wa fedha shilingi bilioni 1.7, uhifadhi usiofaa wa nyaraka tu za barabara shilingi bilioni 5.6, ununuzi bila kufuata Kanuni za Zabuni shilingi bilioni 2 na vifaa ambavyo havikuingizwa kwenye *ledger* karibu shilingi bilioni 4.6; hapo karibu unapata shilingi bilioni 14.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna kazi ya kufanya, tunahitaji kufanya kazi kubwa sana kwenye eneo hilo, tusipoisimamia Serikali ipunguze matumizi itakuwa tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninaomba wakati wa bajeti unakuja, kuna vile vifungu ambavyo vinaelekea kwenye matatizo makubwa. Yale mafungu tunayajua sijui *fuel and equipment*, *other goods* na *services* na nini vyote hivyo tuviangalie. Serikali lazima ipunguze matumizi katika maeneo hayo. Tutatatuaje jamani matatizo ya wananchi kule, tuna matatizo ya shule kule chini? Sekondari hizo za Kata zina tabu kweli kweli; maji ni matatizo, afya ni matatizo, lakini utakuta fungu la *hospitality* linaletwa hapa likiwa na fedha nyingi sana. Wakati fulani mwaka juzi, ninadhani niliona kwenye Wizara moja wamelundika mambo mengine kwenye *hospitality*, fungu moja linaonyesha shilingi bilioni 1.8; za nini na za kazi gani? Wapunguze hivi vitu, tunapoenda kwenye ofisi za wakubwa hatuhitaji *hospitality* ya chai wala soda, sisi ni kazi tu inatosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kila ofisi inakuwa na *hospitality*, basi mwisho wa yote inafikia kwenye *billions of money*, lazima vitu hivyo tuviangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa nirudi kwenye Mkoa wangu wa Manyara, ambao umetajwa kwenye ripoti hii kwa kiwango kikubwa na kwa sababu Kamati zimefanya ziara huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, niipongeze Kamati ya *LAAC* iliyofanya ziara kule, walifanya kazi nzuri sana, sasa wameonyesha sana ambayo tungependa yarekebishwe. Kwa hiyo, ninataka niwapongeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua vilevile Kamati ya Huduma za Jamii, ilikwenda kwenye ziara Mkoa wa Manyara na mimi mwenyewe niliongoza na taarifa yake bado, nina hakika itakuja. Taarifa zote za Kamati ni vizuri viwekwe Mezani zijadiliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwenye ukurasa wa 23 wa Taarifa hii ya Mwenyekiti wa *LAAC*; suala la mafuriko kwenye Ziwa Babati. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, imekwishatoa na imechambua vizuri sana matatizo ya mafuriko kwa Mji wa Babati. Halmashauri ilikwishaomba fedha, iliomba karibu shilingi milioni 200 na sasa tena zinahitajika fedha karibu jumla ya shilingi milioni 600.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali imekwishaelekezwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwamba, kuna haja ya kuzuia mafuriko katika Mji wa Babati. Tunaomba fedha hizo zitolewe kwenye bajeti ili kazi ile ifanywe. Mafuriko ya Mji wa Babati ni mafuriko ambayo yamekuwa yakijirudia baada ya miaka fulani na sasa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ametoa ripoti kamili tofauti kabisa na ameikabidhi kwa Serikali. Tunaomba fedha hizo tuzione na tunaomba kazi ifanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru Kamati ya *LAAC* imetembelea Soko la Gallapo, iliangalia barabara ya Gallapo - Kashi iliyopo kwenye Wilaya ya Babati na kwa kweli barabara hiyo ya Mamile - Gallapo ina Makongoro, ambayo haipitiki na karibu barabara itakatika kwenye maeneo yale. Kwa hiyo, tunashauri maeneo haya yadhibitiwe na Serikali kwa kuongeza fedha kwa ajili ya Halmashauri ya Wilaya ya Babati ili maeneo haya yadhibitiwe. Vilevile barabara ambazo zilikuwepo kwenye Jimbo la Babati Mjini nazo zimepata matatizo wakati huu wa mvua. Kwa hiyo, nilikuwa ninaomba barabara ambazo zinakwenda Nakwa, barabara ambayo inakwenda Imbilili kule, barabara ambayo inakwenda Gallapo zote sasa zimeathirika kwa mvua, zinahitaji kupewa fedha za kutosha ili ziweze kufanyiwa ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninakubaliana na Kamati kwamba, Zahanati ya Gallapo ambayo kwa muda mrefu tulisema ipandishwe hadhi kuwa Kituo cha Afya, ninashukuru Kamati ya *LAAC* imeweza kuliona hilo. Tuliwahi kumpeleka Makamu wa Rais kule, tukadhani sasa tumemaliza kazi, lakini ikaonekana kwamba, bado kulikuwa kunahitajika baadhi ya mambo mengine. Sasa ninadhani zahanati ile iwe Kituo cha Afya ili malengo yale yaliyowekwa kwa ajili ya kuhudumia watu wa eneo lile, ambacho ni

Kituo cha Afya muhimu sana kwa eneo lile. Gallapo ni eneo lenye watu wengi sana na ni vizuri tuwasaidie kuipandisha hadhi zahanati hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya Magugu, eneo hili ni gumu kwa sababu hiki ni Kituo cha zamani sana na kina matatizo makubwa, sitaki hata kuyasema. Nitaomba kama kuna Mjumbe wa Kamati, akipewa nafasi aweze kuyasema, lakini Kituo hiki cha Afya hakina hata chumba cha maiti, maskini ya Mungu kuna tatizo kweli hata choo ni matatizo, mashuka kwenye wodi ni matatizo, wafanya kazi pale wapo ambao wameajiriwa na wengine hawajaajiriwa. Ninasikia kuna matatizo ambayo *LAAC* iliyaona, tunaomba yale matatizo ambayo *LAAC* iliyaona yarekebishwe pale kwenye Kituo cha Afya cha Magugu. Wapo watumishi pale wanaonekana wananyanyaswa, tatizo hili ninaomba lifuatiliwe vizuri kwa kweli lipate muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Dareda, ninakubaliana na Mheshimiwa Mwenyeiti wa *LAAC* kwamba, sasa iwe Hospitali Teule iweze kuhudumia Halmashauri ya Wilaya na ile Hospitali ya Mji Babati ambayo ndiyo Hospitali ya Wilaya sasa ibebe majukumu.

*(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi ninaomba kuunga mkono Taarifa zote mbili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Omar Kwaangw', ninakushukura sana. Waheshimiwa Wabunge, nimepewa swali hapa; kwa nini Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid amekaa karibu na Mheshimiwa John Cheyo pale kwenye nafasi za *opposition*?

Ninaomba tu niwape taarifa Waheshimiwa Wabunge kwamba, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali Kuu. Kwa hiyo, pale yupo na Mwenyekiti wake wakishauriana ni namna gani watamalizia hii hoja ambayo ipo hapa mbele yetu. Kwa hiyo, ninawaomba wale walioniandikia kuniuliza niwape hiyo taarifa rasmi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kutoa hiyo taarifa, ninaomba sasa nimwite Mheshimiwa Fatma Fereji.

**MHE. FATMA ABDULHABIB FEREJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi ya kuchangia kidogo juu ya Taarifa mbili hizi ambazo zimewasilishwa mbele yetu kuhusiana na Kamati ya Hesabu za Serikali Kuu na Hesabu za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninapenda niwapongeze Wenyeviti wa Kamati hizi mbili, pamoja na Wajumbe wote, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya wakishirikiana na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mengi ambayo yamekwishaongelewa na nisingependa kuyarudia, isipokuwa tu mengine inabidi niyarudie kwa umuhimu wake. Ila ningependa nijikite zaidi kwenye Ripoti ya *PAC*. Ningependa kwenda moja kwa moja kuanzia ukurasa wa 30 hadi ukurasa wa 32 katika *section* ambayo inaongelea juu ya Sheria ya Ununuzi wa Mali na Vifaa vya Umma na Huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana kuona kwamba, pamoja na Serikali kuwa inatueleza mara nyingi kwamba, inatoa elimu ya kutosha kwa wanaohusika na uwekaji wa fedha hizi, lakini bado kuna uvunjwaji mkubwa wa Sheria ya Ununuzi wa Mali na Vifaa vya Umma, pamoja na huduma kiasi kwamba katika kurasa hizo ukiangalia peke yake kuna shilingi bilioni 48.4; hizi ni fedha ambazo zimelipwa bila ya kutolewa bidhaa wala huduma.

Sasa unashangaa inakuwaje Bodi za Wazabuni zimo katika Taasisi za Serikali, lakini hayo mambo yanatendeka? Katika maelezo hayo hayo kuna ununuzi ambao haukuzingatia zabuni za ushindani, yenye thamani ya shilingi bilioni mbili. Hapo hapo kuna matumizi ambayo yamefanywa ya shilingi bilioni 1.3 ambayo hayakupata kabisa idhini ya Bodi ya Zabuni!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukijumlisha kwa pamoja hizo ni karibu shilingi bilioni 51.7. Inawezekana kabisa kwa baadhi ya wengine wetu wakaona ni vijisenti, lakini katika hali ya umaskini wa Watanzania na hali ngumu ya maisha waliyonayo, hizi ni fedha nyingi sana na zinatutia uchungu. Mheshimiwa Kwaangw', alipitia maelezo mengi hapa kuhusiana na Ripoti ya Mkaguzi sipendi kuyarudia, alituonyesha zile *data* na mimi ninaamini kwamba, leo ripoti hizi zingesomwa na wananchi wangesikia uchungu ulioje kwa Watanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninauliza kwa nini haya yanatokea? Serikali iko wapi na inafanya nini? Bodi za Wazabuni zimo, elimu tunaambiwa wamepewa, Wahasibu tunaambiwa wapo, kitu gani kinatokea? Katika hili ninaiomba tena Serikali ifanye jitihada za kutosha, kuimarisha *internal controls* ndani ya Taasisi zake. Tukizungumzia *internal controls* hapa, kuna mambo mengine baadhi ya Taasisi za Serikali kama ilivyo katika Halmashauri, zina Wahasibu wasiokuwa na sifa na kushindwa ku-*manage* kiwango cha fedha ambacho wanatakiwa wakitumie. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali ihakikishe kabisa kwamba, inapeleka Wahasibu wenye sifa katika Taasisi zote, kama njia moja ya kuzuia matumizi mabaya.

Vilevile tunaiomba Serikali ipeleke Wakaguzi wa Ndani, hawa ndio watakao-*ring the bells,* kama kuna kitu chochote wao ndio watakaomwona *Accountant Officer* na kumshtua. Inapofika Ripoti ya Mkaguzi Mkuu ikatujia hapa na *data* hizi za ajabu ajabu na za kutisha, wakati Watanzania wanabinywa kuchangia huduma za kijamii inasikitisha sana. Kwa hiyo, ninaomba Serikali ikazane zaidi katika kuchukua jitihada kuona kwamba, *internal controls* zinaimarishwa na hawa ambao wanahusika katika matumizi haya mabaya, wachukuliwe hatua na hili tusiwe tunaliona tena katika Ripoti za Mkaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea na hapo, ninapenda kugusia suala zima la mahusiano kati ya Ofisi ya *CAG* na Kamati za Bunge, ambazo zinachunga hesabu za *PAC*, *LAAC* na hii Kamati mpya ambayo imeundwa ya *POC*. Nitapenda ni-*quote* kidogo kifungu cha *Public Finance Act Number 6*, ambayo imerekebishwa mwaka 2004, kiko kwa kiingereza kifungu namba 31(1) ambacho kinasema: *"The Controller and Auditor General shall on behalf of the National Assembly examine, inquire into and audit the accounts submitted to him under section 25 of this Act and perform any other function which is authorised to perform by or under this Act."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja kutokana na kifungu hiki utaona kwamba, Ofisi ya *CAG* inafanya kazi kwa niaba ya Bunge. Hilo halipingiki. Sasa unapoiweka Ofisi ya *CAG* chini ya Wizara ya Fedha, ambao ni Serikali, kunakuwa kidogo na tatizo katika mgawanyo ule wa kazi na uwajibikaji mzima, kwa sababu Wizara ya Fedha naye ni mkaguliwa, kwa hiyo ni sawa sawa tu na kesi ya panya ukampelekea paka, inakuwa ni ngumu sana. Sasa tunaloomba katika hili ili Ofisi hii ya *CAG* iweze kutekeleza majukumu yake, vizuri basi ipewe uhuru wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kwamba, Ofisi hii haiwezi kuajiri wafanyakazi wake, lazima wachaguliwe, aombe ndiyo apelekewe. Kwa hiyo, haistajaabishi kuona anapelekewa watu wasiokuwa na sifa, anaweza akaambiwa hakuna. Angekuwa na uwezo kama ambavyo inatakiwa uletwe hapa Muswada unaohusiana na kuunda Sheria ile inayohusu ofisi yake, basi angekuwa na uwezo wa kuweza kuajiri watumishi ambao anawataka na vilevile kuwaondoa wale ambao wanavurunda; angekuwa kabisa na uwezo huo na ingekuwa ni jambo la busara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine katika hili inasikitisha kuona kwamba, ofisi hii ya *CAG* haiwezeshwi vya kutosha, kuweza kutekeleza majukumu yake, pamoja na jitihada inayofanyika bado kuna upungufu. Hadi hivi sasa, Wakaguzi wanaoitwa *Resident Auditors* hawana ofisi zao, wao wanakaa ndani ya Taasisi wanazokagua; hivi kweli uje kwenye nyumba yangu nikufadhili; utaweza kunitolea mabaya yangu, haiwezekani! Kwa hiyo ni kasoro na tunaiomba Serikali iione hiyo kasoro. Wakaguzi hawa wasiwe wanakaa katika Wizara ambazo wanazikagua; wanapopewa chai, kahawa na kubebewa mifuko yao, tuna wasiwasi kwamba, hawatayatoa yale ambayo yapo hasa yale ambayo ni mabaya katika Wizara hizo. Kwa hiyo, hilo ni la pili ambalo ningependa kuliongelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana, mimi ni mjumbe niliyepita wa Kamati ya *PAC*. Niishukuru Ofisi yako ya Bunge, pamoja na wafadhili, walituwezesha tukaweza kwenda kwenye mikutano, makongamano na semina mbalimbali, zinazohusiana na ufanisi wa kazi za Bunge katika uchungaji wa mahesabu. Mara nyingi tunapokwenda huko, tunapata masuala ndani ya zile semina hasa sisi Watanzania tunajikuta hatujui tuko wapi; jambo ambalo limeongelewa leo hapa na mimi ninapenda nilitilie mkazo; tunapoleta ripoti hizi basi ni lazima Serikali itupe majibu. Tunapokwenda kwenye hizo semina na mikutano huwa tunaulizwa haya kila mmoja aeleze *process* yake ya ukaguzi, inakwendaje, vipi mnachunga fedha za walipa kodi. Tunaanza kueleza halafu tunasema tunaandika ripoti tunaipeleka Bungeni, wanatuuliza

*what next*? Tunatazamana macho, kwa sababu Serikali haitujibu na wao wanasisitiza kwamba, ili Kamati hizi ambao ndio *march* ya Bunge ziweze kufanya kazi zao kwa ufanisi, basi lazima yale maoni na mapendekezo yawe *implemented*, *follow up* iwepo na tujibiwe kwamba hili ambalo mmependekeza haliwezekani kwa sababu kadha wa kadha. Kwa hiyo, tunaiomba sana Serikali, itujibu tunapoleta mapendekezo yetu inasikitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ripoti hii maoni na mapendekezo yake hayana tofauti na Ripoti ya mwaka uliopita, ambayo tuliiwasilisha hapa Bungeni. Tumelazimika kuja na yale yale maana yake nini? Maana yake ni kwamba, tunaonekana kama hatujapiga hatua, lakini kama yale ambayo tuliyaeleza yakawa yamefanyiwa marekebisho kidogo, basi tungekuwa tumekwenda hatua moja mbele na leo tungekuwa tunaeleza kitu kingine sio kile kile ambacho tumekieleza mwaka jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ninapenda kuliongelea katika hili ni uwezeshwaji wa hizi Kamati, hasa zile ambazo zinakagua miradi na zinakagua matumizi ya fedha za Serikali kwa niaba ya wananchi. Wenzangu karibu wote waliokuja hapa wamelizungumza hilo, lakini na mimi sina budi kulisisitiza. Ninasema kwa *experience* kwamba, nimekuwepo kwenye Kamati ya *PAC* mpaka juzi ambapo nimepangwa kwenye kamati nyingine, lakini mara zote tumeshindwa kwenda kufanya ukaguzi wa ndani ya *field.* Katika mikutano na semina mbalimbali ambazo tunahudhuria juu ya *financial accountability*, unaambiwa kwamba, sasa ukaguzi huu wa mahesabu ya fedha hizi upo lakini msisitizo upo kwenye kuona kitu gani kinafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Msindai ameeleza hapa, unaweza kuambiwa shule hii imejengwa kwa shilingi milioni 300, ukienda kuona ni kitu cha ajabu. Sasa angalau Kamati ya *LAAC*, ninasema angalau; wanasema wamepata kwenda angalau katika Wilaya saba kuangalia miradi. Kamati ya *PAC* haijawahi kwenda kufanya *value for momey audit* popote na hili ni sikitiko kubwa. Kwa hiyo, tunaiomba sana Serikali na ofisi yako iziwezeshe hizi Kamati ziweze kufanya majukumu yao. Kwa kweli ni kichekesho, unapokwenda kwenye mikutano ya *PAC* na Kamati hizi za *PAC*, *LAAC* pamoja na *POC* sijui kwa sababu ya umuhimu wake, lakini huwa na mikutano ya Kikanda ya Kimataifa na kila siku mnakutana kuelekezana yale tuliyosema mwaka jana mmepiga hatua gani. Sasa kila tunapokwenda pale, mnaulizwa Tanzania mmeshaanza *value for money audit,* tunasema bado. Mwaka 2005 bado, 2006 bado, 2007 bado. Inatutia aibu wajumbe wako walio kwenye Kamati ni mahodari wa kazi, Ofisi ya *CAG*, nayo inajitahidi imeanza ku-*recruit* watu kwa ajili ya kufanya *value for money audit* tunaomba sana mziweshe Kamati hizi kifedha na kiutaalam ili ziweze kufanya Ukaguzi wa ufanisi ili ziweze kuwa zimefanya kazi zake kikamilifu na ziwe zimekwenda na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Fereji, lakini wewe ni Mjumbe wa Kamati, umesahau kuunga mkono hiyo hoja, basi tunaendelea.

Waheshimiwa Wabunge, nina orodha ya wachangiaji wengine wawili kutoka upande wa Serikali, nitamwita Mheshimiwa Waziri wa Fedha, baadaye nitamwita pia Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, halafu nitarudi kwa watoa hoja ili waweze kukamilisha hoja zao. Kanuni zinatuambia wao pia ni wachangiaji wa hoja, watakuja hapa mbele kwa ajili ya kuhitimisha hoja zao.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda na mimi nichangie katika maeneo kadhaa, ambayo yamejitokeza na ambayo yanaangukia chini ya Wizara ya Fedha na Uchumi. Kwanza, ninataka nichangie katika maeneo yafuatayo: Kifungu cha 2.2, ukurasa wa 13, kwenye Ripoti ya Kamati inaonyesha kuwa, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, imeshikiliwa na Wizara ya Fedha, kama mojawapo ya Idara zake na kwamba, utaratibu huu haukubaliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchangia na kutoa ufafanuzi kwamba, Ofisi hii sio Idara ya Wizara ya Fedha ni Taasisi inayojitegemea kwa mujibu wa Sheria ya *The Public Finance Act Number 6* ya mwaka 2001, iliyorekebishwa tena mwaka 2004. Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, ina uhuru wa kufanya kazi kwa mujibu wa kifungu namba 31(1) cha Sheria hiyo ya Fedha za Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuhusu kifungu namba 2.2.3, ukurasa wa 14 kwenye Taarifa ya Kamati inaeleza kuwa, ofisi hii haina uhuru wa kuajiri watumishi wake. Kufuatana na kifungu cha 29(1) cha Sheria hiyo ya *Public Operation Act*, Ofisi ya *Controller and Auditor General* ina uhuru wa kuajiri na kusimamia watumishi wake bila kuingiliwa na ofisi nyingine yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi, wamezungumzia kuhusu ofisi kutokuwa na uhuru na Wizara ya Fedha nayo inakaguliwa, ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, katika karatasi tulizopewa leo Muswada mpya kabisa wa *National Audit Office* utawasilishwa katika kikao hiki *for first reading* na ni matumaini yetu kwamba, *second and third reading* inaweza ikafanyika wakati wa bajeti. Kwa hiyo, ningeshauri kwamba, yale yote yanayozungumzwa kuhusu ofisi hii kubanwa au namna gani, kwa sababu Muswada ule umejibu mengi ya hayo; ningeshauri kwamba ni vizuri tukasubiri *second na third reading* ya Muswada huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la bajeti kuwa finyu, kifungu namba 2.2.4, Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali, Bajeti ya Serikali kwa Wizara na Idara za Serikali, hutayarishwa kwa pamoja na Serikali nzima kwa ujumla wake, kwa kuzingatia uwezo wa mapato na vipaumbele vya matumizi. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, inapewa kipaumbele na itaendelea kuongezewa bajeti yake ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria. Kama nilivyosema, katika Muswada ambao utawasilishwa mbele yako, kuna mapendekezo mengi ya kuboresha Ofisi hii. Kwa hiyo, suala la bajeti na mambo mengine, yatakuwa *taken care of* wakati tunakuja kujadili Muswada huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la Usimamizi mbaya wa fedha katika Wizara na Idara, kama ilivyoainishwa katika ukurasa wa 20 wa Taarifa ya Kamati

kifungu namba 3.3.1 cha Taarifa ya Kamati. Wizara ya Fedha na Uchumi, imekuwa ikichukua hatua nyingi za kudhibiti matumizi ya Serikali, ambazo ni pamoja na zifuatazo: Hatua ya kwanza, tumetoa mafunzo mbalimbali kwa Wahasibu wa muda mfupi na mrefu ili kuinua hali yao kitaaluma. Wahasibu wengi wamejipatia mafunzo katika vyuo mbalimbali katika ngazi ya Stashahada, Shahada na Shahada ya Uzamili. Vyuo vingi ambavyo tunafundisha Wahasibu wetu ni Chuo cha Usimamizi wa Fedha, *Tanzania Institute of Accountancy* Arusha, Chuo cha Wahasibu Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Mzumbe pamoja na vyuo vingi vingine vya watu binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali imechukua hatua za makusudi za kuwapeleka baadhi ya Wahasibu nje ya nchi ili kupata mafunzo na uzoefu katika fani ya Uhasibu. Serikali itaendelea kuwapa mafunzo Wahasibu wake ili kuinua uwezo wao kitaaluma na kuendeleza wimbi la Hati Safi. Pili, Serikali pia imeajiri Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu za ndani wengi na itaendelea kufanya hivyo. Kwa miaka miwili mfululizo, tumekuwa tukiajiri Wahasibu lakini kila tukiajiri, tunapata maombi mapya kutoka kwenye Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; tutaendelea kuajiri mpaka tukidhi haja ya Ofisi hizo. Tatu, Serikali ina vitendo *(expenditure tracking)*, vya kufuatilia matumizi ya Serikali kwa karibu na *technical audit* kufuatilia matumizi ya miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, tuna mtandao wa *IFMS* ambao unaendelea kuimarishwa. Wizara nyingi zimeshakuwa na mtandao huu, tunategemea kwamba, katika muda ambao si mrefu, tutakuwa tumekamilisha Wizara zote. Tano, Serikali itaanzisha Idara ya Ukaguzi wa Ndani, ambayo itaendelea kudhibiti matumizi ya Wizara, Idara za Serikali na Taasisi zake. Tunakubali kwamba, kuna udhaifu katika maeneo mengi kama ilivyoelezwa na Waheshimiwa Wabunge wengi, lakini baada ya kukamilisha haya maboresho ambayo tunayafanya, tuna imani kwamba, yatapunguza baadhi ya upungufu ambao umejitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Ofisi ya *Resident Auditors* na Serikali imeshatoa ahadi kwamba, tutajenga ofisi mbili kwa kila mwaka, kutegemea na fedha itakayopatikana, lakini matumaini yetu ni kwamba, hali ya kifedha ikiwa nzuri, tutaweza kujenga ofisi hizi nyingi zaidi kuliko zilivyo hivi sasa. Kuna mambo mengine ambayo yameelezwa kuwa ni tatizo la kupata nyaraka na kadhalika, hayo tumeyapokea tutayafanyia kazi na pale ambapo inastahili, tutatoa majibu yanayotakiwa siku nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaliyojitokeza yanayohusiana na Wizara ya Fedha moja kwa moja ni hayo, ninajua yapo mengine mengi lakini katika muda ambao nimepewa, sio rahisi kuweza kuyajibu yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nitoe mchango mdogo kuhusu hoja iliyo mbele ya Bunge lako Tukufu.

Kama alivyosema Waziri wa Fedha, mambo mengi yamesemwa na ni vigumu kwa muda nilionao, kuweza kutoa majibu yote ya hoja zilizotolewa. Nina mambo machache ambayo ningependa kuyasema kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii ya Mwenyekiti wa *LAAC*, imeorodhesha mapendekezo 14. Kwa hiyo, kusema kweli ninachoweza kusema ni kwamba, tutayapitia yote na tutaona kitu gani ambacho kinaweza kufanyika ili kuondoa upungufu unaojitokeza. La jumla ambalo ninaweza kusema ni kwamba, hoja zinazotolewa na Kamati, hazipingani hata kidogo na msimamo wa Serikali kuhusu nia ya kusimamia matumizi ya fedha za Serikali. Sisi sote tungependa kuona *improvement* katika matumizi ya fedha za Serikali na *value for money*, kwa sababu kwa kufanya hivyo, tunajihakikishia kwamba, rasilimali ya Taifa inatumika kwa manufaa ya wananchi, ambao ndio walengwa wa bajeti tunayopitisha katika Bunge hili. Kwa hiyo, hakuna suala linalokinzana kwamba, labda tuna maoni yanayotofautiana, sote tuna msimamo unaofanana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda jambo moja ambalo ningependa niliseme liko kwenye hii taarifa, linahusu pendekezo la kwanza ambalo linasema wananchi wanaadhibiwa kwa sababu ya utendaji mbovu wa Watendaji katika Halmashauri na kwa sababu hiyo, wananyimwa ruzuku. Ninadhani ni hoja ambayo inahitaji kuangaliwa kwa umakini. Ninachotaka kusema ni kwamba, ruzuku ya maendeleo imewekewa vigezo na vigezo hivi si vya Watendaji peke yao, vilevile na Madiwani wana wajibu wa kusimamia. Kwa sababu *by definition,* Halmashauri ya Wilaya si wataalam peke yao wala si Madiwani peke yao ni *combination* ya wataalam na Madiwani. Kwa hiyo, kuna nafasi ya Madiwani kutenda wajibu wao na kuna nafasi ya wataalam kutenda wajibu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viko vigezo kama sita ambavyo vinatumiwa katika jambo hili. Moja ni lile lililosemwa sana, linalohusu usimamizi wa kihasibu wa fedha, ambalo ndilo linalohusu wataalam. Kigezo cha pili ni uwezo wa kifedha kwamba, Halmashauri inapotakiwa kuchangia je, inakuwa na uwezo wa kuchangia. Sasa huwezi ukasema uwezo mdogo wa Halmashauri, unatokana na udhaifu tu wa wataalam, maana hata Madiwani ambao ni wawakilishi wa umma, nao wana wajibu vilevile wa kuchangia kuona Halmashauri inakuwa na uwezo wa kifedha katika kuchangia. Vilevile kuwa na bajeti; vikao vya Halmashauri ndio vinavyopitisha bajeti, kwa hiyo, ispokuwepo bajeti unakuwa umepoteza kigezo kingine cha kupata hiyo fedha inayoitwa ruzuku.

Lipo suala la manunuzi kama ambalo limeongelewa sana na ipo michakato ya kiutendaji katika Halmashauri na vilevile utekelezaji na uwezo wa kutekeleza miradi yenyewe. Haya yote ni mambo ambayo kwa apamoja ndiyo yanaamua kama Halmashauri fulani ime-*qualify* au haiku-*qualify*, sio *issue* ya kihasibu peke yake; ni *management* kwa ujumla, pamoja na *political leadership* ya hizo *council*. Kwa hiyo, nilikuwa ninafikiria kwamba ni vizuri kulitazama hili katika upana wake, kwa sababu vigezo hivi viliwekwa ili kuziwezesha Halmashauri hizi ziwe na *condition* ambayo itazilazimisha ku-*improve,* zikinyimwa ruzuku sote tunaathirika. Sasa ninaamini kwamba, vigezo hivi vimefanya kazi nzuri tangu vilipoanzishwa kwa sababu kumekuwepo na maendeleo mazuri sana katika suala hasa lile la utunzaji wa vitabu na ufungaji wa vitabu vya hesabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ukitazama siku za nyuma huko, Halmashauri hizi zilikuwa na *problem* zaidi; nyingine zilikuwa haziwezi kufunga mahesabu kabisa na nyingine zilikuwa zinachelewa kufunga mahesabu. Tumepiga hatua kiasi, katika taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Fedha za Serikali inaonyesha kwamba, mwaka 2004/2005 kulikuwa na Halmashauri 62 zilizopata Hati Zinazoridhisha. Mwaka uliofuata zikawa 53, mwaka huu zimekuwa 100 na kwa ukaguzi wa mwaka 2006/2007, hakuna Halmashauri hata moja ambayo imepata Hati Chafu. Kwa hiyo, kumekuwepo na *improvement* ambayo imetokana na kuzibana hizi Halmashauri, kwa kutumia vigezo hivi ili kila mmoja anayejitahidi sasa anahakikisha kwamba, harudi nyuma alikotoka ambako amekuwa anakosa kupata fedha.

Kwa hiyo, pamoja na kwamba, Mheshimiwa Hamad Rashid alikuwa amesema kwamba, hii ni *collective punishment* ya kukamata mifugo baada ya kufuata nyayo, lakini ninadhani hii ni ya kistaarabu zaidi kuliko kufuata nyayo maana ina *condition* ambazo zinaeleweka. Ile kufuata nyayo wakati mwingine, unaweza ukakamata mifugo kwa nyayo ambazo si za ng’ombe wale ambao unaowatafuta. Nilitaka nizungumzie hilo, kwa sababu limesemwa sana lakini ninataka niseme vilevile kwamba, *improvement* hii imesaidia. Sasa hivi kuanzia mwaka huu, hakuna Halmashauri itakayonyimwa ruzuku, kwa sababu zote zina-*qualify* na hiyo ni hatua nzuri sana.

Jambo lingine ambalo ningependa nilizungumzie, ambalo limezungumzwa hapa ni suala la watumishi wanaokaa kituo kimoja kwa muda mrefu sana na kwa hiyo, inaathiri ufanisi. Mimi ninakubaliana na wale wanaosema hivyo na hatua zimeanza kuchukuliwa. Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ni Madiwani, wanaotoka kule kwenye Halmashauri, wameshaona mabadiliko mengi sana yanafanyika. Hatujaimaliza kazi hiyo, lakini ninataka kuwahakikishia kwamba, tutaendelea kule ambako kuna watu wamekaa kwa miaka 25 mpaka wamekuwa wenyeji kabisa wa pale, halafu wameacha kabisa ile kazi wengine wanafanya biashara zao wenyewe, itabidi tuwaondoe katika maeneo hayo ili tuweze ku-*balance* na kuleta ufanisi zaidi katika utendaji wa Halmashauri.

Vilevile lipo suala la kwamba, kuna Wakurugenzi hawana sifa; kama kweli wapo hiyo itakuwa ni bahati mbaya. Halmashauri hizi zimepewa mamlaka ya kujadili na kuchukua hatua za kinidhamu na kuripoti pale ambapo inaonekana Mkurugenzi wa Halmashauri hajiwezi kabisa na kwamba, kupungukiwa kwa sifa kunaathiri maendeleo ya eneo hilo. Kwa hiyo, hatuwezi kubaki tunalinda maslahi ya mtu badala ya kulinda maslahi ya wananchi. Tukipata taarifa za namna hiyo, tutachukua hatua zinazostahili.

Ile habari ya kusema kwamba, watendaji wanahamishwa kutoka Halmashauri moja kwenda nyingine, jamani wakati mwingine usifanye *decision blanket* kabisa. Tunayo mifano mizuri tu ya Halmashauri na Watendaji ambao wana mgogoro na Mwenyekiti tu. Wakati mwingine, Mwenyekiti ana *interests* zake, sasa ana-*impose* zile *interests* kwa *management* na *management* ikikataa inakuwa *problem.* Sasa huyu huwezi kumwadhibu kwa sababu ya mahusiano yake tu na mwingine, inabidi umtoe hapo kwa

sababu sio kila atakakokwenda atakuwa na uhusiano mbaya. Kama kweli ame-*mess-up* na utendaji wake kweli ni mbovu, sasa hapo tunamwajibisha pale pale.

Lakini kama ni mambo ya uhusiano tu wewe unataka *tender* na yeye amekataa, halafu unasema sasa tusimpeleke popote, watakosa wa kupata Wakurugenzi. Kwa hiyo, ninafikiri ni vizuri tusiwe tunawaadhibu wasiostahili kuadhibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la fedha zilizokwenda katika Shule na kusema ya kwamba, vigezo vinavyotakiwa havikufikiwa; tutaendelea kulishughulikia kwa kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Elimu ili tuwe na uhakika kwamba, kweli tunapata fedha zinazolingana na mahitaji. Tumebadilisha kidogo viwango vinavyokwenda katika shule katika ujenzi wa madarasa na nyumba za walimu kwa ajili ya kuzingatia hali halisi iliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninadhani niseme tu kwamba, tutafanya kila jitihada zilizo katika uwezo wetu, kuhakikisha kwamba, haya yote ambayo umeyasema humu, tutayasoma tena kuangalia ni kitu gani kinawezekana na kile ambacho hakiwezekani, tutasema hiki kilishindikana. Kile kilichoshindikana huwa kina sababu, maana mambo haya ni mengi na yanagusa haki za watu, kwa hiyo, huwezi kufanya bila kuwa na uangalifu wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninadhani niseme ya kwamba, ninaunga mkono hoja na ninaahidi kuzingatia haya tuliyoyasema na kila linalowezekana litachukuliwa. Hivi sasa tunachukua hatua katika *issue* ya *value for money.* Tunaiimarisha TAMISEMI ili iwe inafanya kazi ya kufika kule kwenye miradi. Ninaamini, kupata Hati Safi ni hatua moja, lakini tungependa kupata Hati Safi ya utekelezaji wa miradi *on the ground.* Hiyo ndiyo itakayotuhakikishia kwamba, maendeleo ya wananchi kweli yanakwenda kama yalivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninaomba nitoe tu mwongozo wa kuhitimisha hoja zetu, ambazo wachangiaji wote tumemaliza kuwasikiliza. Hoja ambazo zipo mbele yetu ni mbili, ambazo zinahusu Kamati mbili tofauti. Sasa tunapofikia hatua ya kuridhia na kuzipitisha katika Bunge hili, itabidi tuziamue moja baada ya nyingine. Kwa hiyo, utaratibu utakuwa kama ifuatavyo:-

Nitamwita kwanza Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali, yeye nitampa nusu saa atatoa maelezo ya yale yaliyozingatiwa katika hoja yake na baada ya hapo, tutaiamua hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali. Halafu nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa na yeye vilevile tutafanya kama nilivyoeleza. Kwa hiyo, baada ya utaratibu huo nilioueleza, ninaomba sasa nimwite Mheshimiwa Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali ili aweze kuhitimisha hoja yake na Bunge lipate muda wa kuiamua hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati karibu.

**MHE. JOHN M. CHEYO – MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuhitimisha hoja ambayo tumeweka leo asubuhi mbele yako. Kama ilivyo kawaida, ninaomba nitumie nafasi hii kwanza, kuwatambua wale wote ambao wamechangia hoja hii na labda kumpunguzia mzigo mwenzangu, ningewataja tu wote kwa sababu baadhi yao wamechangia hoja zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla waliochangia ni watu 14, wakiwemo Mawaziri wawili, ambao wamehitimisha. Waliochangia kwa njia ya kuzungumza ni Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed - Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa *PAC*, Mheshimiwa Estherina J. Kilasi, ambaye alikuwa Makamu Mwenyekiti wa *PAC,* Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji na Mawaziri wawili; Mheshimiwa Mustapha H. Mkulo, Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Stephen M. Wassira, Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa njia ya maandishi ni Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Sevelina S. Mwijage, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Magadalena H. Sakaya na Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme moja ambalo ninaona ni jambo ambalo linafurahisha. Nilipotoa hotuba yangu kwa mambo ya fedha nilisema, hakuna itikadi hapa; itikadi ni moja tu, fedha ya Serikali itumiwe vizuri na hili limeonekana kabisa katika majadiliano tangu asubuhi na mchana wa leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, amesisitiza mambo yafuatayo: Kwanza, Serikali itekeleze mapendekezo ya Kamati. Nilifikiri kwamba, Mheshimiwa Mkulo alipokuwa anachangia, angejibu ile hoja yangu pili kwamba, hatupati majibu, tangu mwaka jana tulileta hapa mapendekezo lakini yeye ni Mhasibu, anajua kabisa utaratibu wa Serikali kwamba, baada ya sisi kuleta mapendekezo hapa, ndiyo maana kwa makusudi nikazungumzia juu ya *accountability loop,* yaani mzunguko wa *accountability* kwamba ni lazima imalizike na jibu kutoka Serikalini.

Kwa hiyo, hakulizungumza hili, lakini nikimwangalia ninadhani anaridhika na mimi kwamba, atafanya sasa ili kama alivyosema Mheshimiwa Fereji, tunaposafiri nchi mbalimbali, tunazungumzia juu ya *best practice*. Njia nzuri za kuweza kuangalia Mahesabu ya Serikali na hii ni mojawapo. Je, ninyi mnapotoa mapendekezo Serikali inasema nini? Kwa hiyo, ninashauri huo uwe utaratibu wa Bunge letu na sisi tukienda kule tujivune kwamba, Serikali yetu inasikia. Kwa hiyo na hili pia limezungumzwa kwa msisitizo sana na Mheshimiwa Kilasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed pia amezungumza *specifically,* juu ya *issue* ya *TANSORT,* ambayo walileta ripoti yao na walienda Uingereza, hatujapata jibu lolote. Kwa hiyo, ninasisitiza tena hapa, mapendekezo ambayo yameandikwa na Kamati yaletwe. Amezungumzia pia juu ya Mwanachi Meremeta na Alex Stewart na amehoji kwamba, mbona hii hajaiona katika Ripoti ya *CAG.* Ukweli ni kwamba, mambo haya ya Meremeta na Alex Stewart, yote yalilipwa kwa kupitia *Bank of Tanzania*. Kwa hiyo ni matumaini yetu, kama kuna *queries* zozote labda tutaziona *queries* hizo kutokana na Ripoti kwenye *POC* ya Benki. Tutaendelea kufuatili ili tuhakikisha kwamba, kama kuna *queries* zozote ziweze zikapatikana. Jambo la *TANSORT* tumeshalizungumza na lipo pia kwenye hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya 2005/2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hati sahihi za malipo, ndio udhaifu ambao tumeusema kwamba, wewe unakuwa na hati ambayo si sahihi za shilingi bilioni 36 na shilingi bilioni 17 zote zinakuwa katika upande mmoja tu wa Wizara moja. Hii ni dosari na kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, ndio msisitizo wa Kamati na tumeuona. Ninataka kurudia hapa, baada ya kuangalia hizi hoja baadae ukija kuziangalia nyingine, nyaraka zimeshapatikana. Sasa ndiyo kusema, Maafisa Wahasibu wanangoja kutengeneza hoja ili waje wajibu hoja; hili halikubaliki, zuia hoja kwa sababu kitabu hiki cha *CAG* ndiyo kinatembea ulimwenguni kote. Kwa hiyo, watu wanapoona *figures* kubwa kubwa wanatuharibia. Ninasikitika Maafisa Wahasibu hawapo hapa, lakini Mawaziri wapo; msisitize watu wazuie hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lipewe uwezo wa kibajeti ili liweze kufanya kazi yake na hili jambo limechangiwa na watu wengi sana. Sisi kama *PAC,* hatukuweza kutembelea mahali popote, hii ni kweli kwa sababu nikiwa Kiongozi wa Kamati hii, nilikuwa siwezi kuelewa kwamba, ninaenda kukagua Wizara ya Maji halafu niende kule niwaambie hebu nipeni hela nikakugue. Hii haiji kichwani. Kwa hiyo, ndiyo maana tunasema tunataka Bunge liwezeshwe na ndiyo maana tumesisitiza kwamba, leteni Muswada wetu wa *National Assembly Fund,* tupate *Fund* nyingi zaidi ili tusiweze tena kuingia katika mambo ambayo hayako sawa sawa; yule unayemkagua ndiyo unaenda kumwomba akupatie fedha ya kwenda kulala na nini! Hii haiendi, kwa hiyo, ndiyo maana hatujatembelea, tumeamua kukaa tu ofisini na sana sana tumeenda Muhimbili na *MSD* kuangalia dawa basi, kwa sababu hatuwezi ku-*compromise;* hiyo ndiyo sababu ya Kamati yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri pia ametusihi kwamba, tusikubali tu kwamba hakuna wataalam na mimi ninakubaliana naye; Wataalam wa Tanzania wapo wengi sana, tatizo ni *attitude of the minds,* lazima tugeuze *minds* za watu wetu. Ukipewa kazi, fanya kwa ufanisi, wahasibu wapo kibao na ninajua Waziri amesema amewapeleka shule. Utapeleka watu shule na shule na mafunzo na mafunzo, lakini kama hawaamini uadilifu ndiyo sifa ya kuwa mtumishi wa mzuri, haitaweza kufika mahali popote. Kwa hiyo, hapa tunachotaka kusema, mtumie wataalam mlionao lakini kwa wale waadilifu.

Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, amezungumzia juu ya *Public Audit Act*; nimefurahishwa na majibu ya Waziri, pamoja na kwamba, tumepata *first reading* sawasawa, tunalifanya; lina mwelewekeo ambao tunautaka na ningeshauri Wizara ya Fedha sasa ifanye juhudi kuhakikisha kwamba, Muswada upo tayari kwa ajili ya majadiliano kabla ya Bajeti ya 2008/2009, kama Mheshimiwa Waziri alivyoahidi.

Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, pia amezungumzia *double accounting*; hili jambo limeelezwa vizuri na tumezungumza mara nyingi pia kwamba, tunamsurubu *RAS* kwa matatizo ya *DED.* Hakuna sababu na ninaona hiki ni kitu ambacho, ofisi zinatakiwa ziangilie zitafanya namna gani ili fedha ambazo tunazihoji kwenye *PAC,* zisiwe ni zile ambazo zinahojiwa na upande wa *LAAC.* Amezungumza pia kuhusu fedha za Wafadhili; ni kweli tumeona katika vitabu mwaka hadi hadi, kila ukiangalia fedha ambazo zimeahidiwa kwa mfano, fedha kutoka nje, miaka mitatu ukiona kwenye ripoti ni *zero*.

Sasa tunamuuliza *RAS;* kwa nini wewe unakubali Bajeti ya namna hii, kila siku *zero* hakuna ulichopata na hii ukiangalia katika *broader term* unaona kwamba, ile Bajeti ambayo tunaileta Bungeni si Bajeti halisi ni kama vile tunakuja kuwahadaa Watanzania; mwaka huu nitatumia trilioni na Waziri wa Fedha anajivuna hapa kumbe hewa baadhi ya fedha mnazotuambia? Sisi tunaunga mkono kabisa kwamba, ule mtindo wa sasa wa *GDS* ni mzuri, kwa sababu fedha inakuja Hazina. Kwa hiyo, unapokuja kuliambia Bunge kwamba, fedha za nje zitakuwa kiasi kadhaa na zitakuja, kweli hizo fedha zinafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid amesema pia tuanze njia ya kujtegemea, kila siku bajeti yetu ni tegemezi mwaka hadi mwaka ni miaka mingapi arobaini au sitini, mia moja au *for how long?* Kwa hiyo, hii ni changamoto kubwa sana kwa Wizara ya Fedha, inapaswa kutafuta njia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Estherina Kilasi, ambaye alikuwa Makamu wangu; mambo yake karibu yale yale ambayo tumezungumza kwenye Ripoti, lakini amesisitiza sana Serikali ijali. Tulisikitika asubuhi kwamba, tunazungumza juu ya utendaji wa Serikali, juu ya fedha ambazo bajeti yake inakuja kuombwa na mara nyingine, mtu anapiga magoti ya maji nisaidieni nipate fedha hizi nikatekeleze a, b, c. Leo tunakuja kuzungumza jinsi ulivyotekeleza na hiyo Bajeti haipo, maana yake nini? Kwa hiyo, tumekuja hapa Serikali labda watu wawili au watatu tu na Wizara ya Fedha alikuwa ni mtu mmoja tu, lakini hakuwa *Pay Master General;* hajajua kwamba, anazungumza na *CAG Office*. *Pay Master General*, ambaye ndiyo mlipaji Mkuu wa Serikali, ndiye anawajibika Kikatiba kuangalia matumizi ya fedha hizi na yeye ndiyo anatoa barua za watu ambao ni Maafisa Wahasibu na kufuatana na Sheria inasema, *they are personal responsible;* yeye yuko wapi; nani ambaye amesikia mambo ambayo tunazungumza hapa na wala sijamwona kuripoti hapa?

Kwa hiyo, ninachotaka kusisitiza kama alivyosema Mheshimiwa Kilasi tushirikiane, Serikali pamoja na Kamati. Tumesema mwaka jana, Mheshimiwa Rais ameshirikiana na Kamati na ndiyo maana, umeona katika upande wa *LAAC,* asilimia 100, lakini bado tuna asilimia 26 na ya mabilioni kwa upande wa Serikali Kuu, ambayo bado

haijafikia kiwango. Sasa tushirikiane hili ni jambo letu sote; Kamati, yaani Bunge, pamoja na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mara nyingine tutakuwa tunawaita hawa Mawaziri tunapokaa na hawa Maafisa Wahasibu, wawe wanaona tunawahoji kitu gani ni jambo zuri sana. Ame-*insist* kuhusu *tresury note*, ambayo tayari nimesha-*recover*. Aidha, majibu ya *CAG* yawe kigezo cha Bajeti, mnapotuomba hapa mimi ninasema *sector committees* ziangalie *perfomance* yako, ilikuwa ni namna gani ndiyo zikupatie fedha. Tunakupa fedha halafu huzitumii vizuri, hakuna sababu ya wewe kama Wizara, upate hizo fedha. Mimi ninakubaliana na jambo hilo kabisa. Amesisitiza juu ya Ripoti ya *TANSORT* na sisi tutaendelea kuifuatilia.

Kamati ziwe na meno, hili ni kweli na ndiyo maana kwenye Ripoti yetu nimesema, sisi tunapendekeza tu pawepo na tozo ya asilimia kumi, lakini ukiangalia mshahara wa unayemwambia, haujafanana na mabilioni ambayo aidha amepoteza au ametumia vibaya katika akaunti yake. Sisi tumesema hapa kwamba, haya mambo kwa nini yule mtu asiwe *demoted* hata kama ukiwa *Principal Secretary*, kuna ubaya gani kuondolewa kama wewe kila mwaka hupati Hati Safi, kwani si kuna Watanzania kibao ambao wanangojea hiyo kazi? Kwa hiyo, ninachosema kwa sababu sisi tunapitia kwa Waziri wa Fedha, ninaomba Waziri wa Fedha awe mkali, kwa njia hiyo hiyo ambayo sisi tunajiribu kuonyesha kama Bunge kwamba, hatupendezewi na hali halisi iliyopo.

Wajumbe wawe wa kudumu; hili ni jambo ambalo tutalizungumza kwenye Bunge, maana kwa kusema kila baada ya miaka miwili kufundisha ni kazi kubwa sana na hiki ni kigezo kimojawapo, tunapokwenda kwenye mataifa wanatuuliza; je, ninyi Kamati yenu inakaa kwa muda gani; unasema kila baada ya miaka miwili na nusu; ni bahati nasibu kama utawarudisha tena au vipi. Hawa Wajumbe ni lazima uwa-*train* na mambo kama hayo. Naye pia ameunga mkono suala la *National Assembly Fund,* ambayo ninakushukuru sana.

Suala la Mheshimiwa Mgana I. Msindai, ninamwachia Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa alijibu, lakini ninaunga naye mkono juu ya Maafisa Wahasibu, ambao wameharibu Mtwara unawahamisha unawapeleka Mwanza na kule wanapata Hati Chafu; unamwondoa tena kule unampeleka Kigoma na huko anapata Hati Chafu; sasa mtu ana Hati Chafu kila mahali kwa nini unamhamisha? Anachafua hapa na pale, ndiyo kitu ambacho tunasema kwamba, wale wanaochafua mahali, wakiondoka wasiingie tena kuwa Maafisa Wahasibu, waende moja kwa moja kule mnapotaka kuwapeleka.

Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', ninashukuru sana kwa pongezi, lakini umesema ni muhimu Kamati kama hizi, zikapewa muda zaidi ndani ya Bunge. Watu wengi wangeweza kuchangia lakini wameshindwa kwa sababu ya muda. Hapa ninataka kusisitiza Sheria inasema; *The Controller and Auditor General* anafanya hii kazi kwa niaba ya Bunge, kwa hiyo, *CAG Report* ni Ripoti ya Bunge. Ninapenda Waheshimiwa Wabunge wote, mchangamkie hii Ripoti. Mnapokuja hapa, kama kuna kitu ambacho unaweza ukazungumzia ukirudi kule kwenye Jimbo lako, unasema kwamba, alikuwa mkali sana juu ya matumizi mabaya ya fedha. Kama kulikuwa na watu wanaangalia

hapa, wanakuuliza ulikuwa mkali na wakiangalia viti vyote hivi hakuna mtu; sasa wanasema wewe bwana ulichangia wapi? *(Makofi)*

Kwa hiyo, Ripoti ya *CAG* ni ya Bunge. Ninaomba hili tulichangamkie sana na ikiwezekana, tupewe muda zaidi. Ni kweli sasa tunaenda na majukumu makubwa zaidi ya *value for money* na *performance audit.* Umezungumza juu ya *performance audit* iliyofanywa juu ya mafuriko, ndiyo mwelekeo huo na dunia nzima inataka kuondokana na kuangalia makaratasi tu kwenye meza; Wabunge waangalie na wafanye *research* kuona kama fedha zetu zilitumika vizuri hapa.

Hii ndiyo *trust* ya ulimwengu sasa na ndiyo maana Mheshimiwa Mkulo amesema kuwa, *tracking record* hata Wafadhili wanaanza kumuuliza *where is your system* ya kufuatilia hizi fedha tulizotoa kama kweli zimefanya kazi ambayo ulitaka ifanyike? Mimi ninaona tulichangamkie hili sote, Wabunge wachangamke wawe ndiyo *assessor* wa *value for money* na *CAG* aimarishwe afanye hiyo shughuli vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Fatma Fereji, naye amezungumza mengi na alikuwa kwenye Kamati na kusema kweli, anayaelewa vizuri sana. Sheria ya Manunuzi ifuatwe, *queries* zimo katika Ripoti yangu *is really a shame*. Wewe unawapa watu shilingi bilioni 1.7 kununua magari, wananunua magari mawili ya shilingi milioni 254; shilingi bilioni 1.4 nyingine hakuna maelezo ambayo yanatosheleza! Hii siyo namna ya kutunza mahesabu yetu. Zabuni zifuatwe, hili ni jambo la maana, *internal controls* hizo ni za maana. Ofisi ya *CAG* inamkagua mtu na kila siku wanakunywa naye chai; siku nyingine unasema ukimwangalia nyani usoni hutamuua, ninyi mnafahamu! Kwa hiyo, haya mambo nayo hayafai ni vizuri na hapa Waziri amezungumza kwamba, ataongeza ujenzi wa nyumba nyingi za Maofisa, ninadhani hili ni jambo jema.

Mheshimiwa Fatma Fereji pia amesisitiza juu ya kujibu hoja na hilo nimeshalielezea vizuri. Uwezeshaji wa Kamati, nalo nimelizungumza vizuri. Mheshimiwa Lazaro Nyalandu naye amezungumza zaidi kuhusu *GBS;* kwamba, tuwe na uhakika wa fedha tunazopata. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Paul Kimiti kwa mchango wake wa maandishi; naye ametoa pongezi na ameomba Kamati ziwezeshwe. Wabunge ambao ni Wahasibu tunawakaribisha kwenye Kamati yetu waingie, lakini hapa hatutaki tu Uhasibu, tunataka watu ambao wataweza ku-*appreciate value.* Sio lazima uwe Mhasibu kuweza kuona kwamba, hapa kweli tumetendewa haki na fedha ambazo tumewapa hawa. Hao ndiyo Wabunge makini, wanaotaka kuona kweli fedha za walipa kodi zinafanya kazi. Hao ndio Wabunge tunaowataka kwenye Kamati na sio Wabunge wavivu, kama tuna vikao mara nyingine mpaka saa mbili usiku uwepo; kama ni kikao cha kusafiri uwe tayari na hii si kwa Kamati ya *PAC*, tunaangalia jambo ambalo ni mahususi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masomo ya muda mrefu ni kweli lakini ubaya hatuna muda, tuna siku sitini tu na hizo lazima tuangalie mahesabu yote ya mwaka mzima na tutembelee katika muda wa siku sitini; ni jambo gumu sana. Adhabu ya tozo mimi ninakubaliana na wewe kabisa; adhabu hii haifai. Ninadhani tubuni mambo makubwa zaidi. Wizara ya Fedha hapa ukiangalia Mahesabu haya, nimeyataja kwa makusudi, kuna

Wizara ukiangalia *Vote 22*, hiyo ndiyo mbaya zaidi, huwezi kupata *reconciliation.* Sasa kama Wizara ya Fedha, huwezi ku-*reconcile*, utawawajibisha vipi kwa wengine?

Tumesema juu ya Waziri Mkuu, kuna mabilioni hapa nao wachangamkie hapa. Kama hizi Wizara kubwa ambazo ndiyo viongozi zinaonyesha mambo kama hayo; je, wale wadogo wakianza tutaweza kuwadhibiti vizuri? Ninashukuru sana kwa kuweka hilo.

Mheshimiwa Lazaro Nyalandu vilevile amezungumzia juu ya uhuru wa *CAG;* ninakushukuru vigezo vya majengo ya Wabunge. Ninadhani hili Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, atalizungumzia zaidi, lakini amesema kwamba, kuna sehemu nyingine wanajengewa ghorofa kwa ajili ya Wabunge na wengine wanajengewa vibatari na nini. Ninadhani pawepo na *standard* ya kuweza kuangalia haya mambo.

Ninamshukuru sana Mheshimiwa Savelina Mwijage kwa pongezi, kama alivyosema lazima iwajibike na itusikilize. Waziri wa Fedha umesema, katika Ripoti yetu hapa kwamba, *CAG Office* ipo ofisini kwako. Mimi ninafikiri hatuwezi kubishana hapa, kuna mambo ambayo tulipendekeza *White Sand Hotel* ni afadhali yazingatiwe. Kwa mfano, pamekuwa na wakati, *CAG Office* haikukaguliwa kwa miaka miwili, kwa sababu Waziri wa Fedha alikuwa hajaamua ni nani awe Mkaguzi. Sasa kama Ofisi ya *CAG* haikaguliwi kwa miaka miwili; utasema nini kwa mataifa? Kwa hiyo ni mapendekezo mengi, ninafikiri ni vizuri tukakubali tu kama vile Sheria inavyosema, hii isogee zaidi Bungeni kuliko kukaa Wizara ya Fedha. Uhuru, kisheria na kinadharia ndiyo lakini ukweli; si sawasawa mpaka leo watumishi wa *CAG* lazima aende Utumishi na afuate mtindo huo huo wa usaili, halafu unasema huyo hapana huyo ndiyo. Ulimwenguni kote, Ofisi hii iwe *independent*. *TRA* inaajiri watu wake, haipaswi kwenda Ofisi ya Utumishi ili kwenda kupata watumishi.

Kuhusu Bajeti finyu, *again* ni wewe ndiyo unayeshirikiana nao. Sisi katika mapendekezo yetu, tungependa hii iangaliwe na taasisi ambayo ni tofauti na Wizara ya Fedha. Kwa hiyo, hayo ndiyo mambo ambayo tunafikiri yangeweza kuimarisha.

Tunashukuru kwamba, angalau Sheria inakuja na kwa hiyo ninatumai Ofisi ya Spika, itatupa hiyo Sheria tuiangalie Kamati zetu tatu zote kwa pamoja. Tunasema hivyo kwa sababu kama tukimuimarisha *CAG*, ndiyo unaliimarisha Bunge kuangalia au kusimamia shughuli za kibajeti. Kwa hiyo, tunaomba tupewe huo Muswada, tuangalie sisi Kamati zote tatu tuone kama unakidhi mahitaji ambayo tumeyataka. Ninaamini kwamba, kumekuwa na mafunzo mengi na *IFMS* nayo inafanya kazi na pia imeweka vitu mbalimbali ndani ya Ofisi, lakini bado havijatosha. Weka mguu, ninajua wewe ni Waziri na rafiki yangu mpya; *that is the area where you need to show good result*. Kwa hiyo, siwezi kukupaka mafuta hapa bado, hebu angalia zaidi utafanya nini na tena wewe ni Mhasibu, una madigrii kibao umebakisha uprofesa tu. Kwa hiyo, angalia hilo juu ya Idara hii, haijatosha hata kidogo.

Mheshimiwa Waziri, amekubali kwamba, atajenga ofisi lakini kama pakiwa na Bajeti ya *CAG*, watafanya programu wao wenyewe wajenge wapi na mambo kama hayo.

Amesema mengine atatujibu baadae na ukishasema hilo lipo ndani ya *Hansard,* basi angalia ni mambo gani ya kujibu uyajibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninataka tu kusema, mambo ambayo ni ya ujumla. Kwa hiyo, la kwanza tunachosisitiza hapa kama Kamati ni Ushirikiano kati ya Serikali na Kamati; kuthibiti na kuhakikisha kwamba, fedha za Serikali zinatumika vizuri. Ninaona hili si jambo baya; mnaonaje Waheshimiwa Wabunge, mbona hampigi makofi hili ni ombi zuri na ndicho tunachokisisitiza? Kwa hiyo, tushirikiane kwa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili la kusisitiza ni kwamba, Bunge liimarishwe, lifanye kazi yake ya kuidhibiti na kusimamia Serikali kwenye mambo ya bajeti. Kuna ubaya gani; ndiyo kazi yetu tumepewa na Katiba Ibara ya 63 na ndiyo maana tunachaguliwa na wananchi; kuna ubaya hapo Waheshimiwa Wabunge? Kwa hiyo, tunaomba jamani hili liweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu nina wito kwa wananchi; ninasema Ripoti au Taarifa ya *CAG* ni Ripoti yenu. Nimesema katika mzunguko wa *CAG Report* ni kwamba, ikishawekwa Mezani na ningeshauri kama tovuti haipo kwa *CAG*, iwekwe. Wananchi tumieni Ripoti ya *CAG* kuuliza maswali. Waandishi wa Habari tumieni Ripoti ya *CAG* kuuliza maswali na kuandika makala yenu vizuri. Makala ambayo yanaandikwa ovyo ovyo kama yalivyokuwa yanaandikwa juu ya Mheshimiwa Spika wetu, hayafai! Angalia Ripoti ya *CAG* na kama ni masurufu ya safari, Mheshimiwa Spika, hachukui hela ya kwenda nayo; Mheshimiwa Rais, hachukui hela ya kwenda nayo; Mheshimiwa Jaji Mkuu hachukui hela ya kwenda nayo; sasa kama huyu hachukui hela utamwambia kwamba Spika umechukua hela kwa vipi? Kwa hiyo, haya mambo angalieni Ripoti ya *CAG*, msitumike ovyo ovyo na sasa mambo ya ufisadi haya ndiyo matatizo tupu. *(Makofi)*

Baada ya hitimisho hilo, sasa ninaomba kutumia muda uliobaki kuliomba Bunge hili, lipitishe Azimio la kukubali Mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali, yaliyomo katika Taarifa ya Kazi ya Kamati hii ya mwaka 2006 na mwaka 2007, kuanzia ukurasa wa 34 mpaka ukurasa wa 37.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) ilipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue nafasi hii, kwanza, nikupongeze sana kwa umahiri wako katika kutoa hoja hii na kuweza kuihitimisha, baada ya kazi nzuri ambayo umeifanya mbele ya Bunge letu Tukufu na imeungwa mkono na Waheshimiwa Wabunge. Ninakupongeza sana Mwenyekiti, Wajumbe wa Kamati na Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla. Basi niombe tu kwamba, Serikali izingatie yale yote ambayo yamehitimishwa na kupitishwa na Bunge letu katika

Ripoti ya Kamati hiyo.  Baada ya kumaliza kupitisha Ripoti ya Kamati ya Hesabu za Serikali, sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, aje hapa mbele aweze kuhitimisha hoja yake na hivyo basi, Bunge lipate nafasi ya kuipitisha hoja hiyo. Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa karibu mbele tafadhali.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA - MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba na mimi nikushukuru kwa jinsi unavyoliendesha Bunge letu na kwa kunipa nafasi niweze kuhitimisha hoja ambayo tuliiwasilisha leo asubuhi katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile Mwenyekiti wa *PAC,* amekwisha kuwatambua waliochangia hoja zetu zote mbili, kwa kuwa hoja hizi ni hoja dada, ninaomba niwatambue wale waliowasilisha kwa maandishi, hoja ambazo zilikuja moja kwa moja kwangu ili na wao waweze kuona kwamba, hoja zao zimefanyiwa kazi. Wabunge hao ni pamoja na Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma na Mheshimiwa Omar S. Kwaangw'.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla, hoja zilizoletwa kwa mdomo hapa ndani ya Bunge lako, zimelenga kuiimarisha hoja tuliyoiwasilisha hapa, pamoja na mapendekezo yake. Katika ujumla wake, hoja hizi zimelenga kwenye maeneo ambayo nitayagusia na kuyatolea ufafanuzi, lakini kimsingi yapo maeneo ambayo ni ya utendaji na yapo yanayohitaji sheria zibadilishwe na ambayo yanaweza kugusa sera.  Kwa hiyo ni juu ya Serikali kuchukua yale ya kisera na kuangalia yale ambayo yanahitaji taratibu za sheria zifanyike, lakini yale ya kiutendaji, tungependa Serikali iyapokee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi, nianze tu na hoja ambayo Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Stephen Wassira amekwisha kuitolea ufafanuzi.  Hoja iliyozungumzwa sana na Wabunge wengi hapa; Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Mheshimiwa Mgana I. Msindai na hatimaye Mheshimiwa Omar S. Kwaangw'; ya wananchi wasio na hatia wasiadhibiwe kwa sababu ya Hati Chafu ambayo hawakuisababisha wao.  Ninashukuru kwamba, Mheshimiwa Waziri amesema kuanzia sasa, hakuna Halmashauri itakayonyimwa kwa sababu zote zimeingia katika utaratibu huo, zime-*qualify*. Ninashukuru sana kwa utafafanuzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameeleza vilevile kwamba, Halmashauri ni pamoja na Madiwani, ninaomba niseme tu hapa kwamba, Kamati imezingatia suala la Halmashauri; ni dhahiri Halmashauri ni Madiwani, pamoja na Watendaji, kwa pamoja.  Serikali ni vyema ikatambua kwamba, kuna majukumu yanayofanywa na Madiwani na yanayofanywa na Watendaji.  Madiwani katika mambo fulani fulani hawaingii na Serikali ikiwemo Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, imesema mara nyingi Madiwani wasiingie jikoni.  Kama ni kweli Madiwani wasiingie jikoni, basi hatuna namna nyingine isipokuwa kusema suala la kuandika vitabu si la Madiwani.  Madiwani

wasipowekewa mezani, hawawezi kusaidia. Wanaweza wakaomba, wakadai, wakafanya nini, lakini kama halikuwekwa, hawawezi wao kulazimisha wala kufanya chochote. Wanaweza wakaomba Mkurugenzi na timu yake, waandae hesabu safi, wakaulize kila mkutano, isipotekelezwa, hawana namna nyingine. Ndilo hili tunalosema kwamba, kigezo hiki kinaonea wananchi wasio na hatia na Madiwani katika hili hawana uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vigezo tunavyopigia ni pamoja na kigezo kwa mfano; kama Halmashauri haina mkaguzi wa ndani, inapoteza maksi na ina uwezo wa kunyimwa maksi hadi sasa. Madiwani hawaleti makaguzi wa ndani, analetwa na Serikali. Haya ni mambo ambayo tunatakiwa tuyazingatie; Mkurugenzi akikosekana, Halmashauri inapoteza maksi. Zipo Halmashauri zina Makaimu kwa muda mrefu, Madiwani hawawezi kulazimisha apatikane Mkurugenzi, hili ni jukumu la Serikali. Ndiyo haya tunayosema, wakinyimwa Wilaya inawafanya wananchi wasio na hatia, kukosa ruzuku bila wao wenyewe kuhusika. Kwa hiyo, ninashukuru kwamba, labda sasa kwa kuwa Wilaya zote zimeingia, tatizo hili litapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile niseme suala la Wahasibu kupelekwa kufuatana na daraja na ngazi, limezungumzwa hasa na Mheshimiwa Paul Kimiti. Ninadhani huko nyuma, tulikuwa na madaraja ya Halmashauri na watalaam wetu walikuwa wanapelekwa kufuatana na daraja la Halmashauri husika. Kwa hiyo, ninadhani Serikali iangalie tu hizo taratibu ili waweze kupelekwa wataalam wetu; awe Mkurugenzi, Afisa Mhasibu au mafisa wengine, wote wapelekwe kufuatana na daraja. Uzoefu umeshajionyesha, unafika mahali kwa mfano mahakamani, hata kesi zinakataliwa kwa sababu mhasibu hana cheti kinachotambuliwa kimahakama kwa mujibu wa sheria zetu. Sasa haya yanatuletea athari kubwa. Kwa hiyo, tungeomba Serikali ilichukulie hilo kwa uzito wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja imeletwa kuhusu manunuzi ya Halmashauri kuwa yafanyike kwa pamoja. Hoja hii imezungumzwa sana na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, Mheshimiwa Diana Chilolo na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa. Niseme tu kwa kifupi, Sheria ya Manunuzi inataka katika kila chombo cha Serikali kuwe na kitu kinachoitwa Mpango wa Manunuzi *(Procurement Plan)*. Ukitengenezwa Mpango wa Manunuzi na Serikali ikafanya mpango wa kununua kwa pamoja, tutapata manufaa makubwa, kwa sababu tutaokoa fedha nyingi za walipa kodi. Tunapoteza fedha nyingi kwa kila mtu kununua anavyotaka. Mkurugenzi yule ananunua *Nissan Patrol*, yule ananunua Toyota, huyu mwingine sijui amenunua gari la aina gani, lakini tukinunua haya magari kwa pamoja, tutapata *discount*, tutapata *benefits* za kuwa na fedha za kuleta magari ya aina moja, lakini pia na vipuri ambavyo vinaambatana nayo. Sasa hapa hatupati hiyo *benefit*. Kwa hiyo, tungependa Serikali iyazingatie haya na iweze kuomba vyombo vyake viweze kufanya mpango wa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengine nitayaruka kwa sababu ya muda, lakini nichukue yale makubwa. Kulikuwa na swali kwamba, Manispaa Mpya, Miji na Wilaya Mpya, zisaidiwe kipekee kukamilisha ujenzi wa ofisi zao. Hili limeletwa hasa na Mheshimiwa Paul Kimiti; ametoa mfano kabisa kwamba, Jengo la Halmashauri ya Sumbawanga linahitaji shilingi milioni 500. Sasa kwa Manispaa mpya kuacha jengo na

hela zinakwenda kidogo kidogo, kwa utaratibu wetu ulivyo, majengo hayo si rahisi kukamilika na wakati mwingine unapewa labda shilingi milioni 50; unafanya kitu gani? Unapotaka kuweka zege, Waswahili wanasema zege halilali; sasa wewe una shilingi milioni 50, unahitaji shilingi milioni 100 kwa zege; siku hiyo utafanyaje? Kwa hiyo, ninadhani ni vizuri Serikali ikaangalia, labda kuwe na mpango kutoka kwenye vyombo vyetu pia kuonyesha *action plan*, lini wanahitaji na wanahitaji kiasi gani ili Serikali iangalie namna gani inaweza kuwasaidia. Hilo lipo pia kule kwangu Karatu, Jengo la Halmashauri lipo hivyo hivyo, karibu shilingi milioni 300 zinahitajika, ninadhani limesimama sasa kwa muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za miundombinu hasa barabara nazo zinakwenda kwenye utaratibu huo, unaomba fedha za kutengeneza barabara hasa Manispaa ambao wanaomba hela za kuweka lami, japo ni kidogo, lakini zikija kidogo kidogo, inakuwa ni vigumu kutekeleza mpango mliojipangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Paul Kimiti na Mheshimiwa Diana Chilolo, wamezungumzia sana suala la elimu *(capacity building)*, yaani kujenga uwezo wa Madiwani pamoja na Watendaji kwa ujumla na nitalirudia hilo baadae. Kulikuwa pia na swali la utaratibu wa kanuni kutoa Taarifa za Kamati kwamba, hautendi haki. Hili limezungumzwa na Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Mheshimiwa Omar Kwaangw'.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yatosha tu niseme hapa kwamba, Kamati hizi tatu; Kamati ya *PAC*, Kamati ya *POC* na Kamati ya *LAAC*, zinasimamia Serikali kwa niaba ya Bunge zima. Nimeacha kwa makusudi sehemu ya pili ya Ibara ya 63(2) kwamba, Bunge linasismamia na kushauri. Nimeacha kuzungumzia makusudi sehemu ya kushauri, kwa sababu hiyo kazi ya kushauri tunaifanya hapa Bungeni. Kamati kwa niaba ya Bunge zima, inafanya kazi ya kuisimamia Serikali. Sasa Kamati inaposimamia kwa niaba ya Bunge na inapoleta mapendekezo ndani ya Bunge, hatuhitaji kuiomba Serikali, hatutegemei hisani ya Serikali; ni wajibu wa Kikatiba kuisimamia Serikali, inapoelekezwa kufanya kitu ifanye kwa sababu huu ni wajibu wa Kikatiba. Katika hili, ninaomba Serikali ituelewe na tunapotoa mapendekezo, hatuhitaji katika hili kujadiliana kwa undani sana. Tunaelewa sisi ni Wabunge, Wazalendo na watu wa Taifa hili, pale inaposhindikana jambo, kukiwa na mawasiliano na sisi tunaelewa. Pale kunapokuwa na *communication*, sisi tunaelewa, lakini kama hakuna mawasiliano, mambo yameelekezwa, hakuna hatua zinazochukuliwa, ndiyo kitu ambacho Wabunge wanakilalamikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni muhimu nikaliunganisha na la Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu; tusipoiimarisha ofisi hii, hatuwezi kutegemea Kamati hizi tatu zikaisimamia Serikali. Kamati zinaweza kuwa ndani yake na wataalam wa aina mbalimbali; kuna wanasheria, wahandisi, watu wa elimu na watu wa afya kwenye Kamati zetu. Lakini, hizo hazisaidii peke yake, kwa sababu ukaguzi wa fedha wa vitabu na hata wa *performance audit*, unahitaji ofisi imara inayojitegemea, yenye fedha za kutosha ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu. Ninashukuru kwamba, Sheria hiyo (Muswada) tumeambiwa italetwa na ninadhani Wabunge watatusaidia katika kuiunga mkono ili ofisi hiyo iweze kupata fedha na kuweza kufanya kazi yake vizuri, isaidie Bunge letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Kamati kupewa meno, limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi.  Labda niseme hapa katika mchango mmoja wa maandishi nimepata mfano, inawezekana sisi Tanzania tunajifunga sana kwa mifumo tuliyonayo.  Watu wanafikiria kwamba, Kamati za Bunge kupata meno haiwezekani, kwa sababu majukumu haya ni ya Serikali.  Kuna nchi za wenzetu, nimepewa mfano kama ni wa kweli na ni sahihi ni vizuri tukauangalia na kujifunza. Kwa mfano, Uganda; Bunge la Uganda nimeambiwa kwamba, wao katika Sheria au Kanuni za Tozo, wanapokuta ukaguzi umefanyika na *CAG* ndiye anayekagua, *CAG* ndiye mtaalam, amekuta kuna upotevu wa wazi wa fedha, vifaa kwa mfano, vinavyotakiwa kupokelewa havikupokelewa au vimepokelewa kidogo au havikupokelewa kabisa, manunuzi ya ujenzi ni hewa, sasa hivi unangojea tena uchunguzi wa aina gani?  Haya ndiyo, mambo yanayoshangaza!

*CAG* ndiye mchunguzi kwa niaba ya Serikali, inawezekana ikatakiwa *special audit*, lakini nitaongezea sehemu nyingine pia kwamba, *CAG* hatafuti wizi kama wizi, lakini anapoonyesha kwamba kuna kitu hiki, vifaa havikupokelewa, fedha hazikupatikana, wanasema wenzetu kule wao wanakuwa na Polisi anakaa kwenye Kamati, ikishaamua kwamba hapa kumetokea wizi; ofisa anayehusika, pale pale anachukuliwa na Polisi na Sheria inachukua mkondo wake, siyo Bunge linachukua mkondo ni sheria inachukua mkondo wake, kwa sababu Polisi ni chombo kilichohalalishwa na sheria kumchukua anayehusika na mambo ya wizi, vitu ambavyo ni hewa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi tusione kwamba, haya tunakwenda na utaratibu wa Sheria au hatuko kwenye Utawala wa Sheria, haya ni mambo ambayo tunatakiwa kuyaangalia ili kuona ni namna gani tutaokoa fedha nyingi za Watanzania. Kama unazungumzia ufisadi, fedha zinazopotea kwenye Halmashauri, vitu ambavyo havipokelewi au madaraja ambayo hela zimetumika lakini madaraja hakuna, hapa unaeleza nini?  *CAG* alitupa mfano kule Tanga wa jengo ambalo hatimaye hata kile kilichojengwa kinatumika kama *bar*.  Sasa unapofikia hatua hii, unafanya kitu gani tena?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninadhani Serikali iliangalie hili na inapoleta kanuni kama tulivyoomba kanuni zetu zirekebishwe, tungependa katika Kanuni za Tozo, tuwe na meno makali zaidi na haya mambo yaweze kufanyiwa kazi inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mfuko wa Bunge ili Kamati zifanye kazi yake, ninaomba nilirudie; niungane na wale waliozungumza kwamba, fedha hizi zinazoombwa kuliwezesha Bunge, haziendi kwenye mifuko ya Wabunge, zinawasaidia Watanzania. Fedha zinazopotea kidogo kidogo, zimetumika kwenye mifuko labda ya watu au hazijulikani zimeenda wapi, ziweze kufuatiliwa kwenye *site* kwa ajili ya ukaguzi wa ufanisi *(performance audit).  Value for money* iweze kuonekana fedha zimekwenda wapi, watakaonufaika ni Watanzania siyo Wabunge.  Kwa hiyo, ninaomba huo utaratibu wa *National Audit*, Serikali isikie kilio hicho na Sheria hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu,

tunaomba iweze kufanya kazi ili mafungu hayo yanayokwenda chini ya *National Assembly Fund*, yaweze kufanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja ya utaratibu wa kulipa mishahara, imetoka kwa Mheshimiwa Jacob Shibiliti. Amesema kwamba, kuna utaratibu siku hizi tunalipa mishahara tunapokuwa tumeshinikizwa, ninadhani kuna mifano ya hivi karibuni, haiko hasa kwenye hoja yetu, lakini Wabunge wanaruhusiwa kujadili, pamoja na taarifa iliyoko sasa hivi ambayo wamekwisha kugawiwa, kuna mishahara inachelewa sana kulipwa hasa kwa walimu na wafanyakazi wa afya. Ninatoa mfano kwamba, mpaka waandamane au wagome, ndio hela inatolewa. Sasa unajiuliza, hivi baada ya kugoma kama hela zimepatikana, zilikuwa wapi kwanza; kwa nini siku mbili baada ya walimu kugoma, hizo fedha zimepatikana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wanauliza, hili ni suala la kulifanyia kazi, zinapokuwa zimepatikana, maana yake zilikuwa zimelala mahali. Sasa nani alikuwa anahusika mpaka walimu wameandamana au wamegoma au wafanyakazi wamegoma, maana yake taifa limepata athari, kwa muda walipogoma, kazi hazikufanyika, uzalishaji umesimama, kama ni kutoa elimu, *standard* ya elimu imeathirika. Yule mhusika ameachwa alivyo; nani amehusika na anachukuliwa hatua gani? Tungependa Serikali iyatazame mambo haya kwa umakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na suala ninadhani hili ni *specific* kabisa kwa Mheshimiwa Jacob Shibiliti, lakini lipo sehemu mbalimbali za nchi. Anasema, Serikali ilitangaza kupitia Bunge hili kuwa, utaratibu wa ushuru na kero ndogo ndogo ulifutwa. Ule ushuru *(collections)*, zile ambazo ziliitwa makusanyo ya kero, zimeanza kurudishwa kinyemela. Sasa kama zilitangazwa kupitia Bunge, kuwa Serikali iliziondoa kwa nchi nzima, zinaporejeshwa kinyemela, ninadhani Serikali lazima ifuatilie kuona kama maagizo yake yanatekelezwa. Ni nani huyu, baada ya Serikali na hasa Serikali ikitamka Bungeni ni nani anayerudisha tena haya ambayo yalipigwa marufuku na Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala kwa mfano la *barriers* kwenye barabara; Waziri Mkuu ninadhani wa awali aliwahi kutangaza kwamba, *barriers* kwenye barabara zimepigwa marufuku. Mheshimiwa Shibiliti anasema, kule kwake kuna kijiji kama sikosei ni Misasi, *barriers* hizo zimerudi. Mheshimiwa Waziri Mkuu, tangazo hili lilitolewa na wewe, ninadhani umelisikia. Agizo lako likikiukwa, wewe mwenyewe ndiye unayeweza kulirekebisha. Ninaomba liwe limesikika kwa utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa *performance audit* na *value for money*, ninadhani umezungumziwa na wengi hasa Mheshimiwa Mgana Msindai na Mheshimiwa Diana Chilolo, sitaki kulirudia, umuhimu wake unaeleweka. Suala la Madiwani na Watendaji wa Kata hasa kuhusu posho yao, nyenzo za kazi; Wabunge waliochangia kwa maandishi na hata Mheshimiwa Msindai, wamesema posho yao ni ndogo, kwa utaratibu wa sasa fedha nyingi sana za Serikali zinapelekwa kwenye Serikali za Mitaa. Fedha hizi zinasimamiwa na Madiwani na Watendaji katika ngazi ya vijiji, lakini hawa wanaozisimamia, maslahi yao ni madogo sana. Mimi mwenyewe juzi nilitembelea

kwenye Kata moja inaitwa Patembo kule Kiteto, nilianza kuzunguka toka saa tatu asubuhi mpaka saa 12 jioni, sikuimaliza. Una Mtendaji wa Kata na Diwani wamepewa Kata hii, sehemu kubwa ni msitu, hivi wanafanyeje kazi? Tunaiomba Serikali iangalie maslahi ya watu hawa, ambao wanafanya kazi nzuri sana, lakini maslahi yao kwa bahati mbaya ni mabaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hoja ya kusema tumechukua mfumo wa Madiwani kutoka kwa wenzetu Uingereza, ninafikiri Serikali iifikirie kauli hiyo mara mbili. Wenzetu wa Uingereza, anayeomba Udiwani ni mtu aliyetosheka. Hao waliotosheka Tanzania hatunao! Wanaoomba Udiwani ni watu wa kawaida kama sisi, wanahitaji na wao waishi, wana familia, wana watoto wanaosoma, wanataka wasaidiwe. Watendaji wetu wa Kata hivyo hivyo. Kwa hiyo, ninadhani hiyo hoja imefika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni uhamisho wa fedha, ameizungumza sana Mheshimiwa Msindai; fedha zinahamishwa kutoka akaunti moja kwenda nyingine na amesema ni haramu. Ninaomba nirudie kwamba, kwa kweli hiyo iwe haramu, kwa sababu mara nyingi zinahamishwa kutoka kwenye mfuko ambao unalenga maendeleo kama barabara, maji na afya, lakini zinatumika kwa usafiri au zinapelekwa kwenye *general fund* ambayo ni matumizi ya kawaida. Ninadhani ni vizuri sote tukatumia lugha moja, tukapiga kelele suala hilo likomeshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la nyumba za walimu ninadhani halihitaji mjadala. Taifa letu limewekeza fedha nyingi sana katika elimu. Ukitaka elimu usipomjali mwalimu, usitegemee kupata chochote hata ungejenga madarasa mazuri kiasi gani. Unahitaji kwanza mwalimu tena mwenye mazingira mazuri, unahitaji nyenzo za kufundishia, upate watoto, sasa nenda kwenye taratibu za kawaida za *syllabus* na kadhalika. Nyumba za walimu zinakatisha tamaa. Tunajua ni *priority*, Serikali inafanya jitihada kubwa, lakini tunapokuwa na jitihada hizi, hebu tujaribu kuangalia *priority* zetu, mengine tuyaache. Tumeshasema hivi, ukiacha kununua magari kwa kila Mkurugenzi wa Serikali, ukapeleka hela hizo hata kwa mwaka mmoja, nyumba ngapi za walimu utajenga? Ninadhani tulifanyie kazi hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vigezo anavyotumia *CAG*, limeshazungumziwa. *CAG* wa Fedha za wananchi ni nani? Ameuliza swali hili Mheshimiwa Omar Kwaangw' na ninaomba niliweke vizuri zaidi, tena niende mbele kuliko hata Mheshimiwa Kwaaangw'. Sijui kama tumegundua kwamba, tunapofanya *audit* hii ambayo inayoripotiwa, mara nyingi tunaishia kwa fedha zilizopelekwa na Serikali Kuu kwenda kwa Halmashauri. Kinachokaguliwa ni jinsi walivyopeleka wao kwenda chini. Zilivyopelekwa chini, mara nyingi ukaguzi wake hatuupati na taarifa nyingi zilizochambua kwenye *Local Government* zinaeleza hivyo. Ninadhani ni vyema suala hili Serikali ikaliwekea msisitizo na ikalitazama kwa jicho la huruma; namna gani hizi fedha tunazopeleka vijijini, zinaweza zikakaguliwa kwa utaratibu mzuri na tukajua tunapata *value for money*. Kamati inaweza kuangalia, lakini inaangalia baada ya kutumika. Tusipozisimamia na tukapata *feedback* nzuri, bado tunaweza kuwa na tatizo katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalam kukaa miaka kumi, Mheshimiwa Stephen Wassira amelijibu, ninashukuru sana. Ninadhani nisiongeze, lakini kikubwa pale ni kwamba, jitihada ziongezeke kwa kasi ya kuona hawa wasiendelee kukaa, kwa sababu wengine wanakaa eneo moja mpaka hata mawazo yao yanafanana na ya wananchi wa pale. Kama ni mwalimu amekaa, hana tofauti tena na wananchi katika kijiji kile, sasa inapoteza ile maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na fedha kutumika vibaya na hasa wananchi maskini na ametoa mfano aliyechangia, anasema hizi fedha za wananchi tunazopeleka, nyingine zinatumika vibaya, nyingine hatuzisimamii na nyingine hatutoi miongozo. Kwa mfano, mbolea ilikuwa shilingi 35,000 na sasa ni shilingi 75,000. Hivi huu umaskini kwa wananchi wa Tanzania tunauondoaje na akatoa mfano wa Mikoa ile ya Kusini; Iringa, Mbeya na Ruvuma. Sasa kama hii ni kweli, basi hii ni hali ya kutisha, ninadhani Serikali iangalie tunaweza kulidhibiti vipi hilo. Hii ni hoja iliyotolewa, sina takwimu ambazo nimezifanyia kazi wala Kamati haikulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hoja ya Serikali kutoa ahadi nyingi na haitoi majibu, kama nilivyosema, hatutegemei miujiza toka Serikalini, tunachotaka ni mawasiliano yawepo. Kama ni kweli jambo fulani haliwezekani, basi Bunge lipewe taarifa. Bunge hili ndilo lililotumika kuzindua Mkataba unaoitwa na Serikali, *Client Charter*. Sasa kama Mkataba huu ukizinduliwa Bungeni, tena tukatumia fedha nyingi sana kuuzindua; kama unasema ndani ya siku saba barua inajibiwa; kwa nini hata hoja hizi zisipate majibu angalau ndani ya muda mfupi tangu zilipopokelewa? Hata kama haiwezekani, ni kitu gani kinazuia? Sasa kama *Charter* ile haifanyi kazi kwa Bunge na kwa Wabunge, je, itafanyaje kazi kwa wananchi au kwa watumishi wa kawaida kule chini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kuwa, kuna hoja ya upelekaji wa ruzuku kwa kufuata mtiririko wa *bureaucracy* au umangimeza. Ninadhani Serikali iangalie ruzuku zinapopelekwa mtiririko ukoje. Baada ya Mheshimiwa Rais kubadilisha, kwa mfano, mfumo wa elimu na mambo kadhaa kuachiwa TAMISEMI, ninadhani ule mtiririko sasa utaangaliwa upya katika mfumo mpya unaotengenezwa. Kwa hiyo, ninadhani hilo lichukuliwe na Serikali.

Mheshimiwa Omar Kwaangw', anatoa taarifa kwamba, Kamati imetaja mambo maalumu kwenye shule yake na angependa tutoe taarifa kwamba, shule tuliyoisema ya Karesi amepokea taarifa mchana huu kutoka kwa Mkurugenzi wake na Eng. Kalobelo kwamba, Shule ya Msingi Karesi baada ya kutembelewa na Kamati ya Bunge na yeye mwenyewe kufuatilia tena, shule hiyo sasa imeanza kupauliwa. Tunamshukuru Mkurugenzi, kwa hatua alizochukua, lakini Kamati bado itapenda kupata taarifa ya maandishi watakapokuja mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuhusu gari la zimamoto, kwenye Taarifa ya Kamati tulisema kwamba, gari hilo liliahidiwa na Kamati ilipofika halikuonekana, ameletewa taarifa kwamba, taratibu zote za kupata gari hilo na kulifikisha Babati zimekamilika. Leo mchana walikuwa wanakamilisha usajili ili kupata namba ya gari na

tarehe 25 Aprili gari hilo linatarajiwa kufika Babati. Tunashukuru kwa hatua zilizofanyika, tunamshukuru pia Waziri wa Mambo ya Ndani, kwa taratibu zote alizofanya kuwezesha gari hiyo iweze kupata *clearance* zote zinazotakiwa kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na suala la *Special Audit* ya Wabunge wa Zanzibar, alizungumza sana Kiongozi wa Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kwamba, fedha zinazotengwa kwa ajili ya Wabunge kwa upande wa Zanzibar, hazijawahi kuwafikia Wabunge. Anauliza hizi fedha zimeenda wapi, tungependa suala hili lisiachwe, Wabunge wanapokuwa ndani ya Bunge wote wana hadhi sawa; Wabunge wa Zanzibar wana hadhi sawa kama wale wa Bara na kwa msingi huo, haki zile zinazotolewa kwa Wabunge ni lazima ziwe sawa. Kama kuna tatizo, tungependa fedha hizi zifanyiwe utaratibu na kwa bahati mbaya, Waziri anayehusika, hakujibu zaidi. Kwa kuwa kuna Waziri wa Fedha kule, sina uhakika kama angeweza kujibu, tungeomba hizo fedha zifanyiwe *Special Audit* kwa sababu ni za Jamhuri ya Muungano; Waziri wa Fedha na *CAG* wanawajibika kutolea taarifa hizo fedha zilikwenda wapi.

Baada ya kusema hayo, ninaomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge waliochangia na ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu lipitishe Azimio la Kukubali Taarifa na Mapendekezo ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa mwaka 2006/2007, kama ilivyo katika taarifa yetu ya kazi ya Kamati katika kitabu chetu ukurasa wa 27 hadi ukurasa wa 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninaomba pia nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, pamoja na Makamu Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Mgana Msindai, Wajumbe wa Kamati na Wabunge wote, kwa kazi nzuri waliyoifanya na hasa uwasilishaji mzuri alioufanya Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Baada ya kupokea hitimisho la hoja kutoka kwa Mwenyekiti, sasa Waheshimiwa Wabunge, ninaomba muiamue hoja ya kwamba, Bunge sasa lipokee na kuikubali taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa ya mwaka 2005/2006

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa )*

*(Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC)*
*ilipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, lipo suala moja lililojitokeza kwamba, muda wa kujadili taarifa hizo hautoshi na kwa kuwa wawasilishaji wa hoja hizo wamekuwa ni Wenyeviti wa Kamati na pia ni Wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya Bunge, nitawaomba mara tutakapokuwa kwenye kikao hicho, hoja hii ipate nafasi ya kujadiliwa na kuona ni namna gani utekelezaji wake, utakuwa ni mzuri zaidi na kuweza kuwasaidia Wabunge kutimiza kazi zao na kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

Waheshimiwa Wabunge, mnakumbuka kuwa leo asubuhi tulikuwa na uchaguzi wa wawakilishi katika vyombo viwili muhimu na niliwaahidi kwamba, washindi wetu watapata nafasi ya kusema maneno machache ya kushukuru kwa heshima waliyopewa na Bunge letu. Nitaanza kumwita Mheshimiwa Simbachawene, ambaye leo Bunge limempitisha kwa kura zote kuwa Mjumbe wa kuliwakilisha Bunge letu kwenye Bodi ya Ufundi Arusha na baadaye nitamwita Mheshimiwa Prof. Feetham Banyikwa, naye atafanya vivyo hivyo.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla, kwanza, ninayo heshima kubwa mbele yenu, kwa furaha niliyonayo nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini zaidi niwashukuru wote kwa uaminifu mkubwa mliouonyesha kwangu na kuniamini ili niweze kwenda kuwawakilisha katika Baraza la Chuo cha Ufundi cha Arusha. Ninapenda tniwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na Bunge zima kwa ujumla kwamba, niliomba nafasi hii kwa sababu nilijua nitamudu na kwa wale wasiofahamu, niwataarifu kwamba, mimi pia nimesoma katika Chuo kile kwa hiyo, ninayafahamu matatizo ya Chuo kile. Vilevile nimepata fursa hii ya kuwa Mbunge na hivyo nimezifahamu sera kwa uzuri sana za mambo ya ufundi katika nchi yetu.

Waheshimiwa Wabunge, sipendi niwachoshe, ninawashukuru sana kwa uaminifu mkubwa mlionionyesha nami sitawaangusha. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninashukuru sana Mheshimiwa George Simbachawene. Nami kwa niaba ya Spika, ninaomba nichukue nafasi hii, kukupongeza sana kwa ushindi ulioupata siku hii ya leo.

**MHE. PROF. FEETHAM F. BANYIKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Naibu Mawaziri na Wabunge wenzangu; kwanza kabisa, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Ngara, ninapenda kutoa ahsante sana kwa kunipa kura zenu zilizonipa ushindi. Vilevile nimpe hongera Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, kwa ushindani mzuri. Kampeni zilifanywa kistaarabu kwa vile sote tulitumia barua kuombea kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kunichagua kuwa Mbunge wa Bunge la Afrika, inaonyesha kwamba, Wabunge wenzangu mnaimani na ninapenda kuwahakikishia kwamba, nitaifanya kazi hii mpya kwa nguvu zangu zote nitakazopewa na Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana, ninapenda kuwaahidi ya kwamba, sitawaangusha; nitapokea mawazo yenu na nitayapeleka katika Bunge la Afrika na nitakapopata majibu, nitayawasilisha hapa Bungeni.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Prof. Banyikwa. Umesahau kutambua kwamba, Rais wa Bunge hilo yupo hapa ndani leo, kwa hiyo, ninafikiri amekupokea na amezingatia ushindi wako wa leo.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba niseme kwamba, suala lililojitokeza leo kama nilivyosema, kwa mujibu wa Kanuni namba 64(4), nitalitolea maamuzi kwa wakati nitakaoona unafaa. Ninaomba niwashukuru kwamba, tumeweza kushirikiana vyema katika shughuli zote tulizozipanga kwa siku hii ya leo, zilikuwa nyingi lakini tumeweza kumaliza yale yote tuliyoyapanga.

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe Wabunge wa CCM kwamba, kikao chao kipo kama kilivyotangazwa. Baada ya kusema hayo, ninaomba sasa niliahirishe Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. Ahsanteni sana.

*(Saa 01.41 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi, Tarehe 24 Aprili, 2008 Saa 3.00 Asubuhi)*